ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

MHE. PANDU AMEIR KIFICHO - SPIKA

1.Mhe. Balozi Seif Ali Iddi	MBM/Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa na Rais
2.Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Jimbo la Dimani.
3.Mhe. Omar Yussuf Mzee	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo/ Kuteuliwa na Rais
4.Mhe. Haji Omar Kheri	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora/Jimbo la Tumbatu
5.Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais/Kuteuliwa
6.Mhe. Mohammed Aboud Mohammed	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa
7.Mhe. Abubakar Khamis Bakary	MBM/Waziri wa Katiba na Sheria/Jimbo la Mgogoni.
8.Mhe. Hamad Masoud Hamad	MBM/Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Ole.
9.Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Kuteuliwa
10.Mhe. Juma Duni Haji	MBM/Waziri wa Afya/Kuteuliwa
11.Mhe. Zainab Omar Mohammed	MBM/Waziri wa Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto/Kuteuliwa
12.Mhe. Abdillah Jihad Hassan	MBM/Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo/Jimbo la Magogoni
13.Mhe. Ali Juma Shamuhuna	MBM/Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Jimbo la Donge.

14.Mhe. Mansoor Yussuf Himid	MBM/Waziri wa Kilimo na Maliasili/Jimbo la Kiembesamaki
15.Mhe. Nassor Ahmed Mazrui	MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Mtoni
16.Mhe. Said Ali Mbarouk	MBM/Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Gando
17.Mhe. Haroun Ali Suleiman	MBM/Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika/Jimbo la MaMakunduchi
18.Mhe. Suleiman Othman Nyanga	MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Jang'ombe
19. Mhe. Haji Faki Shaali	MBM/ Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Mkanyageni
20.Mhe. Machano Othman Said	MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Chumbuni.
21.Mhe. Othman Masoud Othman	Mwanasheria Mkuu
22.Mhe. Issa Haji Ussi	Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Chwaka
23.Mhe. Zahra Ali Hamad	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Nafasi za Wanawake
24.Mhe. Dr. Sira Ubwa Mamboya	Naibu Waziri wa Afya/Kuteuliwa na Rais
25.Mhe. Bihindi Hamad Khamis	Naibu Waziri wa Habari,Utamaduni,Utalii na Michezo/ Nafasi za Wanawake
26.Mhe. Haji Mwadini Makame	Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Jimbo la Nungwi
27.Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi	Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Fuoni
28.Mhe. Abdalla Juma Abdalla	Jimbo la Chonga
29.Mhe. Abdalla Moh'd Ali	Jimbo la Mkoani
30.Mhe. Abdi Mosi Kombo	Jimbo la Matemwe
31.Mhe. Ali Abdalla Ali	Jimbo la Mfenesini

32. Mhe. Ali Salum Haji	Jimbo la Kwahani
33. Mhe. Ali Mzee Ali	Kuteuliwa na Rais
34 .Mhe. Amina Iddi Mabrouk	Nafasi za Wanawake
35. Mhe. Asaa Othman Hamad	Jimbo la Wete
36.Mhe. Asha Abdu Haji	Nafasi za Wanawake
37.Mhe. Asha Bakari Makame	Nafasi za Wanawake
38.Mhe. Ashura Sharif Ali	Nafasi za Wanawake
39.Mhe. Bikame Yussuf Hamad	Nafasi za Wanawake
40.Mhe. Farida Amour Mohammed	Nafasi za Wanawake
41.Mhe. Fatma Mbarouk Said	Jimbo la Amani
42.Mhe. Hamza Hassan Juma	Jimbo la Kwamtipura
43.Mhe. Hassan Hamad Omar	Jimbo la Kojani
44.Mhe. Hija Hassan Hija	Jimbo la Kiwani
45.Mhe. Ismail Jussa Ladhu	Jimbo la Mji Mkongwe
46.Mhe. Jaku Hashim Ayoub	Jimbo la Muyuni
47.Mhe. Kazija Khamis Kona	Nafasi za Wanawake
48.Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa	Jimbo la Kikwajuni
49.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk	Jimbo la Kitope
50.Mhe. Mbarouk Wadi Mussa	Jimbo la Mkwajuni
51.Mhe. Mgeni Hassan Juma	Nafasi za Wanawake
52.Mhe. Mlinde Mbarouk Juma	Jimbo la Bumbwini
53.Mhe. Mohammed Haji Khalid	Jimbo la Mtambile
54.Mhe. Mohammed Mbwana Hamad	Jimbo la Chambani

55.Mhe. Mohammed Said Mohammed Jimbo la Mpendae

56. Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak Nafasi za Wanawake

57.Mhe. Mussa Ali Hassan Jimbo la Koani

58. Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali Jimbo la Uzini

59.Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa Nafasi za Wanawake

60.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi Nafasi za Wanawake

61.Mhe. Nassor Salim Ali Jimbo la Rahaleo

62.Mhe. Omar Ali Shehe Jimbo la Chake-Chake

63.Mhe. Panya Ali Abdalla Nafasi za Wanawake

64.Mhe. Rashid Seif Suleiman Jimbo la Ziwani

65.Mhe. Raya Suleiman Hamad Nafasi za Wanawake

66.Mhe. Rufai Said Rufai Jimbo la Tumbe

67.Mhe. Saleh Nassor Juma Jimbo la Wawi

68.Mhe. Salim Abdalla Hamad Jimbo la Mtambwe

69.Mhe. Salma Mohammed Ali Nafasi za Wanawake

70.Mhe. Salma Mussa Bilali Nafasi za Wanawake

71.Mhe. Salmin Awadh Salmin Jimbo la Magomeni

72.Mhe. Shadya Mohamed Suleiman Nafasi za Wanawake

73.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha Jimbo la Mwanakwerekwe

74. Mhe. Shawana Bukheti Hassan Jimbo la Dole

75.Mhe. Subeit Khamis Faki Jimbo la Micheweni

76.Mhe. Suleiman Hemed Khamis Jimbo la Konde

77.Mhe. Ussi Jecha Simai Jimbo la Chaani

78.Mhe. Viwe Khamis Abdalla	Nafasi za Wanawake
79.Mhe. Wanu Hafidh Ameir	Nafasi za Wanawake
Ndg. Yahya Khamis Hamad	**Katibu wa Baraza la Wawakilishi**

Kikao cha Kwanza – Tarehe 28 Machi, 2012

(Kikao kilianza Saa 3.00 Asubuhi)

DUA

Mhe. Spika, (Pandu AmeirKIficho) alisoma dua

Kiapo cha Uaminifu

Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali:

(Aliapa kiapo cha uaminifu na kukaa katika sehemu yake).

Mhe. Spika: Waheshimiwa wajumbe ahsanteni sana Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali tayari amechukua nafasi yake katika ukumbi huu karibu sana.

TAARIFA YA SPIKA

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, kwanza nichukue nafasi hii kukurejesheni tena katika shughuli zetu za mkutano wa saba unaoanza leo tarehe 28/03/2012. Katika kipindi kilichopita kabla ya mkutano huu tulipata msiba mkubwa kwetu wa kifo cha Ndugu yetu mwenzetu, aliyekuwa Muwakilishi wa Jimbo Bububu Mhe. Salum Amour Mtondoo.

Waheshimiwa wajumbe naona nichukue nafasi hii kutoa taarifa rasmi kwenu juu ya msiba huu, mnamo siku ya Alhamis tarehe 15/03/2012 tulipokea taarifa ya kusikitisha ya kifo cha Mheshimiwa Salum Amour Mtondoo aliyekuwa Mwakilishi wa Jimbo la Bububu Zanzibar kwa tiketi ya chama cha Mapinduzi, alifariki dunia kwenye hospitali ya Mnazi Mmoja ambako alilazwa kwa ajili ya kupatiwa matibabu, kabla ya kupelekwa kwenye Hospitali ya Mnazi Mmoja marehemu alizwa kwenye hospitali ya Jeshi la Wananchi Tanzania hapo Bubunu mjini Unguja kwa siku moja.

Marehemu baadae alihamishiwa hospitali ya Mnazi Mmoja kwa ajili ya kuendelea na matibabu, marehemu alizikwa siku ya ijumaa tarehe 16/03/2012 huko kijijini kwako Bumbwini Misufini Wilaya ya Kaskazini (B) Mkoa wa Kaskazini Unguja.

Mhe. Salum Amour Mtondoo alizaliwa tarehe 14/12/1962 hapo Bububu Wilaya ya Magharibi Zanzibar, alipata elimu yake ya msingi na sekondari katika skuli ya Bububu kuanzia mwaka 1969 hadi mwaka 1979, alijishughulisha na kazi mbali mbali kwa kujitafutia riziki kabla ya kuwa mwanasiasa zikiwemo kazi za ajira na biashara. Katika shughuli za kisiasa Marehemu aliwaki kuwa mjumbe wa Kamati ya Siasa ya Tawi la CCM Bububu na mjumbe wa jumuiya ya wazazi wa Chama cha Mapinduzi Wilaya na Mkoa.

Mhe. Salum Amor Mtondoo alichaguliwa kuwa mjumbe wa Baraza la Wawakilishi wa Jimbo la Bububu katika uchaguzi mkuu wa Zanzibar uliofanyika Oktoba mwaka 2010, katika Baraza la

Wawakilishi alikuwa ni mjumbe wa kamati ya kudumu ya Mawasiliano na Ujenzi. Katika kipindi hicho kifupi aliwakilisha vyema wananchi wa jimbo lake na alifanya vyema kazi hiyo kwa uadilifu na ushirikiano mkubwa pamoja na wananchi wa jimbo lake na wajumbe wenzake wa baraza hili.

Mwenyezi Mungu aiweke roho ya Marehemu mahali pema peponi Amin.

Waheshimiwa wajumbe kwa heshima na taadhima nakumbeni basi tusimame kwa dakika moja mara baada ya kumaliza maelezo haya ili tuweze kumkumbuka mwenzetu na kumuombea dua katika ukumbi huu. Waheshimiwa wajumbe tusimame kwa dakika moja.

(Hapa Waheshimiwa wajumbe walisimama kwa dakika moja na kuomba dua)

Waheshimiwa wajumbe katika msiba huo sio tu kwamba umetugusa sisi lakini pia umewagusa wananchi wa jimbo la Bububu na jamaa wa marehemu, lakini vile vile ndugu zetu, wenzetu, rafiki zetu mbali mbali ambao msiba huu pia nao umewagusa, katika salamu ambazo tumepokea kwa ajili ya kuungana nasi katika rambi rambi zinatoka kwa taasisi mbali mbali zikiwemo salamu kutoka kwa Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Jakaya Mrisho Kikwete na kiongozi wa kampuni ya Aliyousuf Establishment Shehe Abdalla Mohammed Aliyousuf na rafiki zetu wa Arusha Wazee Club.

Wengine kati ya hao walituma salamu zao kwa maandishi na kwa ruhusa yenu waheshimiwa wajumbe naomba nisome salamu za Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Jakaya Mrisho Kikwete ambazo zimesomeka kama ifuatavyo.

Mhe. Pandu Ameir Kificho Spika wa Baraza la Wawakilishi Zanzibar nimepokea kwa mshituko na masikitiko na hudhuni kubwa taarifa ya kifo cha Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi wa jimbo la Bububu kupitia kiti cha CCM Mhe. Salum Amour Mtondoo kilichotokea jana kwa siku hiyo ilikuwa Alhamis tarehe 15 March, 2012.

Kifo chake kimetokea wakati ambapo uongozi na utumishi wake ulikuwa bado unahitajika sana na wananchi wa jimbo lake katika Baraza la Wawakilishi Zanzibar na Tanzania kwa jumla, Chama chetu cha CCM hiyo ni kauli ya Rais kimepoteza mwanachama shupavu kada na kiongozi hodari hakika sote tumepotelewa na mtu wa kutumainiwa ambae pengo lake sio rahisi kuliziba.

Mhe. Spika, nachukua nafasi hii kukutumia wewe salamu za rambi rambi kufuatia msiba huu mkubwa uliotukuta kupitia kwako naomba unifikishie salamu kwa wajumbe wote wa Baraza la Wawakilishi, wananchi wa jimbo la Bububu na familia ya marehemu, kwa familia ya marehemu nawaambia kuwa tupo pamoja nao katika kpindi hiki kigumu kilichojawa na majonzi tele. Majonzi yao na machungu yao ni yetu sote nawaomba wawe na moyo wa subira na kumshukuru Allah Subhana Wataala kwa muda aliojaalia kuwa nae hapa duniani na kwa mchango aliotowa kwa kuendeleza familia sote tumuombee kwa mwenyezi mungu amjaalie mapumziko mema na pepo yake siku yake kiama inshaalla.

Jakaya Mrisho Kikwete Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Waheshimiwa wajumbe naomba kuzitoa salamu hizo kwenu kutokana na msiba ambao ni wetu sote.

Salama nyengine kama nilivyosema zimeletwa na Jumuiya ya Aliyousuf haina haja ya kuzisoma lakini pia naomba mzipokee salamu hizo kwa ndugu yetu, mwenzetu ambae ameungana nasi katika msiba huo mzito.

Lakini bila ya kusahau Waheshimiwa wajumbe pia naomba mpokee salamu za rambi rambi za ndugu zetu wa *Wazee Arusha Club* ambao wao walinitumia meseji kwenye simu yangu wakiungana nasi katika msiba huo mkubwa.

Waheshimiwa wajumbe nakushukuruni kwa kupokea salamu hizo za rambi rambi.

Baada ya hapo nichukue nafasi hii kumkaribisha rasmi ndugu yetu ambaye tayari ameshakula kiapo hivi punde na nimuombe basi afanye kazi yake kama mwakilishi kwa mujibu wa taratibu za katiba, sheria zana ambazo tumemkabidhi azifanyie kazi zana hizo. Kwa hivyo nikuombeni waheshimiwa wawakilishi wote pamoja na Mawaziri tushirikiane nae ili kufanikisha kazi yake kama muwakilishi wa jimbo la Uzini. *(Makofi)*

Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali karibu sana katika shughuli zetu za Baraza.

Waheshimiwa Wajumbe ahsanteni sana *(Makofi)*

HATI ZA KUWASILISHA BARAZANI:

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, naomba kuwasilisha mezani nakala zote za Gazeti Rasmi la Serikali pamoja na vijalizo vyake kuanzia tarehe 28 Januari, 2012.

Mhe. Spika, naomba kuwasilisha.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kuwasilisha mezani hotuba ya majumuiyo ya Mswada wa Sheria ya kufuta Sheria ya Ulipaji wa Mafao kwa Viongozi wa Kitaifa No. 4 ya mwaka 1988 na Sesheria ya Viongozi wa Kisiasa Nam. 6 ya mwaka 1999 na kutunga Sheria Mpya ya Maslahi na Mafao ya Viongozi wa Kisiasa baada ya Kustaafu Pamoja na marekebisho yake na mambo mengine yanayohusiana na hayo.

Mhe. Hamza Hassan Juma (Mwenyekiti wa Kamati ya Kusimamia Viongozi Wakuu wa Kitaifa): Mhe. Spika, kwa niaba ya kamati yangu ya kusimamia Afisi Viongozi Wakuu wa Kitaifa naomba kutoa taarifa kwamba kwa kuwa mswada huu ulishasomwa na taarifa ya kamati tumekwisha kusoma na ilikuwa bado tu Mhe. Waziri kufanya majumuisho.

Kwa hivyo kwa msingi tunashukuru kwa busara alizotumia Mhe. Waziri aliita tena kamati yangu tukakaa tukakubaliana na kimsingi mengi ambayo tumemshauri katika kamati ameyakubali kwa

hivyo kamati yangu haina pingamizi na waheshimiwa wajumbe naomba tuendelee kuunga mkono mswada huu. Ahsante sana.

Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Rais Fedha Uchumi na Mipangi ya Maendeleo: Mhe. Spika, kwa idhini na kwa ruhusa yako naomba kuwasilisha mezani Mswada wa Sheria wa Kufuta Sheria ya Tume ya Mipango Nam.5 ya mwaka 1989 na kutunga sheria mpya kwa ajili ya uendeshaji wa Tume ya Mipango Zanzibar kazi zake, uwezo wake na mambo mengine yanayohusiana na hayo. Mhe. Spika, naomba kuwasilisha.

Mhe. Abdalla Mohammed (Kny: Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha Biashara na Kilimo) Mhe. Spika, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Mwenyekiti wa kamati naomba kuwasilisha hati mezani hotuba ya maoni kuhusu Mswada wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Tume ya Mipango Nam. 5 ya mwaka 1989 na kutunga Sheria Mpya ya Mipango ya Zanzibar, kazi zake, uwezo wake na mambo mengine yanayohusiana na hayo naomba kuwasilisha.

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 42

Matumizi ya Michango ya *Mv Spice Islander*

(Mheshimiwa aliyeuliza swali hili baada ya kupata ufafanuzi ameliondosha swali hili).

Nam. 1

Wananchi Wanaofanya Kazi Nje na Mipango ya Maendeleo

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa (Kny:Mohammed Said Mohammed -Aliuliza:

Maendeleo ya nchi yanatokana na juhudi na michango ya wananchi kwa ujumla wao ikiwa ni pamoja na wanaoishi na kufanyakazi nje ya nchi.

Je, mpango wa wananchi Zanzibar wanaofanya kazi nje ya nchi unajitokeza wapi katika mipango yetu ya maendeleo.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi:Alijibu:

Mhe. Spika, Naomba kumjibu Mheshimiwa Mwakilishi swali lake namba 1 kama ifuatavyo:-

Mchango wa Wanzanzibari wanaoishi nje ya nchi katika mipango yetu ya maendeleo imepewa umuhimu mkubwa katika maendeleo ya nchi yetu na imeainishwa katika Mpango Mkuu wa Kitaifa. Vile vile, katika utekelezaji wa mikakati ya mpango wa kati imeelezwa wazi wazi jinsi Zanzibar itakavyoweza kutumia michango hiyo katika maendeleo yake.

Kwa hivi sasa Mhe. Spika, hatuna takwimu sahihi za michango ya Wazanzibar wanaochangia moja kwa moja katika maendeleo ya nchi, lakini zaidi nataka kusema tuna kitengo kipya hiki

ambacho tumekifungua katika Wizara yetu ya Nchi Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi katika Idara ya uhusiano wa kimataifa, sasa tutatoka kuwashajihisha wazanzibar walioko nje washiriki kikamilifu katika michango hasa katika kuleta miradi ya maendeleo moja kwa moja na pia katika kuwekeza hapa nchini kwetu.

Lakini pia tumegundua kwamba kuna Wazanzibari wengi sana ambao wanawaletea ndugu zao waliopo hapa fedha za kuendeshea maisha yao, mbali ya wanaopitisha kwenye benki zetu lakini hata kwenye ma burade change mengi sana tumefuatilia, lakini zile ni siri na si vizuri kwenda kufuatilia na wale hawakupi hesabu hasa.

Sasa kwa umumla ninichosema kwa siku za usoni tutajitahidi hata kwenda kuwatembelea na tumeshapanga kwenda kuwatembelea katika bara kama la Ulaya. Asia na Arabuni ili kuwashajihisha Wazanzibar walioko kule kuja moja kwa moja kuwekeza na pia kuchangia maendeleo ya nchi yetu.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Mhe. Spika, nashukuru pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza suala moja la nyongeza.

Mhe. Waziri katika jibu lake mama ametwambia kwamba hana data ambazo za uhakika za kutueleza.

Je, Mhe. Waziri haoni kama huo ni udhaifu wa Wizara yake.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi - Alijibu**:** Kama nilivyosema uletwaji wa fedha nchini na Wazanzibari walioko nchi za nje hizo ni siri zao, tumejaribu kwenda kama Postal Bank na kwenye Burade Change hatukuweza kuzipata na hiyo ni siri, hawezi kukwambia mimi nafanya lakini tunashirikiana na Wizara ya Fedha angalau tupate kwa mwaka huu ngapi, lakini kukwambia moja kwa moja wanahisi ni suala la ndani.

Lakini tunashukuru kwamba kazi hiyo inafanywa sana na Wazanzibari wengi sana wamekuwa wanafaidika na suala hilo, mimi sifikirii kama hilo ni udhaifu wa Wizara, kama nilivyosema tumefuatilia lakini tatizo kidogo ni suala nyeti na linawahusu wenyewe ndani.

Mhe. Omar Ali Shehe: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza suala moja la nyongeza lenye kifungu a na b.

Mhe. Spika, katika mipango ya maendeleo utafiti ni kitu cha msingi sana, kama hivyo ndivyo.

(a) Je, serikali imeandaa mpango gani wa kufanya utafiti kwanza kwa kuwatambua hawa Wazanzibari wenyewe.

(b) Kufahamu uwezo wao wa kiuchumi walionao. Lakini kama hilo halijafanyika Mhe. Waziri huhisi kuwa bila ya kufanya utafiti itakuwa tunafanya mipango hewa katika uchumi wa nchi yetu.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Spika, nakubaliana na Mhe. Omar kwamba suala la utafiti ni suala la msingi. Na katika maendeleo yoyote msingi mzuri ni ule unaojengwa baada ya kufanya utafiti. Kwa hivyo mimi nakubaliana na wazo lake kwamba Wizara tufanye utafiti na kuwatambua hawa vatu wetu. Niseme shauri hili tumeshaanza kulitekeleza. Kama nilivyosema mbali ya ziara za viongozi wetu wakuu wanaokwenda huko, wanakutana na Wazanzibari ambao tayari wapo nchi za nje na wenye uwezo ili kuwashawishi wawekeze hapa na kuleta rasilimali zao.

Lakini sisi pia kama Wizara kama nilivyosema tumeshajipangia ndani ya mwaka huu wa fedha kabla haujamalizika tutajitahidi au mapema katika kipindi kijacho cha Bajeti basi tuweze kutoka. Kama nilivyosema tutawafuata Wazanzibari wengi walioko kama mfano Uingereza, Canada, Denmark, lakini pia hata upande wa *Block* ya Arabuni na hata Asia tutawafuata kujaribu kuwatambua. Lakini vile vile tunao Wazanzibari wengi ambao wamesharudi hapa. Tunashukuru na wao wana misingi mizuri tutawatumia watusaidie kuweza kuwatambua na kuwavuta hao wengine waliokuwepo nchi za nje, tunashukuru sana.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Spika, nakushukuru kunipa nafasi hii nikamuuliza Mhe. Waziri suala langu dogo la nyongeza kama hivi ifuatavyo:

Mhe. Spika, katika nchi inayofuata utawala wa kisheria suala zima la kuletwa fedha kwa njia ya panya inakuwa siyo ruhusa. Mhe. Spika, tumepitisha sheria ya *Money Laundring* hapa, lakini vile vile na hivi karibuni tumepitisha Mswada wa Rushwa na moja katika vipengele vya sheria hiyo vinazungumzia mtu kuangalia mali zake alizozichuma na uwezo wake.

(a) Je, Serikali yetu haioni kwamba kuendelea kuwaruhusu watu kuletewa fedha, hatujui kwamba fedha hizi zinakuja kwa njia gani na wanazipata kwa njia gani. Hatuoni sasa hivi tunarudi katika ile sheria ili kudhibiti uingizaji wa fedha ambao usiokuwa wa kihalali.
(b) Hawa Wazanzibari ambao sasa hivi katika suala zima la Serikali Diaspora, kutafuta wale Wazanzibari waliokuwepo nje kuweza kusaidia uchumi wetu. Lakini je, kuna jitihada gani tulizozichukua kwa Wazanzibari hawa hawa wenye uwezo kuweza kuwasaidia Wazanzibari wenzao waliokwama ambao wanataka kurudi kwao.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Spika, ni kweli kwamba hivi karibuni tumepitisha sheria ile ya kuzuia rushwa. Pia nakubaliana na yeye kwamba si vizuri kuwadadisi watu katika mali zao. Lakini sheria tumeshaipitisha hapa Barazani na tumeipitisha na tulizungumza sana suala hili la vipi wale ambao watadhaniwa labda wamejipatia mali bila ya utaratibu unaofahamika njia gani itumike.

Mhe. Spika, nafikiri sote tutakubaliana na Mhe. Hamza pia atakubaliana na mimi, majadiliano yalivyokwenda hapa. Hili tulisema ni suala nyeti lakini kwa wenyewe watu wa sheria walipendekeza jinsi watakavyokwenda kutafuta au kutafiti watu ambao wanahisi kwamba wamepata mali kwa njia ambayo kidogo inatia wasi wasi.

Pia nakubaliana na wewe kwamba kweli kunasheria ile ya *Anti Money Laundring*, sisi Zanzibar kwa *investment* ilivyokuwa kubwa kwa ghafla moja, walitutia wasiwasi wenzetu, kwamba labda hapa kuna mapesa mengi yanaingia kwa kughushi na si halali. Lakini tunashukuru serikali yetu

kupitia Afisi ya Mwanasheria Mkuu, kupitia Afisi ya Wizara ya Fedha, kwa kweli tulisimama kidete, tukasaidiana kutengeneza sheria ile na pia tuliipitisha hapa. Kwa hivyo nafikiri mimi kama kazi hii itaendeshwa kama inavyopaswa nafikiri haitaleta wasi wasi.

Wazanzibari waliokwama ambao wanataka kurudi. Nakubaliana na wewe ni kweli wapo kwa sababu Mhe. Hamza najua yeye ni wa kimataifa anakwenda sana kule Bangalore na kwengineko anawakuta. Sasa naomba tusaidiane anapowabaini hawa, ili tuzungumze na Wizara ya Mambo ya Nchi za Nje, wao ndio dhamana. Sasa wao tutashirikiana vipi jinsi ya kuwakwamua. Si jambo zuri kwamba kweli Watanzania au Wazanzibari wadhalilike huko nchi za nje. Naomba tusaidiane hili ili tuwakwamue waje zao hapa kuliko kufungwa kule na kuteswa. Ahsante Mhe. Spika.

Nam. 2

Kufungwa Barabara ya Bandarini – Forodhani

Mhe. Jaku Hashim Ayoub - Aliuliza:

Katika Mkutano wake wa Oktoba 2011, Serikali ilikubali kuwa hakuna sababu ya msingi kufungwa kwa barabara inayotoka kwenye *"round about"* ya bandarini Zanzibar kuelekea Jumba lililokuwa la kulelea watoto la Forodhani, na kwamba Serikali iliahidi kuifungua barabara hiyo mara moja. Lakini hali halisi ni kuwa baraba hiyo hadi sasa hivi bado imefungwa.

(a) Je, Mhe. Waziri, kwa mwenendo huu tunatakiwa tuielewe vipi Serikali.

(b) Ni lini Wizara yako itakuwa imetekeleza ahadi yake hii ya kuwaondoshea usumbufu usio wa lazima wananchi wanaotumia barabara hiyo.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi -Alijibu:

Mhe. Spika, naomba kumjibu Mheshimiwa Mwakilishi swali lake nam. 2 lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Kwanza naomba kusisitiza tena hili neno la kufunga barabara. Nafikiri niliwahi kuulizwa swali hili na nikasema serikali haikuifunga barabara ile. Lazima tutafautishe kati ya kufunga na kuruhusu gari kupita njia ya mkondo mmoja. Naomba kusema kwamba serikali haikufunga barabara ile.

(a) Barabara anayoizungumza Mheshimiwa kutoka kwenye *round about* ya Bandari ya Zanzibar hadi Forodhani katika jumba la kulelea watoto zamani kwa nia njema kabisa tumefanya hiyo *one way* kwa kudhibiti msongamano wa magari katika Mji Mkongwe. Hili suala tumeshirikiana pamoja na Mamlaka ya Mji Mkongwe, Wizara ya Mawasiliano, Polisi Trafic na sisi Tawala za Mikoa. Hii inatokana na mpango wa kuulinda na kuuhifadhi Mji Mkongwe ambao unaelekeza kwamba mpango wa matumizi ya barabara uwe wa njia moja ili uweze kuendelea kukubalika kuwa ni mmoja wa miji ya urithi wa dunia. Tukumbuke ya kwamba mwaka 2000 Mji Mkongwe

ambao ni miongoni mwa miji maarufu duniani, ulisajiliwa na kutambulikana na Umoja wa Miji ya Kale duniani.

(b) Serikali kupitia Mamlaka ya Hifadhi ya Mji Mkongwe imo katika hatua za mwisho za kukamilisha utayarishaji wa mpango wa Mji Mkongwe wa Kudhibiti Magari. Mpango huo unaelekeza kuwepo kwa njia moja tu ya kuingilia Mji Mkongwe kwa kupitia Shangani ili tuweze kupunguza msongamano wa magari ndani ya Mji Mkongwe na kupunguza athari za uharibifu wa nyumba ambazo ni tete, chakavu na za kale zilizokuwepo karibu na barabara hizo. Ahsante.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Spika, nakushukuru Mhe. Waziri kwa majibu yako mazuri. Kiongozi ni kiyoo na muangaza wa jamii, maneno anayoyasema kuna watu nyuma yake humfuata, kiongozi hatakiwi kuwa na kauli mbili, hasa kutokana na dini yetu ya Kiislamu. Umetoa kauli kutokana na Kikao cha Oktoba kilichopita naomba nikinukuu kurudia tena katika Hansard ya Kikao cha Pili tarehe 13, Oktoba. Magari yanayokuja mpaka Ngomekongwe kuna parking nzuri ya Forodhani kwa hivyo anaweza kuja mpaka huko. Hiyo tumeikubali, swali langu lipo hapa.

Je, kauli yako ipo vile vile na tumeikubali na ulitoa ahadi kuwa itafunguliwa njia ile lakini mpaka leo kibao hakijaondoshwa katika mti ule Msikiti wa Ijumaa.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Spika, ni kweli kwamba katika Kikao kilichopita nilitoa kauli hiyo ya kwanza kwamba tukafanye utafiti na nilimualika Mheshimiwa Mwenzangu aliyeuliza swali lile tuende tukafanye utafiti wa kuona vipi ile *movement* ya trafic iliyopo halafu kama taratibu au sheria zitaruhusu tuweze kufungua. Lakini baada ya kufanya mashauriano na vyombo vingine nilivyovitaja wamesema kwamba hilo haliwezekani kwa taratibu zilizowekwa.

Kwa hiyo mimi nakubali kwa nia safi kabisa, sikupinga moja kwa moja na hiyo ni kawaida, wewe kwanza uchukue kauli uwe *positive* halafu ukalifanyie kazi. Sasa kwenda kulifanyia kazi imekuwa *bad* kwa mujibu wa taratibu zilizokuwepo. Ahsante.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Spika, nakushukuru naomba kuuliza swali dogo la nyongeza kwa Mhe. Waziri. Kwa sababu katika majibu yake amesema kwamba sababu kuu zilizopelekea kufanya njia hii kwa njia moja tu ni kudhibiti uingiaji wa magari na kupunguza mtetemeko ambao unaweza kuathiri majumba ya Mji Mkongwe.

Lakini katika utekelezaji wa agizo hili imepelekea kuwa na msongamano mkubwa zaidi kuliko uliokuwepo mwanzo hasa nyakati ambapo maboti yanayotoka Dar-es-Salaam yanaingia Zanzibar na kusababisha magari kukaa kwa muda mrefu yakiwa bado yapo katika moto. Kwa hivyo kama suala linalosababisha msongamano, msongamano umekuwa mkubwa zaidi. Lakini kwa magari yale kubakia katika moto na kubakia katika barabara kwa muda mrefu haoni kama inaongeza mtetemeko na hivyo kufanya lile lengo lililokusudiwa lifikie kinyume chake.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Spika, kabla sijamjibu Mhe. Jussa nilikuwa nina ombi moja, kidogo Waheshimiwa Wajumbe

wanapozungumza waikaribie hiyo maiki kwa sababu huku kidogo mkiwa mbali hatusikii vizuri. Kwa hiyo nimeyasikia lakini kama sikuyapata vizuri naomba radhi. Lakini huwa tunapata tabu kidogo tukiwa huku naomba kidogo tuikaribie maiki. Samahani sana Mhe. Spika.

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Jussa Ladhu swali lake la nyongeza kama ifuatavyo. Nakiri kwamba ni kweli kumekuwa na msongamano wa magari hasa katika eneo hili la bandarini wakati boti zinapoingia na kutoka. Lakini ukweli kwamba msongamano ule unakuja, unajua madereva ndio sisi, Mhe. Jussa dereva na mimi ni dereva na wengineo.

Kila mmoja hatutaki ku-*observe* ile sheria hilo ndio tatizo. Kwa sababu tumekataza kwamba gari zisije upande huu, lakini utakuta wengine wanazileta na wanakuwa wabishi. Sasa ndio wanakuwa wana *block* moja hiyo. Halafu ukenda pale Bandarini penyewe utakuta hakuna taratibu, kila mmoja anafanya atakavyo. Sasa hivi tunajitahidi tusimamie ili tuwaachie wenyewe vyombo vya sheria na sisi ni vizuri umetutanabaisha na hilo tumeliona, tutalifanyia kazi.

Mimi nahisi kweli hilo tatizo lipo, lakini kama sote tutatii, tutafuata zile taratibu zilizokuwepo nafikiri mambo yatanyooka sana.

Mhe. Asha Bakari Makame: Ahsante sana Mhe. Spika, kwanza nichukue nafasi hii ya kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha sote kufika hapa katika hali ya usalama na afya njema.

Mhe. Spika, Mhe. Waziri ametuelezea ni sababu zipi ambazo zinafanya njia ile ifungwe. Lakini Mhe. Spika, niungane mkono na mjumbe aliyemaliza kuuliza swali kwamba amezidisha msongamano mkubwa sana wa magari.

Sababu nyengine ambayo inazidisha na kuna mpango gani ya kwamba yale madubwana, maana hata siyajui jina lake, yameenezwa kuanzia pale Bandarini wakati wa msongamano wa meli, madude ya masaruji yamefika mpaka kwenye njia. Ni utaratibu gani ambao ameutumia Mhe. Waziri kwa msongamano huo wa magari.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) na **Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi:** Mhe. Spika, ninachotaka kusema yale ma- *block* ya saruji yanayowekwa ndio yale niliyoyasema madereva ndio sisi, wengine hatutaki kufuata taratibu. Sasa yale yamewekwa kuzuia watu wasiende huko kusikotakiwa.

Nitakuja mfano kwenye geti la Bandarini pale yalikuwepo na yaliwekwa kwa sababu *tax drivers* walikuwa wanapanda mpaka juu. Mimi mara nyingi huwa napita nakagua naona hiyo hali, lakini baada ya kuwekewa huo utaratibu nenda sasa hivi yameshaondoshwa yote, hayapo sasa hivi yameshaondoshwa.

Kwa sababu wameelekezwa na wamefahamu. Mimi ninachoomba Mhe. Spika, Mhe. Asha tusaidiane, anaposafiri akiona siku nyengine akiwa kachukua *tax* afuate taratibu zilizokuwepo na tuwaelimishe wengine.

Sote tukifuata taratibu nafikiri itatusaidia. Juzi katoka China Mhe. Asha kaona kule sio ma–*block* tu lakini wale wanaweka visu, ukigusa tu na mpira wako njia sipo unapasuka. Hayo yote ni jinsi ya kuwadhibiti madereva. Ahsante.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Spika, nasikitika kwa kusema kwamba Waziri kalidanganya Baraza kwa kusema kwamba ma- *lock* yale yameondolewa. Mpaka dakika hii tunavyozungumza ma-*block* yale yapo pale pale na namuomba akitoka Barazani akayaangalie. Naomba aurekebishe usemi wake huo.

Mhe. Spika: Mhe. Waziri nenda kahakikishe ili iwe kumesemwa kitu sahihi na labda Waziri wa Miundombinu anataka kusema kitu. Maana si kubwa kwamba yameondolewa yakarejeshwa tena.

Mhe. Waziri wa Miundo Mbinu: Mhe. Spika, na mimi nakushukuru kwa kuleta ufafanuzi kidogo katika suala hili. Mimi Afisi yangu iko pale, namuhakikishia Mhe. Jussa hayo ma- *block* hayapo.

Mhe. Spika: Tukahakikishe kama hayajaondoshwa basi yaondohwe kama mlivyokusudia.

Nam. 23

Uwekezaji Uliokwama wa Agakhan Foundation Mangapwani.

Mhe. Hamza Hssan Juma – Aliuliza:-

Eneo la Mangapwani limemilikishwa kwa Shirika la Agakhan Foundation kwa ajili ya uwekezaji mkubwa wa Hoteli ya kitalii na kujenga kiwanja cha mchezo wa Golf, mchezo ambao hupendwa sana Duniani, hasa na matajiri wakubwa.

(a) Mhe. Waziri, Je, mbona mradi huo kwa muda mrefu umekwama.

(b) Unaweza kutuambia kuna jitihada za kuukwamua mradi huo.

(c) Je, wananchi hasa wa Mangapwani unawaambia nini kuhusu uwekezaji huo ambapo walitegemea kupata ajira katika eneo lao.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo – Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako na kwa idhini yako kwa heshima kubwa naomba kujibu swali la Mhe. Hamza Hassan Juma, rafiki yangu huyu, swali lake lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, mradi uliotajwa na Mhe. Mwakilishi tokea mwaka 2008 umefutwa baada ya kusimamishwa mkataba wa kukodishwa ardhi kutokana na muwekezaji kushindwa kutekeleza kama ilivyotarajiwa. Kwa maana hiyo mradi huo kwa sasa haupo tena.

(b) Mhe. Spika, kutokana na kwamba mradi wenyewe umeshafutwa na kwa kuwa wawekezaji hawakuomba kurejeshwa kwa mradi huo, serikali haioni haja ya kufanya jitihada za kuurejesha tena kwa wawekezaji hao. Kwa sasa serikali inatafuta wawekezaji wengine wa uhakika ambao watapenda kuliendeleza eneo hilo kwa kuwekeza miradi mbali mbali ambayo itakuwa na manufaa kwa wananchi wa Mangapwani na Wananchi wa Zanzibar kwa ujumla.

(c) Mhe. Spika, serikali kwa sasa imeshapokea maombi ya wawekezaji wengine kwa ajili ya kuliendeleza eneo hilo, ili kuona kuwa watakaopewa eneo hilo wataweza kutimiza matarajio ya wananchi wa Mangapwani na wananchi wa Zanzibar kwa ujumla na hasa katika suala zima la upatikanaji wa ajira. Maombi ya wawekezaji hao kwa sasa yanazingatiwa kwa kina. Napenda kuwaambia wananchi wa Mangapwani na wa Zanzibar kwa ujumla kuwa serikali ipo makini katika kupata wawekezaji wenye manufaa na Zanzibar na watu wake.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Spika, nakushukuru tena kwa kunipa nafasi hii kumuuliza Mhe. Waziri swali la nyongeza kama hivi ifuatavyo:

Mhe. Spika, Shirika la *Agakhan Foundation* kabla ya kupewa eneo hili walikuwa na *memorandum of understanding* (MOU) ya serikali, na katika (MOU) ile kulikuwa kuna makubaliano mbali mbali. Walipopewa eneo hili kulikuwa kuna masharti mbali mbali waliyowekeana baina ya *Agakhan Foundation* na serikali, ikiwemo kuondoa kambi iliyokuwepo katika eneo lile. Lakini vile vile serikali kupeleka umeme pamoja na kupeleka barabara na kuwaondoa wale wanachi. Suala hili la kuwaondoa wananchi lilikuwa ni la Agakhan.

Katika makubaliano hayo takriban yale ambayo yalikuwa yafanywe na serikali, serikali haikufanya ikawa anafanya mwenyewe *Agakhan Foundation*. Yeye kama serikali wao ndio waliokuwa hawakutekeleza yale makubaliano na *Agakhan Foundation,* matokeo yake serikali ndio wakamfutia ile hati Agakhan Foundation.

(a) Je, Mhe. Spika, tunaona hapa kwamba haki imetendeka. Kama haki haijatendeka *Agakhan Foundation* amefutiwa hati ile lakini bado mpaka leo ana uwekezaji wake pale unaendelea.

(b) Je, Serikali inatoa tamko gani katika suala hili.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Uchumi na Mipango ya Maendeleo: Mhe. Spika, katika miaka ya 1990 tulikuwa tuna njaa kubwa sana ya wawekezaji hapa Zanzibar. Agakhan alijitokeza na nataka nimkumbushe Mhe. Mwakilishi, Serikali ya Mapinduzi Zanzibar ilimpa Agakhan eneo kubwa sana zaidi ya hekta 70 kwa sababu tulikuwa tuna hamu ya uwekezaji. Alichokifanya tokea miaka ya 90 mwanzoni ameweka *restaurant* tu hajasafisha hata eneo. Tumemuachia muwekezaji huyu muda wote huo. Juhudi za serikali zimeanza kujenga barabara kuelekea Bumbwini, na sasa inakamilika.

Tulichokiona sisi kama ni serikali, kwa kuwa sasa muda umekuwa mrefu kwa yeye hakuna alichokifanya zaidi ya kuweka *restaurant*, serikali imeamua kulipunguza eneo hilo na kumbakishia hekari 20 kwa ajili ya restaurant yake.

Sasa hivi nadhani Mhe. Mwakilishi atakubaliana na mimi, wawekezaji wapo wengi, tuna tatizo la ardhi. Serikali imechukua ardhi yake kwa manufaa ya watu wake. Na kama suala lake linavyoekeza muda mrefu wananchi wa Mangapwani wametarajia kutokana na mradi ule. Serikali sasa inaelekeza ardhi hii kwa wawekezaji wengi ili yale ambayo wanchi wa Mangapwani na Wazanzibari walikuwa wanayatarijia kutoka Shirika la Agakhan wayapate kutoka kwa wawekezaji wengine.

Mimi nadhani serikali imetumia busara sana zaidi ya miaka 25 kama kweli ni muwekezaji angekuwa amefanya majukumu yake, halafu akaiona serikali nayo kutekeleza majukumu yake.

Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi kuuliza swali moja la nyongeza.

Kama nilivyomsikia Mhe. Waziri katika jibu lake mama akisema kwamba serikali imeshapata wawekezaji wengine. Je, Mhe. Waziri wawekezaji hao ni kutoka shirika gani au kutoka wapi. Ahsante.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo: Mhe. Spika, kwa sababu sina ile orodha ya nchi wanazotoka naomba nitampatia Mhe. Mwakilishi baadaye. Lakini wawekezaji wapo kutoka nchi mbali mbali, wengine wanataka kuwekeza katika sekta za Hoteli na miongoni mwao wakiwemo wawekezaji kutoka Uturuki.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii na naomba nimuulize Mhe. Waziri kaka yangu swali la nyongeza la kifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:

Alipokuwa anajibu suala la Mhe. Hamza, Mhe. Waziri alisema kuwa miaka ya 1990 serikali ilikuwa na njaa kubwa ya kuwahitajia wawekezaji.

(a) Namuomba kumuuliza tu kwa sasa njaa hiyo imeondoka na kama njaa imeondoka maana yake kuna shibe. Naomba anieleze kuna shibe gani iliyokuwepo Zanzibar ya uwekezaji.

(b) Amekiri kwamba tatizo kubwa ambalo Zanzibar tunalo ni tatizo la uchache wa ardhi, kwamba wawekezaji wapo lakini ardhi ndogo. Je, serikali sasa itakuwa tayari kupitia Wizara yake chini ya mitaji ya umma kutafuta maeneo yote ambayo yamechukuliwa na watu kwa maslahi binafsi, ili wanyang'anywe wapewe wawekezaji kwa ajili ya maslahi ya Zanzibar.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako na kwa idhini yako naomba kumjibu mdogo wangu Mhe. Hija maswali yake ya nyongeza kama ifuatavyo.

Kwanza nilichokuwa nataka kutafsiri hapa wakati ule Shirika la Agakhan tulilipa eneo kubwa sana kwa sababu ya ile miradi ambayo alitamka mwenyewe. Kwa hivyo tukampa. Kwa sasa tatizo letu sio wawekezaji, tatizo letu ni ardhi, wawekezaji kwa sasa wanakuja wengi sana. Nadhani Mhe. Waziri wa Ardhi atakubaliana na mimi *ZIPA* inavyompelekea barua kila baada ya muda ya kuomba eneo kwa ajili ya uwekezaji.

Mhe. Spika, nataka nimuhakikishie Mhe. Mwakilishi kwamba nitafanya kazi kwa karibu zaidi na Waziri wa Ardhi kuona kwamba maeneo ambayo wanayo watu lakini yamekaa bure na tunao wawekezaji wanataka kuekeza katika maeneo hayo. Kwa sababu ardhi ni ya serikali si ya mtu, basi maeneo hayo tutashirikiana na Mhe. Waziri wa Ardhi tuone jinsi gani tutakavyoweza kuyachukua kwa taratibu na sheria za nchi ili tuwapatie wawekezaji wanaotaka kuekeza kwa manufaa ya watu wetu na nchi yetu.

Nam. 22

Bei ya Karafuu na Mzunguko wa Fedha

Mhe. Jaku Hashim Ayoub – Aliuliza:-

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ilipandisha bei ya karafuu kwa lengo la kuinua kipato cha mkulima na kuongeza mzunguko wa fedha.

a) Je, lengo hilo limetimia kwa asilimia ngapi.

b) Kuna taarifa kwamba mzunguko wa fedha Kisiwani Pemba ni mdogo licha ya serikali kutumia zaidi ya bilioni 28 kununua zao hilo. Je, serikali imefanya utafiti gani kujua sababu ya mzunguko wa fedha kuwa mdogo.

Mhe. Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko – Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 22 lenye kifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

a) Mhe. Spika, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imepandisha bei ya karafuu ambapo mkulima sasa analipwa asilimia 80 ya bei ya kuuzia nje ya nchi, na kutangaza bei ya pesa za Kitanzania 15,000/= kwa kilo sawa na fedha za Kitanzania 22,500/= kwa pishi moja ya karafuu. Mhe. Spika, malengo makuu ya kupandisha bei ya karafuu ni kuleta tija kubwa katika kufanya biashara ya karafuu ambayo itajumuisha kuinua kipato cha mkulima, kuongeza uzalishaji, kupanua mashamba ya karafuu pamoja na kupambana na magendo ya karafuu yaliyokuwa yamekithiri katika miaka ya nyuma, na vile vile kurejesha imani ya wakulima kwa serikali yao.

   Mhe. Spika, malengo hayo yamefikiwa kwa asilimia kubwa sana kwani lengo la Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar lilikuwa ni kununua karafuu tani 3,000, lakini tumefanikiwa kununua hadi sasa tani 4,726 ambapo badala ya kutumia jumla ya fedha za Kitanzania

bilioni 33 na hadi sasa serikali imetumia bilioni 72. Kwa hivyo, Mhe. Spika, lengo limezidi kwa asilimia 30 takriban kwenye manunuzi na asilimia 60 kwenye matumizi.

Mhe. Spika, kwa niaba ya serikali kupitia Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko naomba kuchukua fursa hii basi, kuwapongeza sana wakulima wetu kwa kurejesha imani yao kwa serikali kwa kuwauzia karafuu zao zote katika Shirika la *ZSTC*. Pia nawashukuru kwa kuonesha mashirikiano ya hali ya juu kwa kufanikisha adhma hii nzuri ya Serikali yao ya Mapinduzi ya Zanzibar. Mhe. Spika, tunawapongeza sana kwa hilo.

b) Mhe. Spika, kwa upande wa mzunguko wa fedha hali hii inategemea pamoja na mambo mengine shughuli za kiuchumi na kibiashara zinazofanywa katika maeneo husika. Katika msimu wa mwaka huu serikali imelipa bilioni 72 kama nilivyosema mwanzo kwa manunuzi ya karafuu, ambapo Pemba peke yake zimelipwa kwa wakulima zaidi ya fedha za Kitanzania bilioni 65. Baadhi ya fedha hizo zilizolipwa kwa wakulima ziko majumbani, nyengine zipo kwenye mabenki na nyengine zipo nje ya nchi kwani baadhi ya wamiliki wa mashamba hayo wako nje ya Zanzibar. Serikali kupitia Wizara ya Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo ambapo ipo chini ya Mhe. Rais imepeleka wataalamu wake Pemba kufanya utafiti kujua ni kiasi gani cha fedha kimebakia Pemba au Zanzibar kwa ujumla.

Mhe. Spika, kwa hivyo katika vuno la karafuu la msimu huu kuna viashiria vingi (*indicators*) vinavyoonesha kuongezeka kwa shughuli mbali mbali za kiuchumi kutokana na ujazo wa fedha uliojitokeza. Viashiria hivyo ni kama vifuatavyo:-

- Ongezeko la ujenzi wa nyumba za kudumu na za kisasa kwa wakulima na wananchi kwa ujumla.
- Kuongezeka kwa ununuzi wa vipando kwa wananchi na hasa vipando vya moto kama magari na pikipiki.
- Ongezeko la uanzishwaji wa miradi midogo midogo ya biashara kwa wananchi.
- Ongezeko la bidhaa za biashara zilizoingizwa Kisiwani Pemba na hasa bidhaa za vyakula.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Spika, nashukuru sana kwa majibu ya Mhe. Naibu Waziri hivyo naomba kuuliza swali moja la nyongeza lenye (a) na (b).

a) Mhe. Spika, mimi nataka kufahamu mabadiliko hayo ya bei yamemsaidia vipi mwananchi wa kawaida kwani kwa mujibu wa taarifa za taasisi za fedha bado mzunguko wa fedha Kisiwani Pemba ni mdogo licha ya serikali kupandisha kwa asilimia 300.

b) Kuna taarifa kwa wakulima wa zao hilo kwamba wengi walionufaika ni wale waliovuna kwenye mikarafuu. Je, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar itachukua hatua gani kuwasaidia wananchi wa Pemba.

Mhe. Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Spika, mimi nilitegemea Mhe. Mwakilishi ataipongeza serikali kwa jitihada hiyo iliyochukua, lakini katika jibu langu nimesema kwamba serikali kupitia Wizara ya Nchi Ofisi Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo imepeleka wataalamu wake kufanya utafiti ili kujua ni kiasi gani cha fedha zimebakia nchini.

Lakini kwa ujumla kwa kuwa wengi wa wamiliki wa mashamba makubwa ya karafuu hawapo nchini, basi nimesema kwamba zipo fedha ambazo zipo nje ya nchi.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, Mhe. Naibu Waziri alipokuwa anatoa jibu lake amesema kwamba moja katika matumizi ya fedha za karafuu zinazochumwa na wananchi Pemba ni kujijengea nyumba za kudumu, na hilo ni kweli.

Mhe. Spika, lakini nyumba hizi zinatumia matofali ya kuchonga, kwa hivyo siku zote kuna mmong'onyoko mkubwa wa ardhi na uharibifu wa mazingira kwa sababu ya wananchi kujijengea majumba ya kudumu kwa kutumia matofali haya. Kwa vile bei ya karafuu itaendelea kuwa hivi hivi na wananchi Kisiwani Pemba wataendelea kujenga hivyo Mhe. Naibu Waziri haoni kwamba ipo haja hivi sasa wizara yake kujenga kiwanda cha kudumu cha saruji ili tatizo hili la uharibifu wa mazingira liweze kuondoka.

Mhe. Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Spika, ni kweli kwamba tatizo liliopo Pemba ni kuwa wananchi katika masuala ya ujenzi wanatumia sana matofali ya kuchonga, na ni kweli kabisa kwamba matofali haya yanaharibu mazingira.

Mhe. Spika, mimi nataka nimtoe wasi wasi Mhe. Mwakilishi kwamba suala hilo serikali imeliona na limo katika kufanyiwa kazi, na kwa taarifa ya Baraza lako tukufu tupo tayari katika kuhakikisha tunatafuta kiwanda kuwekeza ndani ya nchi ya Zanzibar ambacho kitazalisha saruji, lakini bado mchakato huo unafanyiwa kazi na hapo utakapokamilika basi Waheshimiwa wa Baraza hili watapata taarifa.

Nam. 94

Walemavu na Mchakato wa Maoni ya Katiba Mpya

Mhe. Raya Suleiman Hamad*:*

(Mheshimiwa aliyeuliza swali hili ameliondoa).

Nam. 4

Chuo cha Ufundi Kengeja

Mhe. Jaku Hashim Ayoub – Aliuliza:-

a) Serikali imechukua hatua gani katika mwaka uliopita wa fedha wa kujenga Bweni la wanafunzi na ukarabati wa makaro ya Chuo cha Ufundi Kengeja Pemba, ambayo afya ya wanafunzi wanaoishi katika chuo hicho.
b) Wizara yako ina mpango gani wa kupunguza tatizo la upungufu wa walimu kwenye chuo hicho.
c) Chuo cha Ufundi Kengeja kimepatiwa kiasi gani cha fedha kwa mwaka wa bajeti unaoendelea na kiasi hicho ni asilimia ngapi ya makadirio ya mwaka.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali – Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali Nam. 4 lenye vifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

a) Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha 2010/2011 wizara ilitumia jumla ya milioni 40 kwa ajili ya kukamilisha kazi za ukarabati wa dakhalia pamoja na mfumo wa maji machafu katika Skuli ya Sekondari ya Ufundi Kengeja. Pia kazi za uchongaji wa milango, madirisha manane zimekamilika, kazi za ujenzi wa bweni la wanafunzi hazikupangiwa katika mwaka uliopita. Kazi hiyo inakusudiwa kufanyika katika mwaka huu wa fedha kwa kuandaa michoro ya ujenzi wa bweni. Kazi zilizofanyika zimesaidia sana katika kuimarisha mazingira ya Skuli hiyo.

b) Mhe. Spika, tatizo la upungufu wa walimu wa sayansi na ufundi inazikumba Skuli zetu nyingi ikiwemo, Skuli ya Sekondari ya Ufundi Kengeja. Wizara inakusudia kuajiri walimu wapya katika mwaka huu wa fedha, na baadhi ya walimu hao watapangiwa kazi katika Skuli ya Ufundi ya Kengeja. Mhe. Spika, ni kwamba tayari tumepata kuajiri walimu 240 na mpango wa kuwagawa walimu hao ndio ambao tunaendelea nao sasa hivi.

c) Mhe. Spika, mradi wa uimarishaji wa elimu ya ufundi umetengewa jumla ya shilingi milioni 400 kwa mwaka 2011/2012. Mradi huu unatekelezwa katika Skuli ya Ufundi ya Kengeja na Taasisi ya Sayansi ya Karume. Mhe. Spika, hadi hivi sasa shilingi milioni 100 zimepatikana kati ya hizo, shilingi milioni 30 ni kwa ajili ya Skuli ya Ufundi Kengeja na shilingi milioni 70 kwa Taasisi ya Sayansi ya Karume. Nakushukuru sana Mhe. Spika.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kuuliza swali moja la nyongeza lenye kifungu (a) na (b).

a) Mhe. Spika, kwa kuwa tatizo hilo limekuwa ni la muda mrefu sana na linaathiri wanafunzi kitaaluma. Hivyo, serikali ina mpango gani wa dharura na wa haraka kutatua tatizo hilo.

b) Kwa kuwa chuo hicho kimekabiliwa na uhaba wa walimu muhimu sana wa ufundi. Je, huoni kuna haja ya kwenda kuazima walimu Tanzania Bara walioko katika Chuo cha *VETA*.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Spika, kama ambavyo nilizungumza katika suala mama kuwa kuna matengenezo ambayo tumeyafanya pale na tumetumia karibu milioni 40, na juzi tu Mhe. Spika, nilikuwa na ziara katika Skuli mbali mbali moja ikiwa ni Skuli hii ya Kengeja nimeona matatizo ambayo yapo pale na hatua tayari tumezichukua matatizo yale yanafanyiwa kazi na muda si mrefu tatizo lile la maji kuvuja litakuwa limemalizika.

Mhe. Spika, vile vile nimesema kwamba tunao walimu 240 ambao tumeshawaajiri katika kipindi hiki, na katika walimu hao 240 basi tutapeleka baadhi ya walimu katika Skuli ya Kengeja. Nakushukuru sana Mhe. Spika.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, kwa kuwa tatizo la bweni la wanafunzi katika Skuli ya Ufundi ya Kengeja lipo kwa muda mrefu na kwa kuwa katika jibu la msingi Mhe. Naibu Waziri amesema kwamba ndio kwanza michoro inatayarishwa juu ya kutayarisha bweni hilo.

a) Je, Mhe. Naibu Waziri atakubaliana na mimi kwamba kwa kiasi kikubwa Wizara imekwenda kinyume na majukumu yake.
b) Mhe. Spika, ili wanafunzi waweze kufanya vizuri katika Skuli ile ni pamoja na kuweka mazingira mazuri ya pale, na kwa kuwa anasema ametumia zaidi ya milioni 40 katika kipindi hiki na mpaka leo hii makaro yanaendelea kuvuja katika kile Chuo. Je, haoni anahatarisha afya ya wanafunzi jambo ambalo linaweza likawafanya wanafunzi wetu wasifanye vizuri katika masomo yao.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Spika, kwanza nataka akumbuke Mhe. Mwakilishi kama Chuo kile tulikianza tukiwa na wanafunzi 75 tu. Kwa hivyo, mazingira ya wakati ule yalikuwa yakiruhusu kwa mujibu wa wanafunzi ambao walikuwepo katika kipindi kile, lakini hivi sasa tuna wanafunzi karibu 164 ambao wapo pale. Kwa hivyo, ni dhahiri inaonesha kuwa nafasi ambayo waliokuwa wakitumia wanafunzi zamani na hivi sasa itahitajika nafasi nyengine. Mhe. Spika, ndio maana Wizara ikaona kama kuna haja ya kujenga bweni jengine kwa ajili ya wanafunzi, ndilo hilo ambalo tumesema tuko katika *process* Mhe. Spika.

Mhe. Spika, kuhusu mazingira mimi nataka nikubaliane nae Mhe. Mwakilishi, lakini tatizo ambalo lipo pale ni kwamba mjenzi ambaye alijenga lile bweni pamoja na nyumba za walimu ilikuwa ni karo moja. Kwa hivyo, Wanafunzi na Walimu wakitumia ile karo huwa inazidiwa inabidi ndio maji yanafura. Mhe. Spika, hilo tatizo mimi nimeliona na ndio nikamwambia Mhe. Mwakilishi kama tuko katika matengenezo baada ya kwenda mimi mwenyewe kuona kwamba kweli kuna tatizo na tayari tumeshapeleka mafundi na muda si mrefu tatizo hilo litamalizika.

Nam. 3

Daraja la Kicha – Pemba

Mhe. Rufai Said Rufai - Aliuliza:-

Wananchi wa Jimbo la Konde na Tumbe wanaishukuru sana Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano kwa kuwawekea daraja la muda kutokana na kuharibika vibaya kwa daraja la Kicha.

Je, Wizara yako ina mpango gani wa kulijenga daraja la kudumu katika eneo hilo baada ya zaidi ya nusu ya mwaka wa Bajeti kupita.

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 3 kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, kabla sijajibu swali hilo nakuomba uniruhusu niseme machache. Mhe. Spika, kwanza kabisa mimi mwenyewe na wananchi wangu wa Jimbo la Ole kwa kupitia Baraza lako hili tukufu tunatoa rambi rambi na pole kubwa kwa wananchi wa Jimbo la Bububu kwa kuondokewa na kiongozi mwenzetu mwakilishi wao, Mhe. Salim Amour Mtondoo inshaallah Mwenyezi Mungu ailaze roho yake mahali pema, peponi. Amin.
Mhe. Spika, nataka pia nimpongeze Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali kwa kuchaguliwa kuwa Mwakilshi wa Jimbo la Uzini naahidi kwamba tutashirikiana katika kutekeleza majukumu yaliyotukabili kwa manufaa ya wananchi. Mhe. Mohammedraza na mimi naungana na Mhe. Spika kukukaribisha katika Baraza hili.

Mhe. Spika, sasa naomba kujibu swali kama hivi ifuatavyo:-

Mhe. Spika, kwanza nimpongeze sana mwakilishi wa Jimbo la Tumbe, lakini pia wananchi wa Jimbo la Konde na Tumbe kwa kuona juhudi za serikali na wakashukuru na wakapongeza. Mhe. Spika, mpango wa kulijenga Daraja la Kicha umekamilika, kazi hiyo inatarajiwa kuanza wakati wowote kuanzia sasa kwa vile hatua zote za kumpata mkandarasi zimekamilika na sasa kinachosubiriwa ni kuingizwa fedha kutoka Mfuko wa Barabara na kumuarifu mjenzi aliyechaguliwa kukasibiana na Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano kufanya kazi hiyo.

Mhe. Rufai Said Rufai: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, ni kwamba Daraja la Kicha hivi tuko katika mwezi wa March na huu ni mwezi wa kipindi cha mvua za Masika na lile daraja limeshakatika.

a) Je, Mhe. Waziri haoni kwamba kuna haja ya kuliondoa na kuyapa nafasi yale maji yaweze kupita vizuri.
b) Kwa kuwa lile eneo walilojenga *culvert* lile fusi lilotiwa limeshaanza mashimo na kuanza kuleta athari kwa magari na wapita njia. Je, haoni kwamba ipo haja angalau mita zile 25 wakaweza kutia lami pale.

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Spika, daraja ambalo limeharibika lilijengwa katika miaka ya 30, na ni bahati mbaya sana kwamba wakati wa ujenzi wa barabara ile iliyojengwa katika miaka ya 90 na *COGEFER*, daraja lile halikujengwa upya kwa hivyo uzuri wake ilisababisha magari makubwa yapite katika eneo lile. Mhe. Spika, uharibifu uliotokea ni kwamba daraja lile liliditia, lakini bado linaruhusu magari ambayo hayazidi tani 5.

Mhe. Spika, ni kwamba juhudi ya kwanza tuliyoifanya ni kuya-*limit* magari yote yanayozidi tani 5 yasipite juu ya daraja, tukaweka alama, tukaweka na matangazo na pia tukaweka na askari. Lakini kama hilo halitoshi Mhe. Spika, kwa juhudi za serikali tukajenga haraka iwezekanavyo kwa dharura kabisa nafasi ambayo inaruhusu kuchukua magari hata ya tani 30 na 40, na hiyo sasa hivi ndio inayotumika.
Mhe. Spika, kama nilivyosema kwamba hii haikuwemo kwenye mpango ni jambo la dharura limetokea na kwa hivyo mfuko wa barabara ulikubali kutoa fedha kwa ajili ya ujenzi. Kwa

hivyo, ujenzi utaendelea kama nilivyoeleza, lakini vile vile hiyo nafasi ambayo sasa hivi ina mashimo wakati daraja hilo litakuwa linajengwa magari yote yatakuwa yanapita pale, hatutaweka lami lakini tutakuwa tunaitengeneza ipitike bila ya matatizo.

Mhe. Abdalla Juma Abdalla: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa uharibikaji wa Daraja la Kicha ulikwenda sambamba na uharibikaji wa Daraja la Koongo pale Pujini na kama ambavyo waliweka kule *culvert* na kule pia walikwenda kuweka *culvert.* Mhe. Spika, kwa kuwa serikali iliwahi kutoa tamko mara moja kwamba madaraja yale mawili yatajengwa sambamba. Je, huu utaratibu wa kutafuta wakandarasi kwa ajili ya Daraja la Kicha ni pamoja na lile la Koongo au nikawajibu nini watu wa Pujini.

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Spika, nilitaka kujibu swali hili pamoja na Daraja la Pujini lakini kwa sababu suala lilikuwa la Kicha nikajibu kwa Daraja la Kicha. Mhe. Spika, zabuni ambayo ilitolewa na wizara yangu ilikuwa ni kwa ajili ya madaraja mawili, Daraja la Kicha na Daraja la Pujini. Kwa hivyo, fedha inayosubiriwa kwa ajili ya kujenga Daraja la Kicha ni fedha hiyo hiyo ambayo itatumika kwa ajili ya daraja la Pujini. Kwa hivyo, namuhakikishia Mhe. Mwakilishi kwamba wakati wowote fedha zitakapoingia na si muda mrefu na kwa sababu mkandarasi tayari tumeshampata lakini hatujamwambia hivyo siwezi kusema ni nani na wala siwezi kusema ni kwa kiasi gani. Lakini namuhakikishia kwamba hii ilikuwa ni zabuni moja na madaraja haya yanajengwa na mkandarasi mmoja na wakati mmoja.

Nam. 6

Kikombe cha Babu

Mhe. Jaku Hashim Ayoub – Aliuliza:-

Tanzania imejipatia sifa kubwa ndani na nje ya nchi kutokana na huduma ya Kikombe cha Mchungaji Ambilikille Mwaisapile (Babu wa Loliondo) kinachosemekana kutibu magonjwa sugu ikiwemo ukimwi, kisukari n.k.

(a) Je, kuna ukweli wowote juu ya kikombe hicho kutibu magonjwa sugu ukiwemo ukimwi.

(b) Je, ni watu wangapi waliopata kikombe cha Babu wamekufa hadi sasa toka Babu huyo wa Loliondo aanze kutoa huduma hiyo.

Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Jaku Hashim Ayoub wa Jimbo la wananchi wa Muyuni swali lake Nam. 6 lenye vifungu a na b kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii Tanzania Bara ilikiagiza kitengo cha Utafiti *National Institute for Medical Research (NIMRI)* kutafuta ukweli wa uwezo wa Kikombe cha Babu kutibu maradhi aliyoyataja ukiwemo ukimwi. Kwa mujibu wa ripoti ya taasisi hiyo Kikombe cha Babu hutibu maradhi mbali mbali kama vile kifafa, shindikizo la damu, sukari, kutoa kinga ya ini juu ya saratani na vile vile kutibu maradhi yanayosababishwa na kirusi aina ya *Herpes Simplex Virus (HSV)* ambacho husababisha maradhi nyemelezi kwa wagonjwa wa UKIMWI. Ndio maana ripoti hiyo ikaripotiwa kuwa Kikombe cha Babu kina uhusiano na tiba ya UKIMWI.

Kwa hili kuna ushahidi wa wagonjwa wanaoishi na Virusi vya Ukimwi (*VVU*) wanaohudumiwa katika baadhi ya kliniki zetu na hasa Hospitali ya Mnazi Mmoja ambao wamekiri kwenda Arusha kupata Kikombe cha Babu. Bahati mbaya baada ya kutumia kikombe hicho na kupimwa tena damu zao wagonjwa hao wameonekanwa bado wanaishi na Virusi vya Ukimwi na hali zao kudhoofika kwa kuacha dawa za *ARVs* kwa kipindi kile ambacho walipewa ushauri na Babu.

(b) Kwa bahati mbaya Kitengo cha Ukimwi cha Wizara ya Afya Zanzibar hakina taarifa hiyo.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Spika, namshukuru Mhe. Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri, wananchi wengi wanataka kusikia kauli ya serikali kwamba kile kikombe kinatibu au hakitibu?

Pili, iwapo dawa hiyo imebainika haitibu maradhi hayo. Je, serikali itachukua hatua gani kwa Babu ambapo itakuwa ni fundisho kwa babu huyo.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Spika, naomba nirudie tena kwamba uthibitisho uliotolewa na *NIMRI* unasema kwamba, kuna baadhi ya maradhi ambayo yanaweza yakatibiwa kama kifafa, shindikizo la damu, kisukari na kutoa kinga ya ini. Pia kuna kirusi aina ya *Herpes* ambacho husababisha maradhi nyemelezi ya wagonjwa wa UKIMWI.

Vile vile nimesema kwamba, baada ya kurudi huko walipotolewa damu Virusi vya Ukimwi vimekutikana bado vipo. Kwa hivyo, kutokana na hilo nathubutu kusema kwamba Kikombe cha Babu hakitibu UKIMWI.

Mhe. Spika: Nashukuru muda wa maswali umekwisha, Mhe. Naibu Waziri nakushukuru, Waheshimiwa Wajumbe nawaomba radhi tulitumia muda kidogo kutoa taarifa ya Spika na shughuli nyengine kwa hivyo maswali mengi yamebaki kwa leo. Lakini naamini yatajitokeaza katika *order paper* zitazoendelea huko mbele. Tunaendelea.

HOJA ZA SERIKALI

Mswada wa Sheria ya Maslahi ya Viongozi wa
Kisiasa ya Mwaka 2011
(Kusomwa kwa Mara ya Kwanza)

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe tutakumbuka kwamba mswada huu ulikwishajadiliwa huko nyuma na tukamaliza na majadiliano, lakini kwa busara za Baraza hili tukaona kwamba ipo haja Mswada ukarudishwa kwenye kamati.

Mwenyekiti wa Kamati ameshatoa taarifa juu ya mswada huu kwamba walikaa na kukubaliana mambo ya msingi, nafikiri nakla zitakuwa zimegawiwa kwa wajumbe juu ya yale mambo ya msingi ambayo Mhe. Mwenyekiti walikaa na waziri.

Halikadhalika Mhe. Waziri pia naye ametoa taarifa kwamba kweli kamati walikaa na wakafikia pahala pazuri. Kwa hivyo, kazi ya majadiliano ilimalizika tangu Mkutano uliopita napenda sasa nichukue nafasi hii kumkaribisha Mhe. Waziri wa Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi ili atoe majumuisho ya Mswada huu. Mhe. Waziri karibu.
Waheshimiwa kabla ya Waziri kutoa majumuisho tulipoanza kuingia ukumbini na kama kawaida yetu kuomba wimbo wa taifa upigwe ambao kwa kawaida huwa unaongoza Waheshimiwa Wajumbe kwa pamoja kuimba wimbo ule wa taifa kwa bahati mbaya mitambo yetu ilikataa kufanya kazi hiyo, mafundi walituaribu kwamba walijaribu mapema na wakaona mitambo inafanya kazi, lakini kwa bahati mbaya sana wakati ulipofika kwamba sasa upigwe wimbo ule mitambo ikakataa, ndio masuala ya mitambo yalivyo. Waheshimiwa Wajumbe nashukuru kwamba kumbe wimbo wetu wa taifa uko katika vifua vyetu, kazi hiyo mliifanya bila ya kuongozwa na vyombo vya mitambo pale. Nakushukuruni mmeifanya kazi hiyo vizuri na shughuli zetu zilikwenda kama kawaida.

Lakini hapo hapo nichukue nafasi hii kuwaomba radhi sana kwamba mitambo yetu ilitukatalia kutuongoza katika wimbo wa taifa kama ulivyo utaratibu wetu. Tunajitahidi ili kuona kwamba mitambo itakuwa inafanya kazi kama kawaida wakati shughuli zetu zinaendelea. Niombe radhi sana Waheshimiwa Wajumbe na sasa nimuombe Mhe. Waziri aendelee.
Mhe. Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako kwa mara nyengine tena nakushukuru sana kwa kunipatia nafasi hii ya kufanya majumuisho ambayo tuliyaakhirisha tarehe 18 Januari, 2012 juu ya Mswada wa Sheria ya Kufuta Sheria Nam. 4 ya Mwaka 1988 na Sheria Nam. 6 ya Mwaka 1999 na Kuanzisha Sheria Mpya ya Maslahi ya Mafao ya Viongozi wa Kisiasa baada ya Kustaafu pamoja na mambo mengine yanayohusiana na hayo.

Mhe. Spika, kama nilivyosema tunakushukuru sana wewe mwenyewe, Waheshimiwa Wenyeviti ambao walikuwa wakikusaidia, lakini pia naomba niwashukuru Wajumbe wote wa Baraza lako tukufu kwa mashirikiano makubwa waliyotupa katika kuujadili mswada huu. Kwanza tulianza kwenye semina halafu tukaja hapa ukumbini, lakini pia naomba nitoe shukurani zangu za dhati kabisa kwa Mhe. Mwenyekiti wa Wenyeviti, Mhe. Hamza Hassan Juma pamoja na kamati yake yote inayosimamia Viongozi Wakuu.

Tulikaa vikao zaidi ya vitano kuujadili, kutokubaliana na mwisho kukubaliana. Kwa hivyo, mimi namshukuru sana na pia wenyeviti wa kamati mbali mbali za kudumu za Baraza la Wawakilishi walishiriki hasa katika kikao cha mwisho ambacho tuliweza kupitisha mambo mengi kwa kauli moja.

Mhe. Spika, sitosahau pia kuwashukuru Waheshimiwa Mawaziri na Manaibu Mawaziri wote nao walinisaidia sana katika ufafanuzi kwa baadhi ya vifungu wakati wa majadiliano. Nawashukuru kwa kazi kubwa sana waliyoifanya.

Mhe. Spika, sasa naomba niwataje Waheshimiwa Wote waliopata fursa ya kuchangia mswada huu. Kulikuwa na jumla ya Waheshimiwa 37 naomba sasa muwatambue mmoja baada ya mwengine.

1. Mhe. Hamza Hassan Juma

2. Mhe. Makame Mshimba Mbarouk
3. Mhe. Rashid Seif Suleiman
4. Mhe. Ismail Jussa Ladhu
5. Mhe. Omar Ali Shehe
6. Mhe. Asha Bakari Makame
7. Mhe. Hija Hassan Hija
8. Mhe. Ussi Jecha Simai
9. Mhe. Salmin Awadh Salmin
10. Mhe. Mohammed Haji Khalid
11. Mhe. Abdalla Juma Abdalla
12. Mhe. Subeti Khamis Faki
13. Mhe. Hassan Hamad Omar
14. Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria
15. Mhe. Mbarouk Wadi Mussa (Mtando)
16. Mhe. Saleh Nassor Juma
17. Mhe. Salim Abdalla Hamad
18. Mhe. Abdalla Mohammed Ali
19. Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak
20. Mhe. Fatma Mbarouk Said
21. Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi
22. Mhe. Rufai Said Rufai
23. Mhe. Abdi Mosi Kombo
24. Mhe. Ashura Sharif Ali
25. Mhe. Farida Amour Moh'd
26. Mhe. Bikame Yussuf Hamad
27. Mhe. Asha Abdu Haji
28. Mhe. Machano Othman Said (Waziri asiye na wizara maalum)
29. Mhe. Haji Faki Shaali (Waziri asiye na wizara maalum)
30. Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika
31. Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano
32. Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali
33. Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko
34. Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi
35. Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora
36. Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais
37. Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo.

Mhe. Spika, tunashukuru wote na ni imani yangu kuwa sikumsahau hata mmoja katika waliochangia.

Mhe. Spika, kama nilivyosema kwamba tunawashukuru sana Waheshimiwa Wajumbe wote kwa hoja nzito zilizotolewa na watu wote waliochangia. Lakini kabla sijazigusa hizi hoja zenyewe na kutoa ufafanuzi mdogo, naomba kidogo kufanya marekebisho ambayo yatatusaidia kutuongoza katika majumuisho yangu. Naomba sana tutumie lile Gazeti Rasmi la Serikali lililotoka mara ya pili, tulitoa la kwanza baadae tukalibadilisha tukatoa la pili. Sasa hili la pili ndio marekebisho mengi tumeyafanya mle tusitumie lile la kwanza. Baada ya kamati kukaa tukafanya marekebisho

kwenye lile la pili ambalo tumeshaligawa. Kwa hivyo, naomba sana tutumie lile la pili ambapo marekebisho yote tuliyafanya na tumeyagawa.

Pia kuna marekebisho mengine ya kifungu cha 26 baadae nitakisoma lakini naamini kishasambazwa au kinasambazwa hivi sasa, naomba radhi sio kikubwa sana ni kidogo tu.
Lakini pia naomba nifanye marekebisho Mhe. Spika, katika Mswada wenyewe kuna mambo ambayo tumeyafuta nahisi bora niyaeleze mwanzo kabisa yatarahisisha yale majumuisho yangu.

Katika vifungu ambavyo tumevifuta moja kwa moja kwanza ukurasa wa 295 juu kabisa kuna ufafanuzi ambao kwanza umeanza katika ukurasa wa 294 'Kiongozi wa Kisiasa' unaendelea ukurasa wa 295 ambao umeanza Waziri, Spika wa Baraza la Wawakilishi, Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi na Mshauri Maalum wa Rais; naomba ile Mshauri Maalum wa Rais tuiondoe katika mswada huu baada ya mashauri mengi ya Waheshimiwa Wajumbe.

Halkadhalika katika ufafanuzi Mshauri wa Rais ….

Mhe. Spika: Mhe. Waziri samahani, hebu rudia ili wajumbe wafuatilie kwa karibu.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Ahsante Mhe. Spika. Kwenye ukurasa wa 294 chini kabisa kule kuna Kiongozi wa Kisiasa, ambayo inaendelea mpaka ukurasa wa 295 juu kabisa ambapo kunaanzia Waziri, Spika wa Baraza la Wawakilishi, Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi na Mshauri Maalum wa Rais. Sasa nasema yule Mshauri Maalum wa Rais tuiondoe.

Halafu tuteremke chini hapo Mshauri wa Rais maana yake ni Mshauri wa Rais aliyeteuliwa na rais chini ya masharti ya kifungu cha 58 cha Katiba, kifungu hiki nacho pia tunakifuta katika mswada huu.

Mhe. Spika, ukurasa wa 297 kifungu cha 10(3) 'endapo Rais Mstaafu atafariki watoto wake waliochini ya umri wa miaka 18 watastahiki kulipwa pencheni' kifungu hicho nacho tunakiondoa. Ukurasa huo huo wa 297 kifungu cha 12(3), 'endapo Makamo wa Rais Mstaafu atafariki watoto wake waliochini ya umri wa miaka 18 watastahiki kulipwa na mengineyo' nacho kifungu hicho pia tunakiondoa.

Mhe. Spika, marekebisho haya yamekuja baada ya maoni ambayo tumeyapata kutokana na michango yenu Wahehsimiwa na zaidi baada ya kuthibitishwa na kamati.

Ukurasa wa 298 kile kifungu kilichopo cha 14(1) ambacho kinasema, "endapo Spika atafariki akiwa madarakani au atafariki baada ya kumaliza muda wake lakini alikuwa bado hajapokea mafao yake…". Sasa baada ya kifungu hicho cha 14(1) tuongeze na 14(2) ambacho kitasomeka kama ifuatavyo:-

"Endapo Spika Mstaafu atafariki basi mjane wake atastahiki kulipwa na mamlaka husika pencheni ya kila mwezi kwa miaka mitatu itakayokuwa sawa na asilimia maalum ya mshahara wa Spika aliyekuwa madarakani".

Hicho tunakiongeza kifungu cha 14(2).

Halafu mwisho wa kifungu cha 15 sasa tunaongeza kifungu cha 16 kwenye sehemu hiyo hiyo ya tatu mwishoni baada ya kifungu cha 15(1)(2) tunaongeza kifungu cha 16. Kifungu hicho kitasomeka kama ifuatavyo:-

“Endapo Rais, Makamo wa Rais au Spika wa Baraza la Wawakilishi atafariki wakati akiwa madarakani mtoto au watoto wao watahudumiwa na mamlaka husika hadi watakapotimia umri wa miaka 20 au ikiwa mtoto wa kike pale atakapoolewa au lolote litakalotokea mwanzo”

Hapa tumeondoa ile kwamba wapewe mshahara kama ilivyokuweko kwenye mswada wa mwanzo au mapendekezo ya mwanzo kuwa wapewe pencheni na mambo mengine yale tumeondoa. Sasa ilivyokuwa wale ni watoto na bado watakuwa tegemezi basi tumehisi kwamba bado watapatiwa huduma. Sasa hicho ndio kifungu cha 16 naomba tukiongeze.

Sasa naomba katika Sehemu ya Nne tubadili nambari, kwenye 16 tuweke 17 na penye 17 tuweke 18 mpaka mwisho wa mswada wote, yaani zile nambari zote zibadilike kwa sababu tumeongeza kifungu cha 16.

Mhe. Spika, mwisho wa mswada wenyewe yaani Sehemu ya Tano, Masharti Mengineyo sasa tukiangaloia ukurasa wa 300 mwisho ni kifungu 25 ambapo zamani ilikuwa 24. sasa tunaongeza kifungu cha 26 ambapo kifungu hicho kitasomeka kama ifuatavyo, nafikiri imeshasambazwa hiyo kopi ambayo nitaisoma.

“Bila ya kujali masharti ya kifungu cha 20 asilimia ya mshahara itakayowekwa chini ya kifungu hicho kwa ajili ya Mjumbe wa Baraza liliopo siku ya kuanza kutumika kwa sheria hii itakuwa kwa kima ambacho hakipungui ni sawa na asilimia mia moja ya mshahara ataokuwa anapata mjumbe huyo siku ya kuanza kutumika kwa sheria hii”.

Pili, “kwa ajili ya kuepusha utatanishi inaelezwa wazi kwamba,

(a) Nyongeza yoyote ya mshahara wa Mjumbe itayofanywa baada ya siku ya kuanza kutumika sheria hii haitahesabiwa kuwa ni sehemu ya mshahara wa Mjumbe kwa madhumuni ya masharti ya kifungu cha kwanza cha kifungu hiki.
(b) Baada ya Baraza liliopo siku ya kuanza sheria hii kuvunjwa kwa mujibu wa katiba, masharti ya kijifungu cha kwanza hayatatumika kwa Wajumbe wa Baraza litakalofuata baada ya hapo na badala yake masharti ya kifungu cha pili cha kifungu cha 20 ndio itakayotumika”.

Kwa ufupi tu Mhe. Spika, kile kikubwa ambacho kilitutanza au kutukwamisha mara ile ilikuwa ile asilimia maalum, sasa asilimia ile kwamba itaamuliwa basi sasa tumeiondoa na tumeweka kifungu hicho kama kilivyosambazwa hapa. Kwa hivyo, tunashukuru kamati imekubali na Waheshimiwa Wajumbe wote wa kamati wameridhia haya. Ni imani yetu kwamba kama lengo letu sote lilikuwa moja na tumeweza kukubaliana, cha msingi kwamba tunasisitizwa kuwa haitopungua kile kiinua mgongo kilichopita mwaka uliopita na kwa hesabu inaonesha tutakuwa

pazuri sina haja ya kuzitaja *figures*, lakini kwa kweli busara imetumika na nazidi kusisitiza kwamba busara itatumika ili mambo yetu yawe mazuri.

Lakini pia hapo hapo tumeongeza kifungu cha (3)(i) cha jadweli la kwanza kitasomeka 'ofisi katika uhai wake'. Yaani kwenye ukurasa wa 301 ile i, j, k, katika (i) basi tumeongeza 'ofisi katika uhai wake', baada nitakuja kufafanua yale mambo ambayo yalikuwa na mawazo tofauti na vipi tulivyokubaliana.
Mhe. Spika, kwa muhtasari hayo ndio makubaliano au ndio masahihisho. Lakini naomba bado sijamaliza, twende kwenye jadweli la nne ukurasa wa 304, fungu la mafao ya viongozi wa kisiasa, linasema chini ya kifungu cha 16(5) ambapo tunasema sasa tumerekebisha itakuwa chini ya kifungu cha 16. halafu ule mfano pia tumeuweka tu, lakini kwa kweli tunaweza tukauondoa.

Sasa hayo Mhe. Spika, ni marekebisho ambayo tuliyafanya baada ya kikao chetu cha mwisho pengine katika marekebisho yaliyosabazwa labda haya hayamo.

Mhe. Spika, kama nilivyosema kulikuwa na hoja kama sita ambazo Waheshimiwa wengi takriban wote baada ya ripoti ya Mwenyekiti wa Wenyeviti wao michango yao zaidi ilizidi kusisitiza michango ya Mhe. Mwenyekiti na kusisitiza yale ambayo Mhe. Mwenyekiti aliyatoa kwenye kamati. Mambo yenyewe sita ni kama ifuatavyo:-

1. Suala la asilimia maalum, nafikiri pale ndipo tulipokwazwa na tukashindwa hasa kuamua, lakini kwa busara zilizotumika na tunamshukuru sana Mhe. Mwanasheria Mkuu kwa kutukwamua kisheria na busara zake.
2. Ilikuwa ni muda muafaka wa mswada kuletwa Barazani, nalo hili tulilizungumza sana na Waheshimiwa wengi waliuliza kwa nini mswada unaletwa saa hizi? Tulikubaliana kwamba ni vyema mswada ukaletwa saa hizi kwa sababu sasa hivi ndio wakati wa kurekebisha mambo, ni wakati wa kuweka sawa mambo, lakini tukija bado mwaka mmoja au miezi sita tukaja kurekebisha kidogo haitoleta picha nzuri. Sasa hili tumehisi bora mambo yawekwe sawa sasa hivi.

Mhe. Spika, hoja ya tatu ambayo ni nzito kulikuwa na dhana kwamba labda viongozi wastaafu wa kitaifa watapata mafao makubwa sana na uchumi wetu mdogo. Lakini kwa kweli baada ya *analysis* ya hali ya juu na kuwaona kwamba hawa ni viongozi wetu na wametumikia nchi hii na wanastahiki kutazamwa kwa jicho la huruma basi sote tulikubaliana kwamba hiyo hiyo keki ndogo tuliyonayo na wao watazamwe.

Mhe. Spika, halafu kulikuwa na suala la ofisi kwa marais wastaafu ndio vile vifungu nilivyosema IJK. Kulikuwa na mawazo tofauti kwamba wazee wetu hawa wakishastaafu kwa nini wapatiwe ofisi, wengine wakashauri labda watumie ofisi nyumbani kwao. Lakini kwa kweli busara imetumika na ikaonekana kwamba hawa viongozi wetu baadhi yao sio wote bado wanao uwezo na nguvu za kutumikia nchi. Kwa hivyo, tumeamua kwamba tuwapatie ofisi moja zile gharama tulizosema zitakuwa kubwa za uendeshaji zitapungua wakiwa wote chini ya *block* moja. Nafikiri hii tumekubaliana na tumeona kwamba ni vyema kwa kweli bado wengine wanaandika vitabu, wengine wanakuwa washauri, wana kazi nyingi.

Mhe. Spika, suala jengine ambalo lilijadiliwa sana ni Washauri wa Rais. Sote tulikubaliana kwamba kikatiba Mhe. Rais anao uwezo wa kuteua washauri wake, lakini ikashauriwa kwamba aaa kwa mswada huu bora wasiwemo humu watafutiwe mwamvuli mwengine ambako huko watatazamwa kimafao. Nafikiri tumekubaliana na sisi kama serikali tumekubaliana hivyo kwamba kikatiba Mhe. Rais anao uwezo huo na atawateua na watamsaidia kazi zake lakini kimafao basi watatazamwa katika mwamvuli mwengine.

Mhe. Spika, kulikuwa na hoja nyengine nzito ambayo ilijitokeza ni matunzo ya watoto wa viongozi wakuu wastaafu. Hili nalo tumepokea sana maoni yenu na ilifahamika hata nje huko kwamba hata mtoto analipwa, kweli mawazo yale tumeyasikia na tukasema hapana wale watahudumiwa lakini sivyo sasa kama vile ilivyokuwa mwanzo. Hizo sheria ukitazama hata mwanzo huko zilikuwa zinasema atapewa mchele kilo 2, atapewa mayai, ile kidogo haipendezi. Sasa yote yale tunayaweka pamoja na tunasema kwamba watoto wale watahudumiwa lakini tutaangalia serikali watahudumiwa vipi.

Lakini Mhe. Spika, naomba nisisitize sana kwamba nashukuru sana busara ambazo zimeoneshwa Mwenyekiti wa Kamati ya Wenyeviti pamoja na wajumbe wenzake na Waheshimiwa Wenyeviti walioalikwa katika mazungumzo yetu yale ya mwisho tulizungumza kwa kuelewana sana na yale ambayo yalitukwaza huko nyuma tukaweza kuyaweka sawa.

Mhe. Spika, kwa kweli ninachoweza kusema kwamba kwa upande wa majumuisho hakuna zaidi ya haya. Sasa mimi naweza kusema kwamba katika kile kifungu cha 26 ambacho tumekiongeza 1, 2 na 3 katika jadweli, jadweli la kwanza litasomeka ofisi katika uhai wake, ile ofisi itakuwa *maintained* na serikali mpaka wakati wa uhai wake wote. Ile tumeiongeza pale naona nayo ina umuhimu wake.

Mhe. Spika, nafikiri baada ya maelez haya mimi niwashukuru sana Waheshimiwa Wajumbe na ninaamini marekebisho tuliyoyafanya kama serikali na tuliyoyafanya pamoja hapa Barazani yamekidhi haja na ni imani yangu kwamba sote tumeshirikiana basi tumalize vyema ngwe yetu hii iliyobaki.

Mhe. Spika, naomba kutoa hoja.

Mhe. Spika: Ahsante sana, nimemuona na Mwenyekiti wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa ameunga mkono. Maana huyu Mwenyekiti mzito akisimama basi mambo yote yanakaa sawa.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Spika, naomba kutoa taarifa kwamba sasa Baraza lako tukufu likae kama Kamati ya Baraza Zima ili iweze kupitia mswada kifungu baada ya kifungu.

KAMATI YA BARAZA ZIMA

Mswada wa Sheria ya Maslahi ya Viongozi wa Kisiasa ya Mwaka 2011

(Kusomwa mara ya kwanza)

Kifungu cha 1 - Jina fupi na kuanza kutumika.
Kifungu cha 2 - Matumizi.
Kifungu cha 3 - Ufafanuzi pamoja na marekebisho yake.
Kifungu cha 4 - Stahiki ya kulipwa mafao.
Kifungu cha 5 - Kukosa sifa za kulipwa mafao.
Kifungu cha 6 - Mamlaka husika.
Kifungu cha 7 - Kupokea mafao kwa utaratibu mwengine.
Kifungu cha 8 - Mafao kulipwa kutoka kwenye mfuko mkuu.
Kifungu cha 9 - Mafao anayostahiki kulipwa Rais Mstaafu.
Kifungu cha 10 - Mafao yatakayotolewa kwa warithi wa Rais Mstaafu pamoja na marekebisho yake.
Kifungu cha 11 - Mafao yatakayolipwa kwa Makamo wa Rais Mstaafu pamoja na marekebisho yake.
Kifungu cha 12 - Mafao yatakayolipwa kwa warithi wa Makamo wa Rais Mstaafu pamoja na marekebisho yake.
Kifungu cha 13 - Mafao yatakayolipwa kwa Spika Mstaafu.
Kifungu cha 14 - Mafao yatakayolipwa kwa warithi wa Spika Mstaafu pamoja na marekebisho yake.
Kifungu cha 15 - Kusita kwa mafao maalum.
Kifungu cha 16 - Huduma za wategemezi pamoja na marekebisho yake.
Kifungu cha 17 - Mafao kwa viongozi wengine wanaoshika ofisi ya kisiasa pamoja na marekebisho yake.
Kifungu cha 18 - Malipo ya mafao kwa warithi wengine wa viongozi pamoja na marekebisho yake.
Kifungu cha 19 - Ugawaji wa mafao kwa warithi pamoja na marekebisho yake.
Kifungu cha 20 - Kuzingatiwa kwa asilimia maalum pamoja na marekebisho yake.
Kifungu cha 21 - Kanuni pamoja na marekebisho yake.
Kifungu cha 22 - Kufuta na kubakiza pamoja na marekebisho yake.
Kifungu cha 23 - Marekebisho ya jadweli pamoja na marekebisho yake.
Kifungu cha 24 - Mkopo kwa kiongozi wa kisiasa pamoja na marekebisho yake.

Kifungu cha 25 - Mafao kwa mjane wa kiongozi wa kisiasa pamoja na marekebisho yake.
Kifungu cha 26 -

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Mwenyekiti, kifungu cha 26 ndio kile kipya ambacho kimeongezwa na kimegaiwa kwenye *paper*. Lakini kina kifungu cha 1 na cha 2, kile kifungu cha 3 kilichomo kwenye ile karatasi si sehemu ya kifungu cha 26.

Ile ni marekebisho mengine ya jadweli lakini hayaingii katika kifungu cha 26. *Marginal note* yake ni Masharti ya Mpito.

Kifungu cha 26 - Masharti ya Mpito.

(Baraza lilirudia)

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Spika, ilivyokuwa Kamati ya Baraza Zima imeupitia mswada wangu kifungu kwa kifungu pamoja na marekebisho yake sasa naliomba Baraza lako tukufu liukubali.

Naomba kutoa hoja.

Mhe. Spika: Ahsante Mhe. Waziri, niwahoji sasa Waheshimiwa Wajumbe wale wanaokubaliana na mswada huu pamoja na marekebisho yake wanyanyue mikono, wanaokataa, waliokubali wameshinda.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mswada wa Sheria ya Maslahi ya Viongozi wa Kisiasa ya Mwaka 2011

(Kusomwa mara yaPili)

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Spika, naomba kutoa hoja kwamba Mswada wa Sheria ya Maslahi ya Viongozi wia Kisiasa ya Mwaka 2011 pamoja na marekebisho yake usomwe kwa mara ya pili.

Mhe. Spika: Niwahoji Waheshimiwa Wajumbe wale wanaokubaliana na mswada huu katika kusomwa mara ya pili wanyanyue mikono, wanaokataa, waliokubali wameshinda.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

(Mswada wa Sheria ya Serikali ulisomwa mara ya pili na kupitishwa)

Mhe. Spika: Naomba nichukue nafasi hii kuwashukuru sana Waheshimiwa Wajumbe kwa kazi nzuri na kwa kweli hekima mnayotoa kwangu na kwa wasaidizi wangu katika kuendesha shughuli zetu zikaenda kwa ufanisi.
Huu ni mswada mmoja wapo ambao ulikuwa na vigingi vizito lakini baada ya hekima kubwa waliyonayo Waheshimiwa Wajumbe tukakubaliana kufikia pahala kwamba mswada huu hebu Mhe. Waziri akaonane na kamati inayohusika. Kwa busara kamati hiyo ilijumuisha pamoja na wenyeviti mbali mbali wa kamati nyenginezo na hata baadhi ya viongozi wenzetu humu ndani pia nao walishirikishwa ili kile kinachotoka pale kiwe ni kitu thabiti kinachokubaliwa kwa pamoja yetu.

Nichukue nafasi hii basi kukushukuruni lakini kuomba kwenu kwamba utaratibu wa aina hii kunapokuwa na mambo mazito basi ni sisi wenyewe ndio wa kuyaamua wala hakuna mgeni au mtu mwengine ambaye anaweza akasaidia jambo hili zaidi ya sisi wenyewe.

Sisi ndio viongozi wa nchi hii na wananchi wanatusikiliza. Niwashukuru wananchi kwamba wanafuatilia kwa karibu sana masuala yetu na pale ambapo wanaona kuna matatizo kati yetu basi kwa kweli wanakuwa hawapati faraja, isipokuwa pale wanapoona kwamba kwa pamoja yetu tumeungana katika kuendesha mambo yetu kwa ajili yao basi kwa kweli wanapata faraja sana. Niwashukuru sana kwa kufanya kazi nzuri ya wananchi. Ahsanteni sana.

Mswada wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Tume ya Mipango Nam. 5 ya 1989 na Kutunga Sheria Mpya kwa ajili ya Uendeshaji wa Tume ya Mipango Zanzibar, Kazi zake, Uwezo wake na mambo mengine yanayohusiana na hayo

(Kusomwa mara ya kwanza)

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo: Mhe. Spika, kwa ruhusa na idhini yako naomba kuwasilisha Mswada wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Tume ya Mipango Nam. 5 ya 1989 na Kutunga Sheria Mpya kwa ajili ya uendeshaji wa Tume ya Mipango Zanzibar, Kazi zake, Uwezo wake na mambo mengine yanayohusiana na hayo.

Lakini kabla sijawasilisha mswada huu napenda kuchukua fursa hii kuishukuru kwa dhati Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo ya Baraza lako tukufu inayoongozwa na Mhe. Salmin Awadh Salmin kwa michango yake katika Ofisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo ikiwemo kupitia na kutoa maoni katika rasimu ya awali ambayo yamesaidia sana katika kukamilisha mswada huu kwa wakati.

Mhe. Spika, Serikali ya Mapinduzi Zanzibar ilianzisha Tume ya mwanzo ya Mipango kati kati ya miaka ya 70 wakati tukiwa na mfumo wa *Central Planning*. Baadae shughuli za tume zilihamishiwa katika Wizara ya Mipango ambako kulikuwa na Idara ambayo ilikuwa ni Sekretarieti ya Tume. Mabadiliko zaidi ya uendeshaji wa tume yalifanywa miaka ya 80 ambapo sheria ilipitishwa ya kuanzisha Tume ya Mipango ikiwa ni chombo kinachotegemea.

Mhe. Spika, Tume ya Mipango imeanzishwa kwa kuzingatia Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984 sura ya 12 na imepewa mamlaka ya kuwa ni chombo cha juu kisheria cha kupanga na kusimamia utekelezaji wa mipango ya kitaifa ya maendeleo katika ukuzaji uchumi na maendeleo ya kijamii kwa ujumla.

Kufuatia Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2010 serikali imedhamiria kuunda upya na kuimarisha Tume ya Mipango na tayari Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi amemteua Katibu Mtendaji wa Tume ya Mipango kwa dhamira hiyo ya kuimarisha tume. Kutokana na dhamira hiyo, serikali imeona haja ya kuifanyia marekebisho sheria ya tume ili iweze kwenda sambamba na mwelekeo na shabaha za serikali.

Mhe. Spika, madhumuni makuu ya kuifanyia mapitio tume ni pamoja na kuangalia muundo mzima kiutawala ikiwemo wajumbe na sekretarieti na kisheria ili kufanyia marekebisho yanayostahiki katika kutekeleza lengo la serikali la kuifanya Tume ya Mipango kuwa kisima cha mawazo sahihi yaani *think tank* kitakachoelekeza hatua za kufuata ili kufikia malengo ya serikali ya kunyanyua hali za wananchi wake.

Mbali na muundo wa kiutawala mapitio yaliyokusudia kubainisha kwa uwazi zaidi majukumu na kazi za tume na namna ya utendaji wake kwa ujumla pamoja na idara zilizo chini yake.

Mhe. Spika, madhumuni ya taarifa hii ni kuwasilisha rasimu ya Mswada wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Tume ya Mipango Nam. 5 ya 1989 na Kutunga Sheria Mpya kwa ajili ya uendeshaji wa Tume ya Mipango Zanzibar, Kazi zake, Uwezo wake na mambo mengine yanayohusiana na hayo. Kwa dhamira ya kupata maoni kwa ukamilishaji na hatimaye kuupitisha mswada wa sheria hii.

Mhe. Spika, kupitia Baraza hili tukufu inakusudiwa:

1. Kupata michango ya Waheshimiwa Wajumbe ili kuimarisha rasimu ya mswada huu.
2. Kupata baraka za Waheshimiwa Wajumbe ili kuendelea na taratibu nyengine za ukamilishaji wa sheria.

Mhe. Spika, serikali kwa kipindi kirefu imekuwa ikichukua juhudi za kupanga na kutekeleza mipango ya maendeleo ili kuimarisha uchumi na ustawi wa jamii. Pamoja na mafanikio yaliyopatikana kumekuwa na changamoto mbali mbali zikiwemo uwezo mdogo wa rasilimali watu, uhaba wa fedha na miundombinu hafifu ya kiuchumi.

Mhe. Spika, kwa upande mwengine kukosekana kwa Tume ya Mipango iliyo imara kumechangia kutokupatikana kwa mwelekeo mzuri wa maendeleo ya kiuchumi na kijamii kama inavyotarajiwa. Aidha, mabadiliko ya kiuchumi duniani yanahitaji taasisi imara ya kuweza kukabiliana na changamoto hizi ili kuweza kuunganisha wadau wote na kuleta mapinduzi ya kifikra za kimaendeleo. Hali hii inahitaji kuwepo kwa Tume ya Mipango iliyo madhubuti kiutendaji, kimaamuzi na kiutaalam.

Mhe. Spika, tume ya awali iliyoundwa chini ya sheria ya mwaka 1989 ilikuwa na wajumbe wasiozidi 7 akiwemo Rais ambaye ni Mwenyekiti. Mwaka 1996 sheria ilifanyiwa marekebisho

na wajumbe wa tume waliongezeka kutoka 7 hadi 9. Aidha, kulikuwa na Kmati za Mipango kwa kila Wizara na Mikoa ambazo zilijulikana kama Kamati ya Mipango ya Wizara au Kamati ya Mipango ya Mkoa. Katibu Mkuu wa Wizara inayoshughulikia na masuala ya Mipango alikuwa ndio Katibu wa Tume.

Mhe. Spika, mapitio ya uzoefu wa Tume za Mipango za Zanzibar zilizopita na zile za nchi mbali mbali zimeonesha kuwa kuna mambo mengi ambayo yanafanana katika nchi hizi. Lakini vile vile kuna tofauti kubwa kwa baadhi ya mambo kama ifuatavyo:

1. Katika nchi nyingi tume zinachukua uhalali wake kwa kuingizwa kwenye katiba au katika sheria za kuanzisha taasisi hizi. Ni nchi chache tu ambazo uanzishwaji wa Tume ya Mipango upo kwa njia ya kiutawala *(administrative order).* Mfano wa nchi hizo ni India.
2. Nchi nyingi Tume za Mipango zinaongozwa na viongozi wa nchi yaani Marais au Mawaziri Wakuu kama Wenyeviti kulingana na mfumo wa utawala wa nchi husika. Hata hivyo, ziko nchi chache ambazo tume zinazoongozwa na watu wengine. Katika hali hii Mwenyekiti huwa ni mtu maarufu mwenye uzoefu, nguvu na heshima kubwa kwa taifa kama ilivyo kwa nchi ya Namibia.
3. Kimajukumu Tume za Mipango zote ni Mshauri Mkuu yaani *think tank* wa Serikali Kuu kwa masuala ya uandaaji na utekelezaji wa mipango ya maendeleo na usimamizi wa uchumi wa kitaifa. Kwa mantiki hii, tume nyingi zinakuwa ni vyombo vinavyojitegemea.
4. Kazi kuu ya tume nyingi ni kuandaa, kuratibu na kusimamia mipango ya maendeleo ya nchi husika.
5. Katika nchi mbali mbali ikiwemo Nigeria na Tanzania Bara tume zina jukumu la kuimarisha mahusiano ya kiuchumi na nchi nyengine.
6. Baada ya kuidhinishwa kwa majukumu ya kuratibu ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa programu za miradi ya maendeleo, ni kazi moja wapo ya msingi ya Tume za Mipango.

Mhe. Spika, mswada huu una sehemu 6 na vifungu 33 kama ifuatavyo:

Sehemu ya kwanza inahusu Utangulizi ambao unaelezea Jina Fupi na tarehe ya kuanza kutumika sheria iliyopendekezwa pamoja na tafsiri ya baadhi ya maneno yaliyotumika katika mswada huu.

Sehemu ya pili inahusu Kuanzishwa, Kazi na Uwezo wa Tume. Sehemu hii ina vifungu 18 kuanzia kifungu cha 3 hadi kifungu cha 21. Kifungu cha 3 kinahusu Kuwepo kwa Tume ya Mipango. Kifungu cha 4 kinahusu Muundo wa Tume.

Kifungu cha 6 kinahusu Sekretarieti ya Tume. Kifungu cha 7 kinahusu Kiapo cha Utii kwa Wajumbe wa Tume. Kifungu cha 8 ni kuhusu Kazi. Kifungu cha 9 ni kuhusu Uwezo ambao kimsingi umegawika kama ifuatavyo:

(a) Kazi za mipango ya maendeleo ya kitaifa zilizotajwa chini ya kifungu cha 11.
(b) Uratibu wa mipango ya maendeleo ya kisekta ambayo imeelezwa chini ya kifungu cha 12.
(c) Kufuatilia na kutathmini kumeelezwa chini ya kifungu cha 14.
(d) Mpango wa watenda kazi na demografia umeelezwa chini ya kifungu cha 15 na

(e) Usimamizi wa takwimu chini ya kifungu cha 16

Tume ikiwa ni chombo cha kitaalamu imeelezwa chini ya kifungu cha 13. Kifungu cha 17 kinaeleza kuhusu sekreterieti ya tume na kazi zake, kuelezwa katika kifungu cha 18. Kifungu cha 19 ni kuhusu uteuzi wa wakuu wa idara. Kifungu cha 20 ni kuhusu wafanyakazi wa tume na kifungu cha 21 ni uhusiano na ushirikiano wa tume.

SEHEMU YA TATU

Mhe. Spika, sehemu hii ni kuhusu utendaji wa Tume ambayo ina vifungu viwili. Kifungu cha 22 ni kuhusu uwezo wa Tume kuhitaji taarifa na kifungu cha 23 ni mawasiliano kwa tume.

SEHEMU YA NNE

Mhe. Spika, sehemu ya nne ni kuhusu vifungu vya Tume ambayo ina vifungu vinne. Kifungu cha 24 kinahusu vikao vya tume, kifungu cha 25 kinahusu uamuzi wa Tume, kifungu cha 26 ni kuhusu kumbukumbu za vikao vya tume na kifungu cha 27 ni kuhusu malipo na posho kwa wajumbe wa tume.

SEHEMU YA TANO

Sehemu hii ya tano ni kuhusu masharti ya fedha ambayo ina vifungu vitatu, vyote vikihusu suala la fedha kwa Ttume, kama vile fedha za Tume, makisio, hesabu na ukaguzi wa shughuli za fedha za Tume.

SEHEMU YA SITA

Sehemu hii ya sita inahusu masuala mbali mbali ina vifungu vitatu, kifungu cha 31 ni kuhusu kuanzishwa kwa kamati na idara. Kifungu cha 32 kinatoa uwezo kwa Waziri kutunga kanuni na kifungu cha 33 kinaelezea kufutwa kwa sheria nambari 5 ya mwaka 1989 na kubakiza.

MAPENDEKEZO

Mhe. Spika, Ili Tume ya mipango iweze kusimamia vizuri utekelezaji wa majukumu yake, inapendekezwa kwamba sheria ya Tume ya mipango nambari 5 ya mwaka 1989 kufutwa na kutungwa sheria mpya.

HITIMISHO

Mhe. Spika, uundwaji wa Tume mpya ya mipango kwa sasa ni muhimu kutokana na changamoto zilizopo na zijazo katika maendeleo ya nchi. Aidha watendaji na uwezo wa utendaji kazi kwa Tume ni muhimu, ili tuweze kufikia malengo ya Dira ya maendeleo ya 2020 na mkuza.

Mhe. Spika, Baraza lako tukufu naliomba kupokea, kuchangia, kuelekeza na hatimaye kuukubali mswada huu wa mapendekezo ya kufutwa sheria ya Tume ya Mipango nambari 5 ya mwaka 1989 na sheria mpya kutungwa ambayo inatoa muongozo juu ya uendeshaji wa Tume ya Mipango ya Zanzibar.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo sasa naomba kutoa hoja.

Mhe. Abdalla Mohammed Ali (Kny: Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo): Mhe. Spika, awali ya yote naomba nichukue nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu

(*Subhana Wataala*) kwa kutujaalia uzima wa afya na tukaweza kuhudhuria katika Baraza lako tukufu, na wale waliokuwa wagonjwa Mwenyezi Mungu awajaalie wapone haraka ili tuweze kuungana nao katika kutekeleza majukumu yetu ya kila siku.

Pili, nikushukuru wewe Mhe. Spika kwa kunipatia nafasi hii ya mwanzo kutoa maoni kwa niaba ya Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo yanayohusiana na mswada huu wa Sheria ya Kufuta Sheria ya ya Tume ya Mipango Nam. 5 ya mwaka 1989 na kutunga Sheria Mpya ya Mipango ya Zanzibar, Kazi zake, Uwezo wake na Mambo Mengine yanayohusiana na hayo.

Mhe. Spika, naomba uniruhusu nitoe mkono wa pole kwa Wazanzibari na Watanzania wote kwa msiba uliotufikia hivi karibuni wa Mjumbe mwenzetu Marehemu Salum Amour Mtondoo aliyekuwa Mwakilishi wa kuchaguliwa na wananchi kupitia Jimbo la Bububu. Pole hizi ziifikie familia yake na wananchi wote wa Jimbo la Bububu tukielewa kwamba msiba huu ni wetu na unamgusa kila mmoja wetu; kwetu sisi ni kusema tu *Inalillahi Wainnailaihi Rajiuun***.** Tuendelee kumuombea Dua kwa Mwenyezi Mungu mwenzetu alietangulia amlaze mahala pema Peponi AMIN. Nasi tuliobaki atupe moyo wa subra.

Mhe. Spika, aidha, nitumie nafasi hii ulionipa kwa kuwashukuru sana Waheshimiwa Wajumbe wenzangu wa Kamati kwa mashirikiano yao ya dhati kabisa waliyonipa kwa muda wote tulipokuwa tukifanya kazi ya kuupitia Mswada huu, mawazo na michango yao naithamini sana.

Mhe. Spika, naomba niwataje waheshimiwa hao kwa majina kama ifuatavyo:

1. Mhe. Salmin Awadh Salmin - Mwenyekiti
2. Mhe. Abdallah Mohamed Ali - Makamo Mwenyekiti
3. Mhe. Mahmoud Muhamed Mussa - Mjumbe
4. Mhe. Rufai Said Rufai - Mjumbe
5. Mhe. Raya Suleiman Hamad - Mjumbe
6. Mhe. Mlinde Mabrouk Juma - Mjumbe
7. Mhe. Bikame Yussuf Hamad - Mjumbe
8. Ndg. Amour Mohammed Amour - Katibu
9. Ndg. Shemsa Maabad Mohamed - Katibu

Mhe. Spika, napenda nichukue fursa hii vile vile kwa kumpongeza Mhe Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo kwa kufikiria na kuandaa Mswada huu muhimu sana na kuuwasilisha mbele ya Baraza lako Tukufu ili ujadiliwe na hatimae upitishwe.

Pongezi hizi pia ziwaendee Katibu Mkuu wa Wizara hii, Katibu Mtendaji wa Tume ya Mipango pamoja na viongozi na watendaji wengine wote walioweza kusaidia kwa namna moja au nyengine kuandaa Mswada huu. Kwa kweli Mhe. Spika watendaji hawa wamekuwa ni washauri wazuri kwake yeye binafsi Mhe. Waziri lakini pia wametoa mashirikiano mazuri pamoja na maelekezo yenye ufafanuzi wa kina kwa Kamati yetu muda wote tulipokuwa tunajadili na kuupitia mswada huu,

Mhe. Spika, sote tunaelewa kwamba kupanga ni kuchagua; na bila ya mipango madhubuti hatutakuwa na maamuzi sahihi katika kuchagua lipi lifanyike na lifanyike kwa wakati gani. Hilo pia linaweza likatusaidia kuweza kujua kutokana na rasilimali zetu basi ni mambo mangapi

tunaweza kuyapanga kwa wakati mmoja na mangapi yanaweza kusubiri kuliko kuyavamia mambo mengi kwa wakati mmoja na ambayo hatuna uwezo wa kuyakamilisha.

Mhe. Spika, mipango hii kamwe haitapangika hewani, ni lazima kuwe na chombo madhubuti cha kuweza kuratibu na kuiendeleza. Kwa vile nchi yetu ina rasilimali chache kuliko mahitaji yetu, hivyo basi serikali kwa makusudi ilianzisha utaratibu wa kupanga tangu miaka ya sabiini. Pamoja na kwamba baadae shughuli zake zote zilikuwa chini ya Idara ya Mipango (wakati ule) ilionekana ni busara yafanyike marekebisho. Hivyo Tume ya Mipango chini ya Sheria Nam. 5 ya mwaka wa 1989 ilianzishwa ambayo ndio leo kwa mswada uliopo mbele yetu tunakusudia kuifuta na kutunga sheria nyengine mpya kwa ajili ya uendeshaji wa Tume.

Mhe. Spika, Sheria hii tunayoikusudia kuitunga madhumuni yake makubwa ni kuunda chombo madhubuti chenye kujitegemea kwa mujibu wa matakwa ya Katiba, lakini kubwa kinakusudiwa kiwe chombo cha kitaalamu ili kiweze kuendana na wakati tulionao. Kwa maana hiyo mapendekezo ya muundo na uwezo wa Tume hii yataweza kutekeleza majukumu yake ya kimsingi katika kufanya kazi za maendeleo ya kitaifa kama zilivyoainishwa kwenye kifungu cha 11, kitaratibu mipango ya maendeleo ya kisekta ambayo imeelezewa chini ya kifungu cha 12, Tume itasimamia na kutathmini mipango hiyo na pia itaandaa mipango ya rasilimali watu na demografia

Mhe. Spika, moja kati ya changamoto kubwa iliopo Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali ni namna ambavyo takwimu zake zisivyotumika kikamilifu. Tume hii kwa makusudi, moja katika kazi yake ni Usimamizi wa Takwimu hizo. Mswada huu kwenye kifungu cha 16 umeeleza ni kwa namna gani Tume itakavyozitumia taarifa hizo za takwimu na kutoa ushauri kwa serikali juu ya mipango ya maendeleo ya kiuchumi na ile ya shughuli za kijamii.

Mhe. Spika, Kamati yetu ya Fedha, Biashara na Kilimo ina matarajio mazuri sana kwa Tume hiyo mpya ambayo itajengwa na wataalamu na kwa maana hiyo yenyewe itakuwa ni chombo cha kitaalamu kama kifungu cha 13 kinavyofafanua.

Mhe. Spika, wakati wa kuupitia Mswada huu kwa pamoja na Mhe. Waziri tuligundua marekebisho madogomadogo mengi ambapo mengine ni makosa ya kiuandishi (*Spelling mistakes*) baadhi ya maneno yalibadilishwa ili kuweka tafsiri nyepesi na yenye kueleweka kwa maana ile ile iliyokusudiwa na vile vile baadhi ya vifungu kuviandika upya katika maana ile ile ya kuhakikisha kwamba vinaeleweka vizuri.

Mhe. Spika, baadhi ya vifungu vilivyoandikwa upya ni kama vile kifungu cha 8(1) (c), 8(1) (f), 9(1) (g), 11(d) na cha 13. Aidha Kamati ilikubaliana na Mhe. Waziri kukifuta kifungu cha 4(4) kwasababu kifungu cha 24(3) maelezo yake yamekidhi haja hiyo na hivyo kuwepo kwake ni kujirejea tu.

Mhe. Spika, kwa vile marekebisho yameonekana mengi Kamati iliona ni vyema mswada huo ukachapwa upya ili Waheshimiwa Wajumbe wausome kwa vizuri zaidi. Nadhani kila Mheshimiwa Mjumbe ameshaupata.

Mhe. Spika, Kamati yetu kwa mara nyengine inaikumbusha Serikali katika suala zima la kuwatunza wataalamu wetu ili waendelee kuitumikia nchi yetu kwa moyo, jambo ambalo litaleta ufanisi wa kazi na kuwa ndio kichocheo cha maendeleo, tunaamini kwamba Tume itakuwa ndio chemchem ya maendeleo yetu katika maamuzi ya vipaumbele vyetu.

Mhe. Spika, safari ya kuelekea kwenye uchumi imara ni ndefu na inachukuwa muda mrefu. Ngazi ya kufikia lengo hilo si nyengine isipokuwa ni mipango mizuri yenye kuelezeka na kutekelezeka. Tusijaribu hata kidogo Tume yetu kuifanya kuwa ni ya kisiasa katika utekelezaji wa majukumu yake bali iwe ni ya kitendaji zaidi. Pamoja na kwamba mapendekezo ya mipango hiyo hatimae maamuzi yake yatapitia kwa wanasiasa lakini mtazamo mkubwa utakaofikiriwa ni maendeleo na si vyenginevyo.

Mhe. Spika, kwa ujumla Kamati yetu imekubaliana na mapendekezo ya Mswada huu ikiwa ni pamoja na marekebisho yake, hivyo tunawaomba Waheshimiwa Wajumbe wenzetu waupokee, waujadili na hatimae waupitishe na kuwa sheria.

Mhe. Spika, kwa niaba ya Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo na kwa niaba ya Wananchi wa Jimbo la Mkoani naunga mkono mswada huu.

Mhe. Spika, naomba kuwasilisha.

Mhe. Spika: Ahsante sana Mhe. Abdalla Mohammed Ali kwa kuwasilisha taarifa ya kamati kwa niaba ya mwenyekiti. Waheshimiwa Wajumbe, nimeombwa na Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo, kuna jambo ametumwa na Mhe. Rais. Kwa hivyo, sasa naomba atoe taarifa hiyo na nimeona ni jambo muhimu kwa sababu ni taarifa ambayo sisi wajumbe tuliomba, kwa hivyo nadhani kuna kitu anataka atupe taarifa kutoka kwa Mhe. Rais. Mhe. Waziri nakuruhusu kutoa taarifa hiyo.
Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Fedh, Uchumi na Mipango ya Maendeleo: Mhe. Spika, ni kweli, lakini nilikuwa naomba tuendelee na shughuli zetu, tutakapofikia kumaliza ndio nitawapa Waheshimiwa Wajumbe hiyo taarifa.

Mhe. Spika: Nafikiri ameona kwamba taarifa nzuri hiyo, inaweza ikafanya furaha kubwa na mjadala usiendelee vyema. Basi tuendelee na sasa naomba nimkaribishe Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa kuendelea na mchango.

Mhe. Mahmoud Mohammed Mussa: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kunipa nafasi ya kuweza kuchangia katika mswada wetu huu ambao umewasilishwa hapa. Mhe. Spika, kwa kweli sina mchango mkubwa sana katika maelekezo haya ambayo nataka kutoa sasa hivi, kwa sababu kazi kubwa tumekwisha kuifanya katika kabrasha hili ndani ya kamati, ambapo ilikuwa tumeshughulika kwa umoja wetu.

Kwa hivyo Mhe. Spika, mimi nilikuwa nataka kuzungumzia suala zima juu ya mapato katika nchi yetu. Pamoja na utaratibu huu ambao tumeshaukubali sasa hivi wa kuunda Tume hii ya mipango, lakini bado tuna matatizo katika nchi yetu, juu ya ukusanyaji wa mapato. Kwa hivyo, pamoja na kazi kubwa ambayo itakuwa inafanywa na Tume hii ya mipango na majukumu ambayo tumeyapanga humu, lakini kuna suala hili la ukusanyaji wa mapato tungependa vile vile,

hii timu ambayo itakuwa inashughulikia suala la Tume ya mipango, vile vile itengeneze utaratibu wa kuboresha njia bora za kukusanya mapato katika nchi yetu.

Mhe. Spika, kwa sababu utaratibu ambao tunakwenda nao sasa hivi Mhe. Spika, nikiri kwamba ni utaratibu ambao umepitwa na wakati. Kwa hivyo, basi tutumie fursa hii kwa Tume hii ambayo tunaiunda sasa hivi ili tuhakikishe kwamba tunaboresha zile njia kuu za ukusanyaji wa mapato, pamoja na kuzidi kuziba ile mianya ambayo inapoteza mapato yetu katika nchi yetu.

Vile vile tunaiomba basi hii Tume ambayo itakuwa inashughulikia masuala haya kufanya makisio na matayarisho kwa sababu ya kupata mapato hususan yanayotokana na vyanzo vyetu kama mfano katika sekta ya mafuta.

Mhe. Spika, sekta hii kwa kweli mapato ya serikali yanapotea sana, tunaomba basi kwa kuptia Tume hii tutengeneze mipango imara, tufanye marejeo ya sheria zetu zaidi hususan katika masuala ya mafuta.

Baada ya maelekezo hayo Mhe. Spika, ningeomba mimi niishie hapo, ahsante Mhe. Spika, naunga mkono hoja.

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipatia nafasi hii na mimi kuweza kuchangia kidogo kuhusu mswada huu. Kwanza nimshukuru Allah kwa kutupa uhai na nampongeza Mhe. Waziri kwa kuleta mswada huu kwa vile unamahitaji ya kuwepo.

Mhe. Spika, mimi kidogo nina mashaka na muundo wa hii Kamisheni. Mhe. Spika, muundo huwa unategemea na madhumuni. Ikiwa madhumuni ni *think tank* kama alivyosema waziri basi kidogo muundo wake unaleta wasi wasi kidogo.

Kwanza, kwa nini nikasema unaleta wasi wasi, kwa sababu Mhe. Rais ndio kiongozi mkuu wa nchi, sasa hawezi tena yeye akaingia katika kamisheni na kamisheni ripoti yake inakwenda katika Baraza la Mapinduzi. Imetajwa hapa Mhe. Spika, katika kifungu cha 3 cha mswada huu sehemu ya pili kifungu cha 3, inasema

Kifungu cha 3

> “Kutakuwa na tume ya mipango ya Zanzibar kama ilivyoelezwa katika katiba hii, ambayo itakuwa ni chombo cha serikali kilicho huru na kinachotegemea ndani ya utumishi wa umma”.

Sasa chombo ambacho ni cha serikali, hiki chombo ndicho kilichotakiwa kiwape maelekezo Rais pamoja na Baraza la Mapinduzi. Lakini ikiwa Rais yumo katika hiki chombo haya mawazo haya yatapelekwa wapi, hili swali la kwanza.

Swali la pili. Huu mswada unatatanisha kidogo Mhe. Spika, kwa ule wa Kiingereza na ule wa Kiswahili. Sasa mimi nimeshindwa hata kuangalia nichangie kitu gani hapa katika muundo. Ukisoma kifungu cha 4 kwa mswada ule wa Kiswahili tume itajumuisha Rais ambaye atakuwa ndio Mwenyekiti, Makamu wa Kwanza wa Rais, Makamu wa Pili wa Rais, mawaziri na wajumbe wengine wa Baraza la Mapinduzi. Wote hawa ni Baraza la Mapinduzi tu.

Lakini ukija kwenye mswada wa Kiingereza unasema, *The commission consists of members whose number including the chairman shall not exceed seven. The charman of the commission shall be president.*

Halafu vifungu vyengine, *the members of the commission shall be the Vice Chairman who shall be appointed by the President.* Haikutajwa hapa *Revolutionary Council Members*. Sasa unatatanisha baina ya huu wa Kiswahili na huu wa Kiingereza sasa tuuchukue upi sisi, huu wa Kiswahili ndio sawa au huu wa Kiingereza ndio sawa. Hilo swali la pili.

Swali la tatu Mhe. Spika, ni lile nililosema pale, kwamba mswada kifungu cha 7, kuhusu *Powers of the Commission,* yaani nguvu za kamisheni yenyewe au uwezo wake.

Mhe.Spika, katika kifungu cha 7 cha mswada kinasema, isipokuwa Makamu wa Kwanza wa Rais na Makamu wa Pili wa Rais, wajumbe wengine na Katibu wa Tume kabla ya kuanza kazi zao, basi watalazimika kula kiapo cha utiifu mbele ya Rais kama ilivyoelezwa katika jadweli hii ya sheria.

Kifungu cha 8(a) kutoa ushauri wa kisera kwa Rais na kwa serikali kwa jumla katika maeneo yote ya kitaifa kwa jumla. Sasa swali langu liko hapa. Ikiwa hii Tume kazi yake kuu ni kutoa ushauri kwa Rais na kwa Serikali kwa jumla ambapo hii ndio Baraza la Mapinduzi, vipi tena Rais anakuwa sehemu, ukitizama kama alivyosema Mhe. Waziri, kwamba kwa sababu Mawaziri wanawajibika kwa Rais. Sasa hapa Makamu wa Rais yeyote yule atakayeteuliwa alikuwa awe ndiye *Chairman,* kwa sababu bado yeye anajukumu la kuwajibika kwa Mhe. Rais. Lakini ikiwa Rais mwenyewe ndio *Chairman,* sasa hiki chombo kitawajibika kwa nani katika Serikali, basi itakuwa ndio ile ile serikali inapanga wenyewe na inatekeleza wenyewe, lakini itakuwa chombo hapana.

Kwa hivyo, kama kunatakiwa kuwe na chombo hasa, mimi nasema mfumo wa kumfanya Mhe. Rais kuwa Mwenyekiti, sikubaliani nao na sikubaliani nao *logical*. Haiwezekani Rais yule yule anayemteua Katibu na wajumbe wengine halafu yeye akawe *Chairman* wa chombo kile tena chombo cha kushauri kuhusu mambo ya kiuchumi na mambo mengine ya kuendesha nchi.

Kwa hivyo, Mhe. Spika, mimi naona tunge-*review* zaidi kuhusu Mhe. Rais kuwa ni mjumbe wa tume hii ya mipango, bila ya hivyo tutakuja kujitanza sisi wenyewe. Kwa sababu Rais mwenyewe hawezi kupewa ushauri na chombo hakiwezi kufanya kazi kwa sababu hiki chombo cha Baraza la Mapinduzi ni *Policy makers* wa Serikali. Hawa ni watu ambao wangekuwa zaidi ni wataalumu ambao wangeichukua nchi katika hali ya kiuchumi, lakini kwa kumuweka Mhe. Rais akawa ni sehemu ya Tume, mimi naona kumekosewa kidogo.

Kwa hivyo, Mhe. Spika, mimi ningeunga mkono hoja kwa sababu ni chombo muhimu na ni chombo cha kitaifa, lakini sikubaliani na hoja kwamba Mhe. Rais awe ndio Mwenyekiti wa Tume hii ya Mipango, ahsante sana Mhe. Spika.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kunipatia fursa ya kutoa mchango wangu japo mfupi katika hoja iliopo mbele yetu. Mhe. Spika, kabla sijenda kwenye hoja kwanza nikushukuru wewe kwa kunipatia fursa na mimi kutoa mchango wangu.

Pili, kwa niaba yangu na kwa niaba ya wapiga kura wa Jimbo la Wawi, napenda nitoe pole kwa wananchi wa Jimbo la Bububu kutokana na kifo cha Mwakilishi wao Mhe. Mtondoo, Inshaallah Mwenyezi Mungu amlaze mahala pema Peponi, amin.

Mhe. Spika, vile vile niitumie fursa hii fupi kumpongeza Mhe. Raza kuweza kuchaguliwa kwa kura nyingi katika jimbo la Uzini. Naamini wanachi wa Uzini hawakukosea kwa kumchagua Mhe. Raza. Ninachokitarajia sasa kwa Mhe. Raza ni mkereketwa katika mambo ya maendeleo. Kwa hivyo, wananchi wa Jimbo la Uzini watarajie sana maendeleo.

Mhe. Spika, sasa niende katika hoja ambayo iko mbele yetu inayosema kwamba Mswada wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Tume ya Mipango Nam. 5 ya mwaka 1989 na Kutunga Sheria Mpya kwa ajili ya Uwezeshaji wa Tume ya Mipango ya Zanzibar, Kazi zake, Uwezo wake pamoja na mambo mengine yanayohusiana na hayo. Mhe. Spika, kama kuna pahala au kuna jambo muhimu ambalo linataka kufanywa na serikali hii ambayo iko madarakani, basi jambo zuri ni hili. Kwa mfano, kama kuna pahala sheria inahitajika hivi sasa kwa kiasi kikubwa basi ni sheria hii ya Tume ya Mipango.

Kwa kweli hivi sasa Wazanzibari tunao wataalamu wengi sana tena wenye mipango mikubwa mno na wenye taaluma za kutosha kwa ajili ya kutayarisha mipango, lakini tunakwama sana katika utekelezaji wa mipango hii. Kwa hivyo, naamini kuwepo kwa sheria hiyo na kuundwa kwa tume hiyo, basi naamini ile mipango ambayo imetayarishwa na wataalamu ambayo mpaka hivi sasa imeganda, basi itaweza kutafsiriwa kwa vitendo kwa ajili ya kupatikana kwa maendeleo katika nchi hii. *(Makofi)*

Mhe. Spika, napata tatizo moja katika uundwaji wa hii Tume Mhe. Waziri wakati alipokuwa akiwasilisha hii hoja nilikuwa nikimfuatilia kwa makini katika majukumu ya hii Tume, alisema kwamba Tume hii itakuwa ni *think tank* ya serikali.

Kwa hivyo, nilitegemea kuwa itakuwa ni *Technical Commission* katika muundo wake, lakini katika muundo mzima niliuona wa Tume hii kama alivyosema mwenzangu Mhe. Rashid Seif Suleiman ni Tume ya siasa zaidi kuliko ya kitaalamu. Kwa kweli mipango inahitaji zaidi taaluma. Vile vile niungane na mwenzangu kwamba hapa wataalamu niliowaona ambao Mhe. Rais atatuwekea tukiangalia kwenye Sehemu ya Pili kuhusu Muundo wa Tume, Mhe. Spika naomba kunukuu kifungu cha 4(1).

Kifungu cha 4(1) kuhusu Muundo wa Tume kinaeleza hivi:-

4. (1) Tumeitakuwa na:-

(a) Rais ambaye atakuwa Mwenyekiti;
(b) Makamu wa Kwanza wa Rais;
(c) Makamu wa Pili wa Rais
(d) Waziri anayehusika na Masuala ya Fedha na Mipango ya Maendeleo na;

(e) Wajumbe wengine wa Baraza la Mapinduzi ambao watakaoteuliwa kwa umoja wao kama wajumbe wa Kamati ya Baraza la Mapinduzi au kwa nafasi yao kila mmoja na Mhe. Rais atakavyoona inafaa.

Kwa kweli Mhe. Spika, hawa wote ni wanasiasa isipokuwa Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo ambaye huyu hivi sasa ndiye mtaalamu na wala sisemi kama aondoshwe atafutwe mtu au waziri mwengine.

Mhe. Spika, labda kifungu cha 4 (ii) katika muundo Mhe. Rais anaweza kuteua wajumbe wengine wasiozidi watatu. Kwa hivyo, ukiacha huyu Mhe. Waziri wa Fedha ambaye hivi sasa ni mwanataaluma na hawa watatu atakaowateua Mhe. Rais, basi waliobakia wote ni Wajumbe wa Baraza la Mapinduzi ni wanasiasa au watu wa *profession* nyengine. Kwa maana hiyo, tume hii kwa mujibu wa muundo huu utakuta ina wataalamu wanne tu.

Kutokana na hali hiyo, nadhani ni vyema wangetajwa hasa kwamba Mwenyekiti Tume atakuwa ni mtu ambaye amebobea katika masuala ya uchumi na asiwe chini ya *degree* ya pili ya uchumi, lakini leo tunamuweka Mhe. Rais wetu ambaye anayo majukumu mengi. (*Makofi*)

Mhe. Spika, tumeshapanga mipango mingi sana ambayo haikufanikiwa, yaani wamepanga wataalamu wetu, lakini hakuna chombo kinachohusika na *translation* ya *theories into practical*. Kwa mfano, kuna MKUZA I baada ya mapitio imegundulikana kwamba kuna mapungufu mengi, pia kuna MKUZA II ambao ndio tunaanza sasa, lakini nao ndio unasuasua pamoja na Bango Kitita ambao tumeelezwa juzi katika mafunzo yetu kuhusu Bango Kitita, basi naamini nao unahitaji upate wataalamu ambao watautoa katika nadharia na kuupeleka kwenye matendo.

Sasa unapoweka muundo huu wa Tume, basi tusitarajie kwamba mipango yetu itakuwa makini katika nchi hii. Kwa hivyo, napendekeza kuwa hawa wanasiasa ni vyema wakapunguzwa, kwa sababu Mhe. Rais wetu anazo kazi nyingi pamoja na Makamu wetu wa Rais pia wanazo kazi nyingi na badala yake hii iwe ni *Technical Commission*, ambayo kweli itakuwa *think tank* na wala sio kama tumeweka jopo la wanasiasa pale na ikawa tena tunazungumzia mambo ya siasa tu badala ya uchumi.

Mhe. Spika, nimelazimika kusema hili kwa sababu mipango ipo lakini haifanikiwi. Kwa hivyo, tunategemea kwamba Tume hii itaweza kutusaidia kuiondosha mipango hiyo kwenda kwenye matendo.

Kwa mfano, hivi sasa wakati tunazungumza Mhe. Spika, kuna mpango wa Mapinduzi ya Kilimo, ambapo juzi Mhe. Waziri alikuja na maneno mazuri hapa kuhusu masuala ya Mapinduzi ya Kilimo, matrekta tumeshapeleka pamoja na mbegu ya *NERICA*.

Lakini ukienda huko vijijini hivi sasa Mhe. Spika, basi yale maneno yaliyosemwa hapa hayakutafsiriwa kwa matendo, kwa kweli matrekta mpaka hivi sasa katika vijiji kadhaa hakuna kilicholimiwa. Vile vile tukiangalia katika suala la mbegu ya *NERICA* yenyewe haipatikani na mvua zinakuja hizi, na hili ni tatizo.

Mhe. Spika, mpaka kule Jimboni kwangu Wawi watu wanasubiri matrekta, niliwaambia kwamba kwa mujibu wa Mhe. Waziri wetu alivyotuwekea mipango ya kilimo, basi tutarajie mafanikio makubwa kama vile magari yatakuja.

Kwa kweli mpaka hivi sasa tunazungumza Mhe. Spika hakuna gari iliyopita katika Jimbo la Wawi na matokeo yake wakulima wanahangaika, pia mbegu ya *NERICA* bado haijapatikana. Sasa itakaponyesha mvua matrekta hayaingii tena na mipango haitofanikiwa.

Kwa hivyo, naomba kutoa mapendekezo katika kifungu hiki, kwamba Mwenyekiti wa Kamati asiwe Mhe. Rais wetu na wala Makamu wetu wasipewe kazi hii, badala yake watafutwe wataalamu waliobobea na ikiwezekana Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo awe ndiye Mwenyekiti. Lakini huyo waziri ambaye yupo anafaa na wala asije akatafutwa Mhe. Waziri mwengine ambaye hana taaluma au pengine mimi mwalimu nikaambiwa niwe Mwenyekiti si sawa.

Kwa maana hiyo, atakayewekwa pale lazima awe "*identified"* kwamba Mwenyekiti awe na sifa hizi na jopo hili liwe na watu wa uchumi pamoja na watu wa mipango. Lakini kuwaweka wanasiasa Baraza la Mapinduzi, kwa mfano mimi nimo ukanipeleka pale nadhani sitaisaidia nchi katika mipango, isipokuwa nitaisaidia zaidi katika masuala ya kufundisha Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali tena katika Skuli za Sekondari sio Vyuo Vikuu.
Mhe. Spika, sheria hii ni nzuri isipokuwa Wajumbe wa hii Kamisheni waangaliwe. Mhe. Spika, nimalizie kwa kuunga mkono hoja, lakini suala la mabadiliko yafanywe katika muundo wa tume yenyewe. Ahsante sana Mhe. Spika. *(Makofi)*

Mhe. Ali Abdalla Ali: Mhe. Spika, ahsante sana na mimi kwa kunipa fursa ya kutoa mchango wangu katika Mswada huu wa Sheria ya Tume ya Mipango.

Kwanza niipongeze Serikali kupitia Wizara hii kwa kuleta mswada huu kwa wakati muafaka, kwa sababu tunafuta Sheria Namba 5 ya mwaka 1989 na kuleta sheria mpya ambayo inakwenda na wakati. *(Makofi)*

Mhe. Spika, mimi mwenyewe binafsi pamoja na wananchi wa Jimbo la Mfenesini tunaunga mkono mswada huu. *(Makofi)*

Katika mswada huu naomba nichangie kama mambo matano, lakini mchango wangu sana utakuwa kwa maswali.

Kwanza katika ufafanuzi, wakati alipokuwa akiwasilisha Mhe. Waziri mswada wake alisema kwamba nia ya kumuweka Mwenyekiti kuwa Mhe. Rais nchi nyingi zinafanya hivyo na sisi tumeona iko haja tumtumie Mhe. Rais wetu katika mswada huu, ili awe kiongozi katika hiyo Tume ya Mipango na wala sikatai.

Lakini kwa tafsiri iliyopo hapa inakuwa kidogo haikukamilika kwa hivyo naomba niisome na halafu nitoe mawazo yangu.

Kifungu cha 2 kuhusu Ufafanuzi kinachosema Mwenyekiti naomba kunukuu Mhe. Spika.

Kifungu cha 2 Ufafanuzi kinaeleza hivi:-

> "Mwenyekiti, maana yake ni Mwenyekiti wa Tume inamjumuisha mtu yeyote ambaye wakati huu atakuwa amepewa mamlaka ya kufanya kazi ya Mwenyekiti".

Mhe. Spika, nadhani ngazi ya Rais kuwa Mwenyekiti halafu pakatajwa mtu yeyote naona hii ni tafsiri nzuri nikiendelea kwenye Muundo wa Tume Mhe. Spika, naomba kunukuu.

Kifungu cha 4(1) kuhusu Muundo wa Tume kinaeleza hivi:-

4.(1) Tume itakuwa na:-
- (a) Rais ambaye atakuwa Mwenyekiti;
- (b) Makamu wa Kwanza wa Rais;
- (c) Makamu wa Pili wa Rais

Mhe. Spika, wazo langu sasa kwa kuwa tume hii yote ina wakubwa, basi tusiseme mtu yeyote isipokuwa tuseme kama maana ya Mwenyekiti baada ya Rais tuseme afuatie Makamu wa Kwanza wa Rais na Makamu wa Pili wa Rais na tafsiri imalize, kwa sababu tukisema mtu yeyote inawezekana nikaekwa mimi au mtu mwengine wa kawaida. Sasa itakuwa ile hadhi pamoja na lile lengo litaondoka. Kwa hivyo, naomba wataalamu waiangalie tafsiri yangu na halafu waangalie mswada ulivyo na kama itawezekana basi ningeshauri iwe hivyo badala ya kutaja mtu yeyote.

Wazo langu la pili lipo kwenye ukurasa wa nne kuhusu maadili kwa wajumbe na hapa pia naomba nitoe mawazo yangu kama yatakuwa yanafaa basi yazingatiwe. Naomba ninukuu Mhe. Spika halafu niseme yale niliyoyakusudia.

Kifungu cha 5 Maadili kwa Wajumbe kinaeleza hivi:-

> "Wajumbe wa Tume wasiokuwa katika utumishi wa umma au utumishi wa kisiasa watafuata taratibu za maadili kwa kutunza siri za taarifa zilizopatikana katika utendaji wa kazi zao …"

Mhe. Spika, nadhani hapa nikitafsiri mimi ni kwamba tume ina wajumbe wengi lakini hapa wametajwa sehemu mbili ambao hawakuhusika na Siasa ama Utumishi wa Umma. Kutokana na hali hiyo, kuna ubaguzi inaonesha hawa wengine hawatoi siri.

Kwa hivyo, naomba niweke vizuri kama itakubalika wanasheria wanifuate kama ninavyoelekeza. Kwa mfano, natoa maneno yanayosema wasiokuwa katika Utumishi wa Umma na Utumishi wa Kisiasa. Sasa naisema sentensi ninavyopendekeza iwe "Wajumbe wote watafuata utaratibu wa maadili ya kutunza siri katika utendaji wao wa kazi zao kwa wajumbe wote". Nadhani hii itabagua kwamba huyu aweke siri na yule asiweke.

Hivyo, napendekeza hilo kama litakuwa na msingi basi ingeondoshwa hii kutajwa wasiokuwa watumishi wa umma ama wanasiasa, isipokuwa iachwe Wajumbe wote watunze siri katika

utendaji wao wa kazi. Mhe. Spika, nadhani kama na hiyo itakubalika nafikiri nitakuwa nimetia mchango mzuri katika mswada.

Nikiendelea kwenye ukurasa wa 7 kifungu cha 12 kuhusu Utaratibu wa Mipango ya Maendeleo ya Kisekta. Mhe. Spika, hapa nilivyofahamu mimi ni kwamba bajeti siku zote tunazokwenda nazo hivi sasa huwa zinapangwa na wataalamu na halafu tunaletewa sisi hapa na baadaye tunatoa maoni kwa niaba ya wananchi. Sasa naomba niisome hii Mhe. Spika, halafu niulize swali langu kama ndilo hilo, Mhe. Waziri wakati atakapofanya majumuisho atanijuilisha.

Kifungu cha 12 kuhusu Kuratibu Mipango ya Maendeleo ya Kisekta kinaeleza hivi:-

> "Katika kutekeleza uwezo iliopewa chini ya kifungu cha 9 cha Sheria hii, Tume itaratibu mipango ya maendeleo ya kisekta kwa:-
>
> (a) Kuitisha vikao kabla ya bajeti kwa watu wa kawaida, wataalamu na wanasiasa kwa madhumuni ya kupata mawazo na kuzingatia katika mwaka ujao wa fedha".

Mhe. Spika, nadhani hapa nilivyofahamu kwamba hii bajeti itaanza kwa watu wa chini na iende juu. Sasa kama wazo langu hilo ni sawa, basi sina tatizo, lakini kama si hivyo basi naomba nipate maelezo ya ziada, ili niweze kufahamu kifungu hiki kimekusudiwa nini.

Mhe. Spika, nikiendelea na mchango wangu niende kwenye ukurasa wa 9 kifungu cha 16 kuhusu Usimamizi wa Takwimu na pia naomba ninukuu Mhe. Spika na halafu nitoe mawazo yangu.

Kifungu cha 16 Usimamizi wa Takwimu kinaeleza hivi:-

> "Tume kwa kushirikiana na Afisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali:-
>
> (a) Itaandaa Mpango wa Usimamizi wa Takwimu kulingana na shughuli za kiuchumi kwa Taasisi zote za Serikali na Jumuia Zisizokuwa za Serikali au Sekta Binafsi".

Mhe. Spika, nadhani Afisi hii imeanzishwa kipindi kirefu na takwimu hizi zinafanya kazi muda mrefu. Lakini nashukuru kwamba safari hii imetiwa katika sheria hii kwa ajili ya kuongeza mkazo.

Kwa hivyo, nataka kujua Mhe. Waziri wakati atakapofanya majumuisho ni kwamba hizi takwimu katika Jumuia zisizokuwa za Serikali zitashirikishwa vipi au zitawafikia vipi.
Kwa maana hiyo, kutakuwa na utaratibu ambao unapangwa au mtu mwenyewe wa taasisi ambayo si ya serikali atakwenda kwa Mtakwimu Mkuu wa Serikali kwa ajili ya kuzitumia, kwa sababu hizi takwimu zipo muda mrefu lakini sio watu wengi wanaoelimika katika kuzitumia. Kwa mfano, si Wizara ya Kilimo wala taasisi au *NGO's*.

Kwa hiyo, naomba nipatiwe maelezo juu ya suala hili itafanya vipi serikali, ili kitengo hicho kiweze kutumika na kazi hii inayofanywa na Mtakwimu Mkuu wa Serikali iweze kuleta tija katika serikali yetu.

Mhe. Spika, nikiendelea na mchango wangu kwenye ukurasa wa 10 kifungu cha 19 (2) kuhusu Uteuzi wa Wakuu wa Idara, Mhe. Spika naomba ninukuu na halafu baadaye nitoe maelezo.

Kifungu cha 19 (2) Uteuzi wa Wakuu wa Idara kinaeleza hivi:-

> "Tume muda hadi muda inaweza kupendekeza kwa mamlaka husika kwa Utumishi wa Umma kuhusu masharti ya utumishi, ikijumuisha utaratibu wa motisha, utaratibu wa kuwabakisha wafanyakazi na utaratibu muafaka wa utumishi wa Katibu Mtendaji, Wakuu wa Idara na wafanyakazi wa Tume".

Mhe. Spika, naomba kupata maelezo zaidi kuhusu hii *motisha* imekusudiwa kitu gani na wafanyakazi kubakishwa imekusudiwa vipi, kwa sababu kama taasisi ina wafanyakazi ambao wanafanyakazi kwa misingi ya mikataba waliyowekewa. Sasa ukisema wafanyakazi kuwabakisha umekusudia nini, nataka nifahamu ama *motisha* umekusudia kitu gani, kumpa mtu gari, baskeli, vespa, fedha kwa hiyo nimeomba hapa ili niweze kufahamu zaidi.

Mhe. Spika, sasa niende kwenye mchango wangu wa mwisho kwenye ukurasa wa 12 kifungu cha 24 kuhusu Vikao vya Tume (3) naomba kunukuu Mhe. Spika na halafu niweze kuuliza.

Kifungu cha 24 Vikao vya Tume kinaeleza hivi:-

(3) "Vikao vyote vya Tume vinavyoongozwa na Mwenyekiti

au

ikiwa hayupo vitaongozwa na Mjumbe Mwandamizi wa Tume…"

Mhe. Spika, nilitaka nifahamu kuhusu Mjumbe Mwandamizi kakusudiwa nani?
Vile vile kifungu cha 24(4) naomba kunukuu Mhe. Spika, kinaeleza hivi:-

(4) "Iwapo kwa maoni ya Mwenyekiti au Mjumbe yeyote wa Tume, suala lolote litakuwa lina umuhimu usio wa kawaida usioweza kungoja kuitishwa mkutano utakaotimiza akidi, suala hilo litaamuliwa na Mwenyekiti na angalau nusu ya wajumbe na uamuzi huo utakuwa ni halali na wenye nguvu na uamuzi huo utatolewa taarifa katika mikutano ya kawaida ya mwaka ya Tume".

Mhe. Spika, ninavyofahamu ni kwamba kikao ndicho chenye maamuzi na hapa tunaambiwa akidi haikutimia, lakini Mwenyekiti atatafuta nusu ya akidi kwa ajili ya kutoa maamuzi. Kwa kweli hapa nataka nipate maelezo nje au kwenye kikao ama sehemu gani ama imeandikika vibaya, hivyo naomba na hili litizamwe ili tuweze kuweka mswada wetu katika mtiririko mzuri.

Mhe. Spika, michango yangu hiyo michache niliona nisikae kimya na mimi nitie baraka kwenye mswada huu. Kwa hivyo, kwa kumalizia nikushukuru kwa kunipa nafasi, naomba pia nitamke kwamba mimi mwenyewe binafsi na kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Mfenesini tunaunga mkono mswada huu. Ahsante sana Mhe. Spika. *(Makofi)*

Mhe. Asaa Othman Hamad: Mhe. Spika, nakushukuru sana baada ya kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia uhai na uzima na hatimaye tumefika leo hapa kwa ajili ya kuendelea na shughuli tuliyokabidhiwa na wananchi wa Zanzibar.

Mhe. Spika, naomba nitangulie kusema kwamba chombo hiki ni muhimu sana kwa maana ya kina kabisa kwa uhalisia wa uchumi na maendeleo ya nchi yetu.

Nadhani ingefaa wataalamu wetu chini ya Uongozi wa Mhe. Waziri wa wizara husika swahibu yangu mpenzi kwa mchango wa Baraza hili Tukufu Waheshimiwa Wajumbe, basi ingefaa kwanza wapate semina kuhusiana na mswada huu, ili nao watie baraka zao kabla haujafika hapa. *(Makofi)*

Mhe. Spika, mswada huu ni muhimu sana, lakini tunaukuta kwamba kuna mambo ambayo tungekuwa na fursa nzuri ya kuyajadili huko kabla haujafikishwa hapa. Kutokana na hali hiyo, Waheshimiwa Wajumbe wako tunapata wasi wasi pengine kwa sababu tu fani iliomo humu ni ya kitaalamu sana, na wajumbe wako ni wanasiasa ndipo pale niliposema kwamba kwanza tupate semina kwa ajili ya kusaidia, lakini na sisi pia tusaidiwe kwa taaluma. *(Makofi)*
Baada ya kusema hayo Mhe. Spika, Zanzibar ni miongoni mwa nchi ambazo sasa zimekabiliwa na wimbi zito la uchumi, kwa kweli tunahitaji wataalamu kufanya kazi ya ziada na wananchi waelimishwe tena waelewe ni mchango gani unahitajika kwa taifa lao.

Mhe. Spika, sisi kama Wajumbe wa Baraza hili ambao tunawakilisha wananchi, mswada huu si kwamba tunayo mashaka, lakini tunaona kuwa Mhe. Rais wetu tukianza kwenye muundo, ni Rais ambaye amebahatika kuwa ni Mzanzibari wa mwanzo kuiendesha Serikali yenye Mfumo wa Umoja wa Kitaifa. Kwa kweli wazanzibari walichagua mfumo huo kwa nia safi tena kwa mategemeo makubwa.

Kwa hivyo, sasa tungependa tumuachie kazi hii ya kuonesha ni namna gani angeweza kuwaweka wazanzibari mahala stahiki katika suala zima la uchumi na maendeleo yao ya kijamii. *(Makofi)*

Kwa kweli naungana na wenzangu waliosema kwamba Mhe. Rais tunamtwisha mambo haya, tume hii miongoni mwa kazi zake hatimae hasa zile za kisera zinataka zifike kwa Mhe. Rais, lakini Mhe. Rais ni Mwenyekiti wa tume hiyo.

Mhe. Spika, nafahamu na nimemsikia Mhe. Waziri kwamba ni mtindo wa nchi nyengine, lakini pengine nchi nyengine wanafanya hivyo kutokana na hali zao za kiuchumi pamoja na maendeleo ambayo tayari wameshayafikia. Sasa sisi Mhe. Rais wetu shughuli zake kwa hali tuliyonayo anakuwa ni mtu wa mwisho na hii tume tulitaraji ifike mahali impelekee Rais yale ambayo wataona yanahitaji ushauri wake.

Katika hali ya kawaida Mhe. Spika, anapokuwepo mtu mzima kwenye mjadala fulani, basi vijana wanakuwa na ukomo wao wa mazungumzo na huu ndio utamaduni wetu waafrika.

Sasa kuwemo kwake Rais ndani ya chombo hiki, mijadala ya kitaalamu itakapoendeshwa kuna ile hali ya kuona aah! Ni wale au ile *cream* ya serikali kuanzia Rais mwenyewe Makamu wa Kwanza na Makamu wa Pili, yaani wote wamo mule. Mhe. Spika, hata ningekuwa mimi pamoja na umahiri basi kuna maeneo ningeshindwa kuyaingia kibinadamu tu.

Kwa hivyo, nadhani swahibu yangu pamoja na timu aliyonayo, kwamba naiamini sana ni vyema kwenda kulitizama tena eneo hili kwanza la muundo, ili tumuache Mhe. Rais na hata ikibidi pengine katika wawili waliobakia, basi wakachukua mmoja na tukaiacha tume ifike mahala ipeleke huko juu pale watakapoona wametanzwa.

Mhe. Spika, kwa mawazo yangu nadhani tungempa faraja sana Mhe. Rais na ile dhana tuliyokusudia kwamba yeye ndiye *top leader* wa nchi hii pamoja na serikali yake.

Kwa kweli tume hii inahitaji wataalamu waliobobea kwenye nyanja za kutafiti, kwa maana ya tafiti za kiuchumi na maendeleo ya jamii yetu.

Mhe. Spika, wakati nilipokuwa nikiupitia mswada huu nimeona Mhe. Rais anayo nafasi ya kuteua wajumbe watatu na waliobaki ni wale waliomzunguka yeye Rais wakiwemo Wajumbe wa Baraza la Mapinduzi na wengine wanaofanana na hao.

Mhe. Spika, hawa wala sitaki niseme wasiwemo, lakini mimi ninapendelea kwamba idadi kubwa iwe ni wataalamu na wachache mno wawe ni wanasiasa, kwa sababu hawa *decision makers* Mhe. Spika kama nilivyotangulia kusema kuwa, wataalamu wanafika mahala wanaona tabu kuzungumza mengine mbele ya viongozi wakubwa wa namna hii.

Kwa hivyo, ni vyema tungewapa fursa wataalamu wetu wakaenda huko na kutafiti, Mhe. Spika kwenye tafiti inafika mahala kunakuwa na ubishi, lakini ni ubishi wa kimaendeleo, yaani watafika mahala wakubaliane au pale wanaposhindwa kufikia makubaliano ndipo hapo tutakwenda huko juu kwenye viongozi wakubwa. Sasa viongozi wakiwepo pale, basi kuwepo kwao pale hawa watapata tabu katika shughuli zao hizi.

Mhe. Spika, suala jengine kuhusu kifungu cha 8(1) (a) naomba kunukuu.

Kifungu cha 8(1) (a) kinaeleza hivi:-

> "Kutoa ushauri wa kisera kwa Rais na serikali katika maeneo yote ya maendeleo ya kitaifa kwa jumla".

Mhe. Spika, watatoa saa ngapi na yote yatakayokuwa yanazungumzwa na kujadiliwa yeye yupo. Sasa kama wenzangu wengine walivyoona kwamba haya mambo kidogo yanagongana hapa, pengine tuseme hivyo tulivyotangulia kwamba Mhe. Waziri angetupa ile semina, haya tusingesema ni mafupi kwa wenzetu waliyoyapanga, lakini sisi kwa muono huu tu inatuchanganya.

Nimesema kwamba tume itakuwa na kazi kubwa ya tafiti, serikali sasa hivi pia inawashauri mabalozi wetu walioko nchi za nje sio tu kwamba watuwakilishe, lakini pia wawe ni mabalozi na watafiti wa maendeleo kwa nchi yetu, wafanye kazi hiyo kwa maslahi yetu na nchi yetu.

Sasa tafiti hizi zitakapoletwa na watu watatu walio wataalamu, waliomo wote ni wanasiasa, wasi wasi ni kwamba mambo haya yatakuja kwenda kisiasa zaidi kuliko kule tulikofikiria tufike, na tunakotaka tufike ni kule kwenye maendeleo yetu na ya nchi yetu kwa faida yetu na wazanzibari wote kwa ujumla wake.

Mhe. Spika, mchango wangu sio mrefu, ilikuwa ni wasi wasi nilioupata tu hasa hasa kwa ushiriki au kwa idadi ndogo sana ya wataalamu waliomo, ombi langu mimi naomba kwamba idadi kubwa iwe ni wataalamu, na wachache wawe ni wanasiasa. Lakini pia na mimi nakubaliana na wengine waliosema kwamba Mhe. Rais kumuweka mwenyekiti hapa nadhani haitokuwa sahihi sana, kwamba wenzetu wanafanya na sisi tufanye, lakini nadhani tutizame wenzetu wakoje na sisi tuko vipi, tunataka kwenda kwa Mhe. Rais pale atukwamue kwa pale tulipokwama, tusimkwamishe sisi mwanzo halafu tukamzunguka tukataka afanye kazi hii itakuwa sijui tuiite vipi.

Tume itakuwa ni chombo cha kitaalamu katika mipango ya kitaifa ya maendeleo ya kiuchumi, lakini pia chombo cha juu kabisa cha kupanga na kusimamia utekelezaji wa mipango hiyo. Mhe. Spika, madhumuni na sababu, yako hivyo nilivyoyanukuu,lakini maudhui mengine huku yaliyotangulia naomba sana Mhe. Waziri anayehusika akae tena na wenzake, timu nzuri ina uwezo mkubwa, tuna mengi,vyanzo vipo,wakavitafute huko ni namna gani tu vitaweza kuleta maslahi kwa nchi hii, haya mengine tunayoyachangia wakiona yatafaa wayachukue hatimae tufikie pale tunapopahitaji kwa maendeleo yetu na uchumi imara wa nchi yetu.

Mhe. Spika, baada ya kusema hayo ni imani yangu serikali ni sikivu, Mhe. Waziri ni mahiri na timu yake ipo hapo juu inatusikia humu mwenye wasi wasi wetu, wanaweza kutufanyia jambo tukaona kwamba na sisi tumejiridhisha kwa kuiona sura ya maandiko haya yamebadilika na maana halisi iliyokusudiwa ikaweza kufikiwa.

Mhe. Spika, baada ya kusema hayo nasema ahsante sana. *(Makofi)*

Mhe. Suleiman Hemed Khamis: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako na mimi napenda nichangie kidogo katika mswada huu, mswada ambao ni muhimu na ambao una malengo makubwa ya kitaifa, tunahitaji na sisi kutoa maoni yetu kidogo. Lakini kabla ya hapo mimi nilitegemea kwamba mswada huu usiwe ule wa mwanzo, ingelikuwa ni vyema kama mswada huu ungekuwa baada ya kamati kutoa maelekezo yao, baada ya maelekezo yale na sisi tukafuatilia kama kuna kitu cha kuongeza au kupunguza katika yale. Lakini kwa sababu tunauzungumza huu *original* hatujui kwa nini ukaja huu *original,* tusipate ule ambao kamati imepitia na kutoa marekebisho halafu sisi ndio tukaingia kwenye marekebisho ambayo yangekuwa ni bora zaidi.
Lakini hata hivyo, kutokana na mswada huu na maelezo ya Waziri, mimi umenifanya kutoa mchango wangu, kwa sababu katika maelezo yake makubwa aliyosema, kwamba hichi chombo ni muhimu sana na kusema kweli ni chombo ambacho kinatakiwa kijitegemee kwa mambo yote,

akasema kwamba chombo hiki mfano wake ni kama kisima cha mipango, ina maana taratibu zote na maelekezo yote yanahitaji chombo hiki kiwe na msimamo mzuri sana.

Chombo hiki kinatakiwa kiimarishe uchumi wa nchi hii, sasa katika mipango yake yote hiki ni chombo cha juu kabisa na kinatakiwa kuwa imara, sasa ukiangalia hoja hizi za msingi na mtandiko mzima katika gazeti rasmi la serikali mimi nilihisi kwamba hili jukumu la kumpa Rais kwamba yeye awe ndie mwenyekiti wa shughuli hizi naona tunampa kazi kubwa sana na hatukupata maelekezo kwa nini awe Rais, maana ingelikuwa tumepata ufafanuzi tukajua angalau Rais hapa kachaguliwa kwa sababu ya kitu kadhaa, lakini hatuna maelekezo, sasa kwa kuona tu kwa mtazamo wa mara moja tunaona kwamba haikuwa jambo la busara.

Kwa sababu hiyo ukitizama taarifa zilizopo ni kwamba Tume itakuwa ni chombo cha kitaalamu, katika chombo hiki nimeona zaidi wanaotakiwa ni wataalamu, hao wataalamu ndio watakaoendesha tume hii na wanajua taratibu zote za kuweka uchumi wetu sawa sawa. Kwa hivyo itachambua mwelekeo muhimu wa kiuchumi,hao ndio wataalamu tunaowategemea hapa Zanzibar katika kuliweka suala zima la Uchumi, halafu uchumi wenyewe wa Zanzibar,uchumi wa kikanda na wa dunia.

Kwa jumla kuendeleza mfumo wa utekelezaji wa uingiliaji kimkakati ambao utaipa Zanzibar faida ya pekee na kuweza kulinganishwa na eneo lolote kati yafuatayo. Sasa tuanze kutizama haya majukumu ambayo tayari yameshatiwa ambayo haya yatamlazimu huyu Mwenyekiti ambae ndie dhamana wa Tume hii , sasa ukiangalia kuvutia mtaji unahitajika mtaji hapa, na unajulikana mtaji wapi unapatikana, wawekezaji katika maeneo muhimu, uzalishaji, ushindani katika sekta zote ambazo Zanzibar inaweza kulingana kifaida na kisoko halikadhalika.

Sasa haya yote mimi nikiangalia naona ni majukumu makubwa sana ambayo hatuwezi kufanya tukawaachia marais yote haya, kwa mujibu wa hapa inavyoonyesha kwamba, Rais ndio atakuwa mwenyekiti, Makamo wa Kwanza wa Rais, na Makamo wa Pili wa Rais,ina maana Marais wote tunawashirikisha katika suala hili, halafu Rais mwenyewe ndio mwenyekiti wa shughuli hizi,hatuoni kwamba hapa tunampa mzigo mkubwa sana. Tuangalie kwamba Rais ana majukumu mengi na makubwa ya nchi hii, sasa kumuweka yeye mwenyekiti inamaana sisi tuje tushindane nae Mwenyekiti na kuanza kumzungumza ambae atakuwa ni rais, haiwezekani sisi tukae kitako hapa tumzungumze Rais. Mimi naona baada ya shughuli ya wataalamu jopo lote lililobakia Rais aje kulisimamia na kuweza kutoa maamuzi, lakini isiwe kwamba wao wawe wenyeviti na wao ndio wanaoshughulikia kwamba hii ni kazi yao tunawapa kazi marais sasa na Makamo wa pili wa Rais, huyo Rais na Makamo wa Kwanza na wa Pili wa Rais hawana kazi nyengine za kufanya. Mimi nahisi kwamba hili jopo zima tuwaachie wataalamu waliendeshe halafu hawa viongozi wa kitaifa waliobakia wao kuangalia kama mapungufu yaliyopatikana, au wao kutoa mchango wao katika hili suala zima.

Kwa kweli mswada huu kubwa mimi nimepaona hapo,kama wenzangu walioona na mimi nimeona hapo hapo, saa hatujui kamati ya mswada huu nini maoni yake kwa sababu hii hatujaipata, lakini kama tungeipata tungejua nini wamesema katika kifungu hicho, lakini kwa sababu tuna mswada *original* mimi maelekezo yangu ni kama hayo. Mimi sitaki kuingia ndani sana ya mswada huu kwa sababu mengi yameshazungumzwa na mimi kuonesha kwamba hisia zangu katika suala hili naunga mkono mswada huu kama ulivyokuwa umekusudiwa. Isipokuwa

nitakuwa na mabadiliko madogo madogo ambayo sisi tumeyasema na tunataka mabadiliko hayo yachukuliwe hatua. Ahsante sana. *(Makofi)*

Mhe. Abdalla Juma Abdalla: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili niweze kusema machache sana katika mswada huu, nataka niseme machache, kwa sababu kadiri nilivyousoma na kwa sababu si mwanasheria sikuweza kuona kasoro nyingi, ndio maana nikasema niseme machache halafu niubariki.

Mhe. Spika, kwanza mimi naipongeza sana serikali kwa kuleta mswada huu ambao ni muhimu sana kwa maendeleo ya nchi yetu, jamii nyingi na hata familia na hata mtu binafsi tunakuwa tunafeli kutokana na mipango finyu, sasa tutakapokuwa na mipango mizuri itakuwa ndio chanzo cha maendeleo. Kwa hivyo mswada huu nadhani umelenga kuleta maendeleo ya kweli kwa hivyo naipongeza sana serikali kwa kuwa na malengo ya namna hii, sasa mimi nataka nianze kwenye kifungu cha tano naomba ninukuu kidogo.

Kifungu cha tano (5) kinasema:

> (Wajumbe wa Tume wasiokuwa katika utumishi wa umma au utumishi wa kisiasa watafuata taratibu za maadili kwa kutunza siri)

Sasa nilikuwa najiuliza maana yake ukiangalia muundo, ukiacha wataalamu watatu ambao watateuliwa na Rais, lakini waliobakia wote ni watumishi ama wa kisiasa ama watumishi wa umma. Ukiangalia kifungu cha 20 kinampa uwezo katibu Mtendaji wa Tume kuajiri tena kwa masharti ya utumishi wa umma, kwa hivyo wale wanakuwa kwenye utumishi wa umma moja kwa moja, sasa ukiacha hao wengine ni watumishi wa kisiasa, sasa hawa watakuwa sio watumishi wa kisiasa wala watumishi wa umma mimi siwaoni katika hii Tume. Sasa sijui Mhe. Waziri atagundua wapi nataka aje atwambie ni wapi ambao hawamo katika utumishi wa umma wala hawamo katika utumishi wa kisiasa ambao kifungu hiki ndio kinawalenga kwa maadili.

Ukiacha hapo nataka niende kifungu cha saba (7), ni kiapo cha utiifu hiki, hiki kiapo nasema hiki kifungu kinasema isipokuwa Makamo wa Kwanza wa Rais na Makamo wa pili wa Rais wajumbe wengine na Katibu wa Tume kabla ya kuanza kazi watakula kiapo cha uaminifu.

Sasa ukiangalia *composition* ya hawa wajumbe wa hii tume takriban wote wameshakula kiapo maana yake ni wajumbe wa Baraza la Mapinduzi wameshakula kiapo wote, sasa mimi sijaona hasa mantiki ya hawa kula kiapo tena kwa sababu wengi wameshakula kiapo wote ni pamoja na Makamo wa Kwanza wa Rais na Makamo wa Pili wa Rais, kwa nini wao wasile kiapo na wengine wote wameshakula kiapo kama wao waambiwe wale kiapo tena, mimi nilikuwa nadhani kwa sababu walikula kiapo hakuna haja ya kuwaapisha tena.

Mhe. Spika, halafu niliangalia kifungu cha 8(1)a hii ni habari ya kazi za Tume, hii inasema moja katika kazi za Tume ni kutoa ushauri wa kisera kwa Rais na kwa serikali, lakini Tume na Rais yumo na serikali imo ndio yote hiyo takriban ukiacha wale wataalamu watatu, waliobakia ni Rais, Makamo wa Kwanza wa Rais, Makamo wa Pili wa Rais na wajumbe wa Baraza la Mapinduzi. Sasa kutoa ushauri wa kisera kwa Rais hii ikitaka iwe, lakini Rais awe hayumo

katika hii tume, halafu na hii serikali nayo haipo kuna jopo la tume la wataalamu watupu watoe ushauri wao kwa Rais na serikali, lakini wao wenyewe Tume ni serikali.

Mimi nafikiri hapa sio lugha nzuri kusema watoe ushauri wa kisera kwa serikali, ni wao wenyewe wakae tu kama hivi kazi zao ambazo zimeelezwa vizuri sana basi wakae tu wapange mipango na utekelezaji wa kuratibu na kusimamia lakini hili suala la kutoa ushauri kwa Rais wakati Rais mwenyewe yupo katika tume, nahisi hii lugha katika kifungu hichi haikutumika vizuri .

Mhe. Spika, nimeangalia hizi kazi za tume kwa kweli ni mambo muhimu sana, na mengi sana na mazuri sana, lakini mimi nilikuwa nataka nisisitize sana katika maeneo hasa yanayohusu mapato ya nchi, ni mambo yanayohitaji kusimamiwa kwa karibu sana, na nilikuwa naishauri sana hii Tume ikishaundwa basi itoe kipaumbele maalum katika kuratibu kwa karibu sana makusanyo, yaani vile vianzio vya mapato vile vinavyokusanya pesa. Maana yake mipango ikiwa haina matumizi Mhe. Spika, sidhani kama italeta ufanisi wowote, mtapanga wee lakini mwisho wa kupanga itabidi tuwe na fedha za kuweza kutumia.

Mhe. Spika, mimi nasikitika sana mpaka leo serikali bado imeacha mianya ya pesa za serikali kuvuja katika makusanyo, nitatoa mfano nilipokuwa nasoma ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali kuna taasisi muhimu kweli kweli za makusanyo hapa hata mahesabu yao ya mwaka hawafanyi, jambo ambalo hatujui wamekusanya kiasi gani na Hazina wamepeleka kiasi gani hatuoni.

Sasa tukifika hapo ukweli tutakuwa hatupo makini na vyanzo vyengine tumepata siri pale uwanja wa ndege,pale idadi ya watalii wanaoingia nchini sio idadi inayoripotiwa serikalini na wale wakiingia pale wanalipa sasa pale panavuja pesa nyingi kweli kweli, nilikuwa naomba sana Mhe. Waziri pamoja na hii Tume waziri kama muhusika wa mapato lakini pamoja na hii Tume itakayoundwa ifuatilie kwa karibu sana.

Mhe. Spika, nchi hii pesa zinakusanywa nyingi na zingetusaidia sana kupunguza changamoto lakini mianya ya uvujaji wa pesa ni mingi mno, nilikuwa nashauri sana Tume hii ikishaundwa kwa kweli katika jambo muhimu sana ni hili, nafikiri kama nilivyosema hamna makosa sana katika mswada huu, nilisema nitoe Baraka zangu tu na mimi naunga mkono mia juu ya mia. Ahsante sana.

Mhe. Spika: Nafikiri kama wapo wengine waendelee kujitayarisha tuendelee na hiyo kazi jioni, sasa nimuombe Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais mara baada ya kuakhirishwa kikao hiki aje atoe ile taarifa aliyoomba aitoe, mimi wakati huo kitini nitakuwa sipo lakini mtakuja kunambia wenzangu kulikuwa na nini.

Waheshimiwa Wajumbe nichukue nafasi hii kuwashukuru tena kwa kazi nzuri ambayo tunaifanya kwa ajili ya wananchi wetu na kwa mashirikiano makubwa, kuna muda mchache tu kama dakika kumi na tano, kwa hivyo shughuli zetu hizi tusitishe ili tuweze kuja jioni na kuendelea na mjadala wa mswada huu.

Lakini tubakie dakika tano mara baada ya kutoka Mhe. Waziri anataka kutoa taarifa kutoka kwa Mhe. Rais.

(Saa 6.45 Mchana Baraza liliakhirishwa
hadi Saa. 11.00 jioni)

(Saa 11:00 jioni Baraza lilirudia)

(Majadiliano Yanaendelea)

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Naibu Spika, awali ya yote naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa utukufu kwa kutujaalia neema ya uhai na uzima, tukakutana tena katika mkutano huu wa saba na jioni hii tukiwa tunaendelea na kikao chetu tukiwa tunazungumzia mjadala huu wa Mswada wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Tume ya Mipango Nam. 5 ya mwaka 1989 na kutunga sheria mpya kwa ajili ya uendeshaji wa Tume ya Mipango ya Zanzibar, kazi zake, uwezo wake na mambo mengine yanayohusiana na hayo.

Kabla ya kuingia katika eneo hilo Mhe. Naibu Spika, naomba pia niungane na wenzangu kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Mji Mkongwe ninaowawakilisha kutoa mkono wa rambi rambi kwa wananchi wa Jimbo la Bububu kwa kuondokewa na Mwakilishi wao Marehemu Mheshimiwa Salim Amour Mtondoo, tunamuombea Mwenyezi Mungu amlaze mahala pema Peponi. Amin.

Pia Mhe. Naibu Spika, nichukue nafasi hii kumpongeza Mwakilishi mpya wa Jimbo la Uzini Mhe. Mohamedraza Hasanali Mohamedali Dharamsi, ambaye asubuhi ya leo ameapishwa kuingia katika chombo hiki kitukufu kilichowekwa na wananchi wa Zanzibar kwa ajili ya kuwasimamia mambo yao na mambo yanayohusu nchi yao. Ni imani yangu kwamba sote tutampa ushirikino wetu kikamilifu na hata kama tulikwaruzana katika kampeni yalikuwa ni mambo ya kampeni, yameishia kule kule. Lakini sasa amekuwa Mwakilishi tunaheshimu maamuzi ya wananchi wa Jimbo la Uzini na tunaahidi kumpa mashirikiano kikamilifu ili kwa pamoja tuweze kutekeleza yale ambayo yametuleta katika chombo hichi.

Baada ya kusema hayo Mhe. Naibu Spika, naomba na mimi niungane na wenzangu kutoa maoni yangu kuhusiana na Mswada huu uliokuwepo mbele yetu. Kwanza kabisa Mhe. Naibu Spika, nilikua naomba niseme la jumla. Kwamba chombo hichi cha Tume ya Mipango katika nchi ambayo imekusudia kikweli kuleta mageuzi ya kiuchumi ni chombo muhimu sana.

Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Fedha, Uchumi, Mipango ya Maendeleo amelieleza vizuri sana hilo katika hotuba yake. Ni matumaini yangu Mhe. Naibu Spika, kwamba Mhe. Waziri na Serikali kwa jumla hawatoishia kukitizama chombo hiki kwa uzuri wa maneno tu katika hotuba za leo, lakini tutakitizama kwa lile lengo lake hasa lililokusudiwa.

Mhe. Naibu Spika, katika nchi za wenzetu kama ilivyoelezwa hapa, Tume za Mipango huwa ndio zenye jukumu hasa la kupanga na kuratibu shughuli zote za mipango ya maendeleo katika nchi husika. Kama alivyokuwa akisema mwenyewe ndio tanuri la fikra ambalo linaiwezesha

serikali kupanga mipango yake kitaalamu na baadaye kuiwachia Wizara zinazohusika na Idara za Serikali kutekeleza.

Ndio maana nakubaliana kabisa na waliosema kwamba chombo hiki ni chombo cha kitaalamu. Kama hivyo ndivyo basi tunapaswa tuipe umuhimu wa aina ya pekee Tume hii. Tukitambua kwamba ikipata watu wenye sifa na uwezo kwa yale ambayo yamekusudiwa kutekelezwa na Tume hii katika vifungu mbali mbali yametajwa basi inaweza kuisaidia sana nchi yetu. Lakini pia ikiwa tutaiwachia nafasi ikafanya kazi zake ilizokusudiwa na kutumika kazi zake.

Moja katika matatizo makubwa katika nchi yetu mbali ya Tume za kudumu kama hizi hata tunapo unda zile Tume za matukio maalum huwa zinafanya kazi zikigharimu fedha nyingi, zinaandika ripoti kubwa kubwa, zinajumuisha mambo mengi ya kitaalamu lakini hatimaye zinaishia katika makabati ya Afisi zetu, zinasahaulika mpaka mara nyengine zinakufa kuundwa Tume zinafanya kazi tena zile zile. Sasa sitegemei kwa Tume kama hii tena turejee makosa yale yale yaliyokuwa yamezoeleka.

Mhe. Naibu Spika, nikiacha hilo niseme mimi naona kuna tatizo moja kubwa la mipango katika nchi yetu. Hili nimuombe sana Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Fedha, Uchumi, Mipango ya Maendeleo, alitizame kwa kina kipindi hichi wakati anaandaa bajeti au mapendekezo ya bajeti ya mwaka ujao wa fedha.

Mhe. Naibu Spika, tuna tatizo mara nyingi tunasema tunaratibu mipango yetu na kwamba kile ambacho kinacholetwa hapa kina *reflect* ile mipango ya kitaifa. Lakini mimi kwa maoni yangu sioni kama tunaifanya kazi hiyo vile ambavyo inapaswa kufanywa. Kama tunapanga mipango ya kweli, lazima itizamwe kwanza ile *vision* ya nchi. Hapa kwetu tuna Dira ya 2020, pengine hiyo Dira yenyewe inapaswa kupitiwa. Nilikuwa najua, hivi karibuni ilikuwa inapitiwa baadhi yetu tulipata kualikwa kwenda kutoa maoni yetu. Tutizame vipaumbele vya dira ile vimejikita katika maeneo gani ya kiuchumi.

Kwa mfano kama katika nchi yetu tumeamua kwamba moja katika misingi ya uchumi wetu ni kuikuza sekta ya utalii kwa kiwango cha juu kabisa. Kama tunasema tunataka kuifanya Zanzibar kuwa ni kituo kikuu cha biashara ambayo imekuwa ndio nyimbo yetu miaka zaidi ya 20 sasa. Kama tunataka kuifanya Zanzibar kwamba ndio kituo kikuu cha huduma iwe za fedha au za aina nyengine katika Afrika Mashariki.
Sasa je, Mhe. Naibu Spika, kiasi gani mipango yetu mengine ikiwa ya elimu, ikiwa ya afya, ikiwa ya miundombinu na mawasiliano, kiasi gani hii nayo inajikita kutupelekea kujenga uchumi wa aina hiyo.

Mhe. Naibu Spika, hilo ni tatizo sugu katika nchi yetu tutasema tunataka kujenga uchumi ambao msingi wake ni utalii, lakini halafu hizi huduma nyengine hazifanyiwi mipango ambayo inapelekea kuukuza utalii. Tunasema kwamba tunataka kujenga uchumi ambao msingi wake ni kuifanya Zanzibar kuwa Bandari Huru na Kituo Kikuu cha Biashara katika Afrika Mshariki, lakini sekta nyengine hazijielekezi hapo. Sasa Mhe. Spika, katika hili nilikua nadhani tunapaswa tutizame wenzetu wanafanya nini.

Mhe. Naibu Spika, Malaysia ni katika nchi iliyopiga hatua kubwa sana za katika nchi za kimaendeleo kwa kutumia mfano kama huu wetu sisi wa kuwa na dira na hiyo yao pia ilikuwa inaitwa *vision 2020* lakini wenzetu walianza mapema kidogo. Wamepita hatua kubwa sana kwa sababu mipango yote imekuwa inapitiwa kwa pamoja na inaelekezwa kuelekea katika mkabala mmoja, hakuna kila mmoja akapanga lake, matokeo yake mnakuja kukuta katika bajeti mipango haiowani. Nitoe mfano mmoja nieleweke Mhe. Naibu Spika.

Kama tunasema kwamba uchumi wetu unataka kujikita katika sekta ya utalii basi inapaswa hata mitaala yetu ya elimu itoe wanafunzi au wahitimu ambao, watai- *supply* sekta ya utalii wale wataalamu na wajuzi wa fani mbali mbali ambazo zinahitajika katika sekta ya utalii. Lakini njoo ukatizame Chuo chetu kinachotoa kozi ya Utalii pale Maruhubi kiko hoi bin taaban, wala hakina sifa ya kutoa watu ambao wanaweza kui-*supply* sekta ya utalii wale watu ambao tunawahitaji na matokeo yake wakati mwengine tunapiga kelele na ukizungumza na wawekezaji wa sekta hii wanasema hatuwapati. Nyinyi mnatulaumu hatuwachukui Wazanzibar wanatwambia hatupati wahitimu ambao wamejitosheleza katika fani hizi na wamepikwa wakapikika ipasavyo.

Sasa je, kweli tunapoelekeza katika sekta nyengine tunalenga hivyo kupanga mipango yetu namna ambavyo tunataka uchumi wetu ukue. Tunasema uchumi wetu tunataka kuigeuza Zanzibar iwe Bandari huru, kuwa kituo kikuu cha biashara. Tunataka kujenga uchumi wa huduma, tumehakikisha kiasi gani mfumo wetu wa elimu unatoa wahasibu, unatoa wanasheria madhubuti, unatoa wakaguzi. Kiasi gani mambo haya yanayohusiana na huduma tunayajenga ipasavyo Mhe. Naibu Spika.

Nasema ni muhimu sana kama tunajenga utalii. Mtalii ili aje hapa anataka ajihakikishie akiugua anatibiwa vizuri. Sasa je, kiasi gani mipango yetu ya afya inajielekeza kutoa huduma bora za Afya kwamba mtalii ambaye anaweza kuja kutoa pato kubwa la nchi haogopi kwamba akija akikumbwa na maradhi mabaya itabidi akimbizwe na pengine kama hali yake imekuwa mbaya hawezi kusafirishwa anaweza akaja akafia katika nchi yetu.

Haya natoa mfano Mhe. Naibu Spika, lakini kwa jumla tunataka tufike pahala kwamba Tume ya Mipango iwe kweli tanuri la fikra kama ambavyo Mhe. Waziri amesema na kuanzia bajeti hii na bajeti zinazokuja kwamba zote zipange mipango ya uchumi wetu kulingana na zile nyaraka mbali mbali tulizonazo, kama ni vision 2020, kama ni MKUZA, zote zituelekeze pahala pamoja sio kila mtu anapangwa vyake.

Mhe. Naibu Spika, wenzetu Kenya katika hili wanatupita sana, sitoi mfano wa Tanzania Bara kwa sababu nao pengine itakuwa jora moja, mkasi mmoja, lakini natoa mfano wa Kenya. Kenya wamekumbwa na machafuko makubwa ya kisiasa baada ya uchaguzi uliopita. Lakini mara baada ya uchaguzi kwa sababu wana mipango, inaelekea wamefanya kazi kubwa kurejesha uchumi wao uliokuwa umeanguka kwa kasi na unarudi katika kiwango kilichokuwepo. Lakini juzi Mhe. Naibu Spika, wamezindua mradi mkubwa sana wa kujenga bandari kubwa sana pale Lamu. Ile bandari ukiitizama si bandari tu kuona kwamba yale mambo yao yote yaliyokuwa *synchronized* unakuta kuna Bandari ya Lamu. Mradi ule unafadhiliwa kwa pamoja na Kenya, Ethiopia na Sudani ya Kusini. Kwa sababu ukitoka bandarini unaunganishwa na reli na barabara ambazo zinazopeleka katika nchi zile kwa hivyo itakuwa bandari ile inahudumia nchi zile.

Lakini pia kunatengenezwa barabara nyengine ambayo itaiunganisha Kenya ivuke nchi za Maziwa Makuu mpaka ifike Cameron. Wanasema pia kutakuwa na daraja la nchi kavu ambalo litaiunganisha Kenya mpaka kufika Cameron mpaka kufika Atlantic. Kwa hiyo unakuta bandari ya Lamu itaiiunganisha Bahari ya Hindi mpaka Bahari ya Atlantic. Unakuta wenzetu hata ukenda katika elimu inajielekeza hapo, ukenda katika Afya inajielekeza hapo, na sisi Mheshimiwa tosome kwa wenzetu wale. Wenzetu wa Kenya katika hili wapo mbali sana, kwa sababu wana mtu nina hakika Mhe. Waziri wa Nchi anamfahamu Profesa Anyan'g Nyong'o, ni mtu ambaye amebobea katika fani hizi za *public policy.* Kwa muda mrefu alikuwa Waziri wa Mipango na Maendeleo na pia ameshiriki kikamilifu kuiandaa ile *vision 2030* ya Kenya ambayo ipo pale.

Kwa hivyo Mhe. Naibu Spika, nasema tuyatizame haya, nayasema haya kwa jumla kabisa kwa sababu katika Mswada ni muhimu kujua haya tunayoyapitisha tunadhamiria kikweli au tunaendelea kurudufisha vyombo tu lakini baadaye hatuvipi nafasi yake wala hatuteuwi watu ambao wanaweza kwenda kuzifanya zile kazi ambazo zimekusudiwa.
Mhe. Naibu Spika, sasa niende katika Mswada. Mhe. Naibu Spika, katika Mswada kwanza na mimi nilikuwa nina maoni kama wenzangu katika Kifungu cha Pili katika utangulizi, kwenye tafsiri ya neno "Mwenyekiti". Nimesema hapa "Mwenyekiti" maana yake ni Mwenyekiti wa Tume na inamjumuisha mtu yeyote ambaye kwa wakati huu atakuwa amepewa mamlaka ya kufanya kazi za Mwenyekiti. Huku mbele ukijaukisoma tafsiri ya "Rais" inasema maana yake ni "Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi"

Kifungu cha Nne cha sheria hii nikifanya rejea kinasema kwamba Tume hii itamjumuisha Rais ambaye atakuwa ni Mwenyekiti. Sasa kama Rais ndio Mwenyekiti wa Tume, nilikuwa nadhani hapa ingepaswa ionekane hivyo. Kwa sababu tukijatukisema kwamba inayomjumuisha mtu yoyote ambaye kwa wakati huo ndie amepewa mamlaka ya kufanya kazi ya Mwenyekiti kama vile tumeyaangusha yale madaraka ya yule ambaye amepewa hadhi ya kuwa Mwenyekiti wa chombo hichi.

Nilikuwa nadhani tutofautishe baina ya Mwenyekiti wa Tume na Mwenyekiti wa Kikao. Kama Mwenyekiti wa kikao haina haja tena ya kutolewa tafsiri hapa, kwa sababu ukisoma huku ndani yenyewe inajieleza kwamba ikiwa Rais atakuwa hayupo nani atakuwa Mwenyekiti. Kwa hivyo hapo katika tafsiri nilikuwa nadhani inamkwaza kidogo, inaangusha ile hadhi ya nafasi ya Mwenyekiti wa Tume hasa kama akiwa ni Rais.

Mhe. Naibu Spika, naomba niende katika Sehemu ya Pili, Kifungu cha 4.1. Mhe. Naibu Spika, kwa kumsaidia Mhe. Waziri ili afatilie vizuri natumia ule waraka ambao umetupa Kamati kwa sababu walitwambia wameshajumuisha marekebisho yote mle ndani.

Kifungu cha 4 kwa ujumla wake hichi kinazungumzia muundo wa Tume. Mhe. Naibu Spika, mimi tofauti na wenzangu sina matatizo sana na Rais kuwa ni Mwenyekiti wa Tume. Nasema kwa sababu Mhe. Waziri katwambia ni uzoefu wa nchi nyingi kwamba yule *head of state* au kwa nchi za wenzetu ambazo kuna Waziri Mkuu mwenye madaraka basi Waziri Mkuu ndio anakuwa Mwenyekiti wa Tume kama hii. Hili linawekwa makusudi kwamba ile mipango inayopitishwa pale imepitishwa na mtu ambaye amepewa dhamana ya kuendesha nchi kwa kipindi kile kwa hivyo ina hakika ya kutekelezwa baada ya kupitishwa na chombo kile.

Mimi hilo halinikwazi, lakini tatizo langu Mhe. Naibu Spika, ukikisoma kifungu cha 4.1 utakuta wajumbe ambao ndio wajumbe hasa wa Tume, wote ni wajumbe wa Baraza la Mapinduzi. Mhe. Naibu Spika, ili nifahamike naomba tuitizame tafsiri ya kiingereza.

Kifungu cha 4.1 kinasomeka *"The commission shall consist of"* halafu wametwaja pale. Sasa neno "*shall"*hawa ni wajumbe. Lakini ukija kifungu cha pili kinazungumza kwa Kiswahili kinazungumza "Rais anaweza kuteua wajumbe wengine" kwa hivyo hawa watatu wengine waliotajwa hapa wanaweza wakateuliwa na wanaweza wasiteuliwe ni jukumu la Rais mwenyewe kuamua.

Katika kutoa nafasi kama hizi Mhe. Naibu Spika, unaweza ukawa na Tume ambayo *basically* inakuwa kama vile ni kamati ndogo ya Baraza la Mapinduzi kwa sababu itakuwa na Rais, itakuwa na Makamo wa Kwanza wa Rais, Makamo wa Pili wa Rais, hapa imeandikwa Mawaziri lakini nilivyoisoma katika ile ya *original* imeandikwa ni Waziri Anayehusika na Masuala ya Fedha, Mipango ya Maendeleo na wajumbe wengine wa Baraza la Mapinduzi.

Ukitizama inakuwa kama ni Kamati ndogo ya Baraza la Mapinduzi. Sasa kama ni Kamati ndogo ya Baraza la Mapinduzi tulikuwa tuna sababu ya kuiundia sheria. Mimi nilikuwa nadhani ili itimize kile kigezo ambacho kimetajwa katika kifungu cha 13 kwamba hii Tume ni ya kitaalamu basi ilipaswa kwenye wajumbe iwekwe sawa baina ya wajumbe wanaotoka Serikalini wanaotoka Baraza la Mapinduzi, wanasiasa na wajumbe ambao watakuwa ni wataalamu ambao wangeweza kutumika katika hichi kifungu cha (b).

Mhe. Naibu Spika, nachelea ikiwa hawa watakuwa hawazidi watatu kama ilivyosemwa hapa na hawa wa juu pengine wanaweza wakafika 6 au 7, itakuwa *element* ya utaalamu ni ndogo kuliko *element* ya wanasiasa. Kwa hivyo nilikuwa nadhani Mhe. Naibu Spika, hili tulitizame kama kweli tunakusudia ni *think tank* la kama tunakusudia ni kamati ndogo ya Baraza la Mapinduzi inashughulikia mambo ya utekelezaji, basi itakuwa haijakidhi ile sifa ambayo imekusudiwa.

Mhe. Naibu Spika, katika kifungu hicho hicho kifungu kidogo cha 3. Wajumbe wa Tume mbali ya wajumbe wanaoingia kwa nafasi zao, watatumikia kwa kipindi cha miaka mitatu na wanaweza kuteuliwa tena kwa kipindi chengine.

Mhe. Naibu Spika, kwa maoni yangu mimi naona tusiwa *restrict* wajumbe kwa miaka mitatu. Kwa sababu kwanza kama nilivyosema kazi hii ni ya kitaalamu. Na kazi za kitaalamu zina sifa moja, kila ukiendelea kuifanya ndipo unapoongeza ujuzi wako na unapopanua maarifa yako. Unaweza ukawa msomi mzuri wa uchumi lakini kwa vile hujapewa nafasi ya kutumika ukawa ule utaalamu wako umeganda lakini kila ukipewa nafasi ya kuutumia ule uzoefu wako unazidi kuongezeka ule ujuzi. Mimi nilikuwa nadhani tusifunge miaka mitatu.
Mhe. Naibu Spika, kipindi cha Serikali ni cha miaka 5 kwa hivyo ingependeza angalau basi miaka mitano, kipindi ambacho Rais na yeye anatumika katika yale madaraka yake ya Urais ili na hawa na wao wapate muda mzuri wa kujenga uzoefu na halafu waweze kutoa mawazo yanayofaa.

Mhe. Naibu Spika, kifungu chengine ambacho nataka nikitolee maoni ni Kifungu cha 6(2) kinachozungumzia Katibu wa Tume. Hapa katika sifa zake imesemwa kwamba mtu atakuwa ana sifa za kuteuliwa kuwa katibu ikiwa atakuwa angalau na shahada ya kwanza. Katika fani ambayo inahusu mipango ya maendeleo, uchumi au masuala ya fedha.

Mhe. Naibu Spika, mimi kwa maoni yangu haidhuru tumezoea sana tukiambiwa kwamba hii ndio kigezo cha chini kabisa cha watu wengi wanaofikiriwa. Lakini nilidhani kwa Tume kama hii kwa uzito wake basi ingetizamwa Katibu wake akawa ni mtu angalau ana Shahada ya Pili. Nimewapa mdano hapa kwamba kwa wenzetu Kenya watu waliopewa kazi hii walikuwa ni watu wenye ma-*PhD* kama Profesa Anyan'g Nyong'o. Najua kwa hivi haijamzuia mwenye *PhD* kuteuliwa, lakini mara nyengine tukishakuweka sifa ya chini Shahada ya Kwanza, anaweza akatafutwa huyo wa Shahada ya Kwanza.

Kwa hivyo nilikuwa naomba Mhe. Naibu Spika, hili waziri alitizame na tufikirie kuweka angalau Shahada ya Pili katika fani hizi. Huyo atakuwa sio tu kuwa amepata ile basic education au elimu ya msingi ya ujuzi wa fani lakini pia atakuwa ameongeza na kiwango fulani cha kujenga uwezo mkubwa zaidi katika fani hii.

Mhe. Naibu Spika, jengine nakuja kifungu cha 8(1) (a). Kwa mujibu wa masharti ya sheria hii kazi za msingi za Tume zitakuwa (a) kutoa ushauri wa kisera kwa Rais na kwa Serikali kwa jumla katika maeneo yote ya maendeleo ya kitaifa kwa jumla.

Mhe. Naibu Spika, sasa napata matatizo kidogo, kwa sababu kwanza unaposema inatoa ushauri kwa Rais lakini Rais mwenyewe ndio mwenyekiti wa Tume hii. Mimi nilikuwa nadhani hapa kidogo tukiweka Rais wakati yeye mwenyewe ni sehemu ya hichi chombo, inakuwa imeandikwa katika lugha ambayo haifurahishi naona kama ina mgongano fulani. Kwa hivyo mimi nilikuwa nadhani tungesema tu kutoa ushauri kwa serikali bila ya kumtaja Rais.

Mhe. Naibu Spika, vile vile katika Kifungu cha 8(1) (d) hichi kinazungumzia kutayarisha na kuandaa mipango ya maendeleo ya kitaifa ya muda mrefu, muda wa kati na muda mfupi na kuratibu mipango hiyo kwa Serikali kuu na Serikali za mitaa. Sasa hili kidogo linanipa shida Mhe. Naibu Spika, hapa kwenye Serikali za mitaa. Kwa sababu katika nchi yetu kwenye Serikali za mitaa kwa maana ya Serikali za mitaa hasa, hazijakuwepo. Na tuliahidiwa muda mrefu sana kwamba tutaletewa *reforms*. Hizi Halmashauri zilizopo za Wilaya haziachii Mamlaka hata ya kupanga mipango ya maendeleo kwa maana ya kuwepo katika *level* ya Tume ya Mipango.

Sasa tunapozitaja tunazitaja sehemu mbili au tatu katika hii sheria, najiuliza hizi zinapanga shughuli gani hasa wakati madaraka yote tumeyalimbikiza katika Serikali Kuu. Nilikuwa nadhani hii tungeiwachia jukumu la kupanga mipango katika ngazi ya Serikali Kuu na hasa kwa udogo wa nchi yetu, sidhani kama Serikali za Mitaa zitakuwa zina *play role* kubwa kama hivyo zinavyotarajiwa kiasi cha kuzungumzia mipango ya maendeleo ya kitaifa.

Mhe. Naibu Spika, hapo hapo kidogo nimepata tatizo naomba Waziri akija anisaidie. Kifungu hichi kinasema kufuatilia na kutathmini miradi na maendeleo ya utekelezaji wa mipango nipo hapa kwenye miradi. Je, kwa kuweka madaraka haya kwa Tume hii, haitoleta mgongano na taasisi nyengine kama *ZIPA*, ambayo nayo imepewa majukumu ya kupokea miradi, kuitathmini

halafu kuiidhinisha. Kwa hivyo nilikuwa naomba hili nalo liwekwe sawa isije ikawa kuna mgongano, hasa kwa kuwa hakuna popote panaposema kama vyombo vyengine kama *ZIPA* vitakuwa chini ya Tume hii. Kwa hivyo nilikuwa nataka hili pia tuliweke vizuri.

Mhe. Naibu Spika, jengine nililonalo katika kifungu hicho hicho nipo kwenye kifungu (i). Kushughulikia masuala yanayohusiana na Ushirikiano wa Kiuchumi, Wakikanda na Kimataifa na kufanya shughuli zilizo muhimu, kuharakisha utendaji kazi uliokamilika wa kazi yote waliyopewa Tume katika sheria hii.

Mhe. Naibu Spika, nilikuwa najiuliza hapa kwamba sisi Zanzibar tuna tatizo kubwa la Mamlaka yetu katika kusimamia uchumi wetu katika eneo la *International Cooperation*. Mara nyingi tumehoji maswali, tumeambiwa hatuna uwezo huo. Sasa je, kwa Tume hii kupewa mamlaka haya si tunajivika kilemba cha ukoka tu. Tume hii itafanyaje kazi ya kushughulikia masuala yanayohusu ushirikiano wa kiuchumi wa Kikanda na Wakimataifa wakati mamlaka haya sisi mpaka leo hatunayo, tunayo kinadharia tu. Tunajua Afisi ya Rais mpaka sasa hivi ndiyo inayoshughulikia mambo hayo, lakini kiuhalisia kila pahala ukiingia unakatwa miguu, unaambiwa hapo Zanzibar haina mamlaka, wenye mamlaka ni Jamuhuri ya Muungano. Nilikuwa naomba na hili nalo kuwekwa sawa.

Mhe. Naibu Spika, kwenye kijifungu cha pili cha kifungu hichi, vifungu vingi vimeanza na maneno kutoa mapendekezo hasa kwenye (b), (c) na (d). Mhe. Naibu Spika, mimi sikuipenda, nilikuwa nadhani Tume hii ndio imepewa jukumu la kupanga hiyo mipango ya maendeleo. Kwa sababu kutokana na kuwa inaongozwa na Rais mwenyewe, kwa hivyo hichi ni chombo kikubwa. Sasa kinaposema kwamba kinatoa mapendekezo, mapendekezo haya yanakwenda kwa nani? Huyo ambaye anakwenda kuamua zaidi ya Rais. Mimi nadhani lugha ingekuwa moja kwa moja tu.

Mhe. Naibu Spika, kwa wenzetu uzoefu ulivyo kwa sababu hichi ndio chombo cha kitaalamu *(think tank)*, hichi ndio kinapanga, hakitoi mapendekezo. Kwa sababu wanafanya kazi kwa misingi ya utaalamu badala ya misingi ya kisiasa. Lakini tukisema kutoa mapendekezo, kama mapendekezo hayo baadaye yanakwenda kwenye Baraza la Mapinduzi ambao ni wana siasa. Tunaweza tukaja tukaishia ikawa wanasiasa *approach* zao ndizo zinazo *determine* maendeleo ya nchi na mipango yake badala ya wataalamu.

Mhe. Naibu Spika, naomba nende katika Kifungu cha 12. Kifungu hichi kinazungumza katika kutekeleza uwezo uliopewa chini ya kifungu cha 9 cha sheria hii. Tume itaratibu mipango ya maendeleo ya kisekta (a) Kuitisha vikao vya kabla ya bajet kwa watu wa kawaida, wataalamu na wanasiasa kwa madhumuni ya kupata mawazo ya kuzingatiwa katika mwaka unaofuata wa fedha.

Mhe. Naibu Spika, suala langu hapa linakuja kwa Mhe. Waziri ili aje anisaidie. Mimi nilidhani Tume inapanga mipango ya *long time* halafu inaigawa kwa vipindi tofauti katika utekelezaji. Sasa baadaye jukumu la kutayarisha bajeti na utekelezaji wake inarudi Serikalini kwa Waziri kila mmoja akichukua sehemu yake inayotokana na ile mipango ilivyoandaliwa.

Sasa ikiwa Tume tunaipa kazi ya kuandaa mapendekezo ya kila mwaka, nahisi kama vile Tume tunaiteremsha mno kwa kazi ambayo ingepaswa kuwa ya Wizara zinazohusika katika sekta zake. La kama nimemfahamu tofauti, itakakuwa kama alivyosema Mhe. Asaa kwa sababu hatukupewa Semina ndio maana hatukuielezwa. Naomba hili kidogo Mhe. Waziri akija atuwekee sawa.

Mhe. Naibu Spika, kifungu cha 13 kama nilivyosema kimeanza vizuri kwamba Tume kitakuwa ni chombo cha kitaalamu. Nakikubali lakini ikiwa kule kwenye muundo wa Tume kifungu cha 4 kitafanyiwa marekebisho ili ku-*reflect concept* iliyotajwa hapa kwamba hichi ni chombo cha kitaalam.

Mhe. Naibu Spika, katika kifungu cha 17, hichi kinazungumzia *secretariat*. Hapa imetajwa *secretariat* kwamba itaundwa na Idara za Utawala za Tume na Kamati ya Kitaalamu ya Tume. Hizi Idara za Utawala za Tume zimetajwa baadaye kwamba wakuu wake watateuliwa na Rais. Lakini halafu kwenye Kamati imesemwa kutakuwa na watu wengine wasiozidi watano, watakaoteuliwa na Tume kutokana na mapendekezo ya Waziri kama masharti na misingi itakavyoelekezwa na Tume.

Nilikuwa nataka nisaidiwe, hapo tunaposema kwamba watateuliwa na Tume. Je, ni Tume kwa ujumla wake kama kikao ndio inateua au Mkuu wa Tume ambaye ni Rais ndiye anayeteua. Kwa sababu wale wakuu wa idara wametajwa wazi kwamba watateuliwa na Rais. Nilikuwa naomba na hili pia akija Mhe. Waziri anisaidie kuniwekea wazi.

Mhe. Naibu Spika, nende kwenye kifungu cha 18(5), kinasema kwamba Wajumbe wa Kamati watalipwa posho na stahili kuhusiana na kazi zao kama Waziri atakavyoidhinisha. Mimi kidogo hapa napata matatizo na hili pia lipo katika wajumbe wa Tume kule mbele pia inazungumzia hivyo hivyo kwamba watapewa posho na stahili zao kulingana na kazi. Mimi nilidhani hichi chombo ni cha kudumu, hawa ili wafanye kazi zao vizuri ni vyema wangelikuwa ni watu ambao wanaajiriwa na wanafanya kazi zao kwa misingi ya kudumu na wanalipwa mishahara, badala ya kuwa ni watu wa vikao kwa sababu ya kamati wanakuja kwa shughuli maalum.

Mhe. Naibu Spika, mara nyingi uzoefu unaonesha ukija katika muundo kama huu watu wanakuwa hawafanyi kazi zao vile ambavyo wanapaswa wafanye hasa na kuzipa *commitment* ambayo inapaswa iwepo. Nilikuwa nadhani hili Mhe. Waziri alitizame tena.

Kifungu cha 20(1) kinasema Katibu Mtendaji kwa kuzingatia sheria ya Utumishi wa Umma Nam. 2 ya mwaka 2011 atapendekeza kuajiriwa idadi ya wafanyakazi kama atakavyoona inafaa kwa ajili ya utendaji bora wa kazi za Tume.

Kifungu cha 20(2) kinasema kwa madhumuni ya kulinda hayo na mamlaka ya kikatiba ya Tume hakuna mfanyakazi atakayehamishwa katika tume bila ya ridhaa ya Katibu Mtendaji. Mhe. Naibu Spika, nilikuwa naomba hili nisaidiwe huku juu katika kuajiriwa idadi imesema atapendekeza, bila shaka wateuzi wanaweza kuwa ni ile Tume ya Utumishi wa Umma. Huku chini inasema hakuna mfanyakazi atakayehamishiwa katika tume bila ya ridhaa ya Katibu Mtendaji. Je, hakukuwa na *contradiction* hapa yupi mwenye mamlaka hasa? Nilikuwa naomba hilo pia tuliweke wazi.

Mhe. Naibu Spika, halafu nije katika kifungu cha 21 kifungu kidogo cha 4, nimesema kwa madhumuni ya kifungu hiki tume itaratibu upangaji wa maofisa wa uchumi na mipango ya maendeleo katika taasisi za utumishi wa umma. Mhe. Naibu Spika, kidogo hili limenipa mashaka, kwanza huko mbele kunazungumzwa kamati za maendeleo ambazo zimeundwa kwa sheria za miaka ya 86 katika mawizara na katika Mikoa. Lakini hapa pia inazungumziwa tume utaratibu wa upangaji wa maofisa wa uchumi na mipango ya maendeleo. Mhe. Naibu Spika, nilikuwa najiuliza kutakuwa na maofisa wengine wapya.

Mhe. Naibu Spika, mimi ninavyofahamu kwa mfano kila wizara katika muundo mpya wa serikali kwa miaka kadhaa sasa kumekuwa na Mkurugenzi wa Mipango, Sera na Utafiti. Je, huyu hawi ndiye mwenye dhamana ya hayo ambayo yangepaswa yafanywe na huyo ofisa anayetajwa hapa. Hatuongezi watu ambao kwa kuajiri tu Mhe. Naibu Spika, na kuongeza gharama serikali kwa kazi ambayo ingepaswa ifanywe na yule Mkurugenzi. Nilikuwa naomba pia hili akija Mhe. Waziri anisaidie.

Mhe. Naibu Spika, nilikuwa naomba niende sehemu ya 4 kifungu cha 24 (4). Hiki kidogo kimenitisha Mhe. Naibu Spika, kinasema:

“Iwapo kwa maoni ya mwenyekiti au mjumbe yeyote wa tume, suala lolote litakuwa lina umuhimu usio wa kawaida usioweza kungoja kuitishwa mkutano utakaotimiza akidi, suala hilo litaamuliwa na mwenyekiti na angalau nusu ya wajumbe na uamuzi huo utakuwa ni halali na wenye nguvu, na uamuzi huo utatolewa taarifa katika mikutano ya kawaida ya mwaka ya tume”.

Mhe. Naibu Spika, kidogo mimi nimepata mshtuko hapa. Kwanza mikutano ya kawaida inafanyika mara nne kwa mwaka, lakini tunasema inapokuwa mwenyekiti hayupo mwenyekiti atakayekuwepo au mjumbe mwengine yeyote wa tume akiona kuna suala muhimu anaweza asingoje kuitishwa kikao akaamua suala akishakupata nusu ya idadi ya wajumbe.

Je, hakutakujakuwa na *possibility* hapa ya watu kutumia mwanya kwa mwenyekiti awe Rais hayupo hao viongozi wengine wakafanya maamuzi ambayo yatakuja kuifunga nchi na baadaye wakati wa kuja kuihalalisha itakuwa kipindi kirefu kimeshapita, pengine kama maamuzi yameshaanza kutekelezwa yakaathiri nchi. Mhe. Naibu Spika, hapa kidogo mimi pamenitisha nilikuwa namuomba Mhe. Waziri akija aangalie vizuri.

Mhe. Naibu Spika, kifungu cha 27 maoni yangu kuhusu mafao na posho za wajumbe. Mimi kama nilivyozungumza kule kwenye kamati sina haja ya kuyarejea tena, mimi nilikuwa naomba hao wanapaswa wawepo wafanye kazi ya kutupangia mipango mizuri ya maendeleo ili tuondokane na yale ambayo yalikuwa yanatukwaza huko nyuma.

Mhe. Spika, niende moja kwa moja katika kifungu cha 31 kifungu kidogo cha 2, hii inahusu ile kuanzishwa kwa Kamati ya Mipango katika kila Wizara na Mkoa. Halafu kifungu kidogo cha 2 kikazitambua zile ambazo zilikuwepo tangu zamani. Lakini kifungu kidogo cha 3 kinasema:

“Kamati za maendeleo za Wizara, Mikoa na Serikali za Mitaa kama itakavyokuwa zitakuwa dhamana kuidhinisha mipango ya maendeleo, usimamizi wa jumla na ufuatiliaji wa utekelezaji

katika maeneo ya mamlaka yao na tume itakuwa dhamana kufuatilia na kuhakikisha kwamba kamati hizo zinafanya kazi kwa ufanisi na mafanikio:.

Mhe. Naibu Spika, hapo kidogo mimi nimepata tatizo, mimi naona kama pana *contradiction* huku nyuma tumeshasema hii tume ndio itakayokuwa na jukumu la kupanga shughuli za maendeleo kwa Serikali Kuu na serikali za Mitaa. Lakini hapo tutasema hizi Kamati za Maendeleo zitakuwa ndio dhamana kuidhinisha mipango ya maendeleo. Je, yupi ana dhamana ya kuidhinisha mipango hii ya maendeleo Mhe. Naibu Spika, pasije pakatokezea mkanganyiko wa madaraka hapa. Mhe. Naibu Spika, nilikuwa naomba hili pia Mhe. Waziri akija alitzame.

Mhe. Naibu Spika, la mwisho kabisa liko katika jadweli kiapo cha utiifu chini ya kifungu cha 7.

Mhe. Naibu Spika, tunaambiwa kila siku kwamba mambo ya uchumi sio mambo ya Muungano, kwa hiyo na mambo ya mipango pia si mambo ya Muungano. Mimi kidogo hiki kiapo kilikuwa kinanikwaza, kwanza kinanikwaza kwa sababu hivi kilivyoandikwa haki-*reflect* Katiba ilivyo kinasema:

“Mimi …… naapa kwa jina la Mwenyezi Mungu kwamba nitakuwa mwaminifu kwa Zanzibar na watu wake ambayo ni sehemu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kwamba nitatumikia kama (Mjumbe au Katibu) kwa Tume ya Mipango, kwa moyo wote na kwamba nitalinda na kuhami maslahi na uchumi wa Zanzibar kwa kufuata sheria zilizowekwa. Ewe Mungu nisaidie”.

Mhe. Naibu Spika, lugha hii tumeshaiwacha kwenye Katiba na katika Kanuni zetu. Lakini pili mimi hata nilikuwa sioni umuhimu wa kutaja hata kama ni moja wapo ya nchi mbili, kwa sababu tume hii inashughulikia mambo ya ndani ya Zanzibar ambayo sio mambo ya Muungano. Na hata ukisoma kiapo tiririkaji huko chini kinaizungumzia Zanzibar kina watu wake. Kwa hivyo, nilikuwa nadhani hii jadweli Mhe. Waziri atukubalie lirekebishwe i-*reflect* kwa yale madaraka ambayo Zanzibar ni yake kwa mujibu wa mkataba wa Muungano basi yaendelee kuwa yetu bila ya kurithisha upande wa pili wa ndugu zetu wa damu. Mhe. Naibu Spika, baada ya kusema hayo nitaunga mkono hoja baada ya kupata ufafanuzi ambao nimeomba, nakushukuru kwa kunivumilia ahsante sana.

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe naomba kuwajuilisha kwamba tumepata ugeni wa wajumbe 10 wamekuja kusikiliza michango yetu katika Baraza letu hili tukufu lilo anza leo. Kwa hivyo, naomba niwatambulishe mmoja mmoja ili muweze kuwatambua.

1. Monica Korzelius - Netherland.
2. Njeri Kamau - UNDP.
3. Aran Corrigan - Embassy of Ireland
4. Mathew Kihulya - Embassy of Ireland
5. Diana Henderson - Development Partner Group
6. Geraldine Zeuner - Embassy of Switzerland
7. Serena Bertaina - European Union Delegation
8. Veslemoy Salvesen - Norwegian Embassy
9. Jeff Smith - America Embassy

10. Dommy Dedeyan - USAID. Ahsanteni sana Waheshimiwa Wajumbe.

Mhe. Ali Mzee Ali: Mhe. Naibu Spika, kwanza nikushukuru kwa kunijaalia nafasi hii leo jioni, wenzangu wengi kwa niaba ya majimbo yao wametoa mkono wa rambi rambi kwa ndugu yetu ambaye ametangulia mbele ya haki. Na mimi kwa niaba yangu mwenyewe binafsi na kwa niaba ya wateuzi wa Rais Jimbo la Ikulu na sisi tunatoa mkono wa pole kwa wafiwa hawa na Mwenyezi Mungu amjalie roho yake ilale pahali pema peponi. Amin.

Mhe. Naibu Spika, kwanza nataka kuchukua nafasi hii kumuomba Mhe. Waziri atupelekee salamu zetu kwa ndugu zetu wa sehemu ya mipango Wizara ya Fedha kuwa ile semina au mafunzo waliotupa kwa siku mbili namna ya kutengeneza utaratibu wa bajeti, namna ya kujua MKUZA na mambo mengine. Mhe. Naibu Spika, mimi huu ni mwaka wa 12 niko hapa bajeti nyingi nimezihudhuria, lakini sijapata kuona miezi 4 kabla ya bajeti kuwa tunaandaliwa mafunzo tukafundishwa. Kwa hivyo, kwa niaba ya wajumbe wenzangu wote tunataka kutoa pongezi kwa Wizara ya Fedha kwa kazi nzuri waliyoifanya.

Mhe. Naibu Spika, hiyo ni moja katika kazi ya mipango kwani mipango inaanza kutoa matunda. Kwa hivyo, ukitizama historia yetu hii ni sheria ambayo leo tunaifanyia marekebisho, sheria Nam. 5 ambayo ilisainiwa na Marehemu Idrissa Abdul-wakil tarehe 31 Julai, 1989, sasa hivi ni miaka 23 sheria hii haijaguswa, huo ni muda mrefu sana. Mhe. Naibu Spika, hii Katiba yetu sasa hivi ni miaka 28 lakini imeshafanyiwa mabadiliko mara 10, yaaani avarage ya kila miaka 2 au miezi 8 inabadilika, hii ni miaka 23. Kwa hivyo, napenda kuchukua nafasi hii kumpongeza Mhe. Waziri na serikali kuona haja ya kufuta sheria hii na kulinda sheria nyengine ambazo zinakwenda na wakati. Mhe. Waziri tunakushukuru sana na kwa juhudi hizi.

Mhe. Naibu Spika, ni kwamba sheria hii ilipoanzishwa mwaka 1989 tukaingia mwaka 90, mwaka 95 Rais wa Zanzibar Dk. Salmin Amour Juma alianzisha Wizara ya Mipango na kule Wizara ya Fedha. Kwa bahati nzuri wajumbe wote wawili waliongoza wizara ile ni Mhe. Ali Juma Shamuhuna na Katibu Mkuu wake ndugu Omar Yussuf Mzee. Kwa hivyo, ndugu Omar ni Katibu Mkuu Wizara ya Mipango ni wao ndio waliozaa wazo la 99, 2000 kwenda mbele huko na 2020.

Mhe. Naibu Spika, ndugu Omar ni mzoefu amekuwa Katibu Mkuu Mipango, mwaka 2000 akawa Katibu Mkuu Ofisi ya Waziri Kiongozi, mwaka 2005 akaingia uwanjani akenda Bara akawa Naibu Waziri wa Jeshini, akawa Naibu Waziri Fedha na mwaka huu amerudi hapa. Kwa hivyo, kukabidhiwa yeye kuwa ni Katibu Mkuu Ofisi ya Rais Fedha kwa wale waimbaji wanasema nyuki kufa juu ya asali ni pahala pake, na nzi kufa juu ya kidonda huyo ndio pahala pake hasa. Hongera sana.

Mhe. Naibu Spika, sasa nije kwenye hii sheria ni kwamba sheria hii haijazuka kifungu cha 125 cha Katiba katika sura ya 12 kinasema:

Kifungu cha 125 (1) “Kutakuwa na Tume ya Mipango ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ambayo ndio chombo cha juu chenye uwezo wa kupanga na kusimamia utekelezaji wa maendeleo ya kiuchumi na mpango ya huduma za jamii katika Zanzibar”.

(2) “Taratibu za utekelezaji wa kazi na majukumu ya Tume ya Mipango pamoja na wajumbe wa tume utakuwa kama ilivyoelekezwa katika sheria itayotungwana Baraza la Wawakilishi”.

Kifungu cha 126. “Wajumbe wa Tume ya Mipango na utaratibu wa mikutano utakuwa kwa mujibu wa sheria itakayotungwa na Baraza la Wawakilishi la Zanzibar”.

Kifungu cha 127. “Kutakuwa na Katibu wa Tume ya Mipango ambaye atateuliwa na Rais”.

Mhe. Naibu Spika, sheria ambayo itafanyiwa mabadiliko imetungwa kwa agizo la Katiba inasema: *The planning commission establishment on the commission there is her by established a commission to be known as planning commission. The commission shall be independent department of government under the office of the president. The commission shall consist of members whose number including the chairman shall be not exceed seven.* Hii sasa imefutwa imeongezwa. *The chairman of the commission shall be the President.*

Kwa hivyo, sheria imefuata agizo la Katiba, sasa kwa kuwa chombo hiki ni chombo chenye mamlaka ya juu kabisa katika mipango sasa hivi kimefanyiwa marekebisho mengine ambayo yanasema: Sheria ya kuanzisha Tume ya Mipango kifungu cha 4(1) tume itakuwa na:

(a) Rais ambaye atakuwa Mwenyekiti;
(b) Makamo wa Kwanza wa Rais;
(c) Makamo wa Pili wa Rais;
(d) Waziri anayehusika na masuala ya fedha na mipango ya maendeleo; na
(e) Wajumbe wengine wa Baraza la Mapinduzi watakaoteuliwa kwa umoja wao kama Wajumbe wa Kamati za Baraza la Mapinduzi au kwa nafasi yao kila mmoja kama Rais atakavyoona inafaa.

Mhe. Naibu Spika, hapa Katiba inasema chombo cha juu chenye uwezo hakuna mwengine anayestahiki kukiongoza chombo hiki isipokuwa Rais. Rais sio mtu, Rais ni taasisi. Mhe. Naibu Spika, chombo kikubwa kama hiki lazima na inapendeza na ndivyo inavyofaa kiongozwe na Rais. Rais ambaye ni mzoefu, mwaka 1995 wakati tunaanzisha vyama vingi huyu Rais wetu kama mwananchi alikuwa Afisa huko Wizara ya Afya, hivyo akaamua kwa kuipenda nchi yake kupigania jimbo na kuingia kwenye siasa. Mhe. Naibu Spika, kule Pemba Wilaya ya Mkoani katika kijiji cha Mkanyageni na hali kule ilikuwa ni ngumu sana lakini akasema mimi ninaacha kazi, akenda kugombania lakini kura zake hazikutosha. Lakini Mhe. Dk. Salmin Amour akamteuwa akawa Naibu Waziri wa Afya kwa miaka 5.

Mhe. Naibu Spika, mwaka 2000 hakuvunjika moyo akaingia tena na kura zake zikatosha, Mhe. Rais Amani Abeid Karume akamchagua akawa ni Waziri wa Katiba na Utawala Bora, akafanya kazi kwa miaka mitatu akapandishwa cheo akawa Makamo wa Rais kwa muda wa miaka 9. Kwa hivyo, sifa kama hizo ndio *CV* ya kusema tunamkabidhi ingekuwa mtu mwengine tungesema hapana, lakini kwa sababu ya sifa hizo basi ana kila sifa, ana uzoefu wa kuongoza chombo hiki.

Mhe. Naibu Spika, na mimi nawaomba wenzangu wale ambao walisema vyenginevyo hivyo tukubaliane chombo hiki akiongoze na tupate faida. Kwa sababu tumeshaanza kuona faida za

tume na mengine mengi tunayaelewa na faida tumeziona. Kwa hivyo, nafikiri ipo haja Rais chombo hiki akiongoze.

Mhe. Naibu Spika, mimi sikutaka niseme sana kwa sababu hili jambo tunalifanyia marekebisho tu, lakini nimeona nichukue muda huu mfupi nieleze haya kwani mengine ni mambo ya kawaida. Lakini mimi nina matumaini wakati tulipokuwa na semina tulisema 2020 imetwambia muda wenyewe haupo, lakini mimi nasema muda upo hivyo tuwape nafasi wenzetu wafanye kazi na tume hii. Mimi ushauri wangu ni kwamba wajumbe wengi wanaingia kwa kura zao, lakini na wale wengine watafute watu wenye maarifa, wenye busara na wenye hekima na ni watu wale ambao haya mambo ya uchumi na mipango na sasa hivi miaka 48 alhamdulilah tunamshukuru Mwenyezi Mungu.

Mhe. Naibu Spika, juzi Mhe. Rais alikutana na Ma-*professor* wametoka Norway, wametoka Marekani, wametoka Uingereza na katika *Professor* mmoja ni mkwe wake Mhe. Omar Yussuf wale tuliokwenda siku ile kule Ulaya kina Mhe. Nassor Ahmed Mazrui, Mhe. Haji Omar Kheir tulimkuta kule Farouk Topan tulikutana na vigogo wa kizungu na yeye huyo Farouk alikuwepo. Mhe. Naibu Spika, hao wote walikuja juzi hapa wakakutana na Mhe. Rais na wako tayari kuisaidia nchi yao, hivyo tuwapongeze kwani ni wenzetu hao. Kwa hivyo, miaka 48 wapo watu ambao wanaweza kupata hizi shughuli na wakazifanya kwa ufanisi.

Mhe. Naibu Spika, kwa hayo machache nawaomba ndugu zangu tuupitishe mswada huu kama asubuhi kwa kauli moja tuendelee mbele na Rais abakie katika kazi hii. Mhe. Naibu Spika, kwa hayo mafupi mimi naunga mkono ahsante sana.

Mhe. Mwanasheria Mkuu wa Serikali: Mhe. Naibu Spika, kwanza nakushukuru kwa kunipa fursa hii na mimi kuchangia machache katika hoja hii ya Mhe. Waziri wa Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo kuhusiana na Mswada wa Kuunda Tume ya Mipango. La pili naomba na mimi niungane na wenzangu kutoa rambi rambi kwa wananchi wa Jimbo la Bububu kwa kifo cha mwakilishi wao Mhe. Salim Amour Mtondoo.

Mhe. Naibu Spika, vile vile naunga na wenzangu kumpongeza Mhe. Mohammed Raza kwa kuungana na sisi hapa. Naamini kwamba itakuwa ni nguzo nyengine katika Baraza ya kutusaidia katika mijadala na hoja mbali mbali ambazo tunazishughulikia. Pia nataka nimpongeze Mhe. Waziri kama alivyosema sasa hivi vyeo vimekuwa vingi sijui nitumie kipi, lakini nitatumia hiki cha mwisho cha walii Mhe. Ali Mzee Ali kwamba tume kwa muda mrefu kama tunavyoona sheria yake baada ya kupitishwa mwaka 1986 ilifanyiwa marekebisho mwaka 1996 na tokea wakati huo tumekuwa tukenda na sheria hiyo bila ya kufanyiwa marekebisho ya msingi.

Mimi naomba pia niwatanabahishe Waheshimiwa Wajumbe kwamba kabla ya kuandaliwa mswada huu wizara ilifanya utafiti wa kina kuhusiana na Tume ya Mipango. Huu ni mmoja katika miswada ambayo imeandaliwa kwa kweli baada ya kufanyika utafiti wa kina kabisa, ni mswada ambao umeandaliwa kitaalamu na nadhani kama ingekuwa wajumbe walipata fursa ya kupitia ile taarifa kwa kina kabisa yenye kurasa karibu 100 inayohusiana na utafiti kuhusiana na muundo bora wa Tume ya Mipango ambayo itatakiwa Zanzibar tuwe nayo, naamini wasi wasi wao au yale maswali mengi ambayo yameulizwa basi yasingekuwepo.

Mhe. Naibu Spika, katika ufiti huu kwanza imezingatiwa huko ambako tumetoka tukiangalia kwenye Tume ya Mipango ni moja katika chombo ambacho kimekuwepo kwenye Katiba yetu kwa muda mrefu, lakini muundo wake umekuwa ukitofautiana kutoka wakati na wakati.

Tulikuwa na tume katika mfumo wa Baraza la Mipango ambalo lilikuwa na wajumbe hadi kufikia 200. Baraza la Mipango kwa sababu lilikuwa linawashirikisha wajumbe kutoka Wilaya zote 10 za Zanzibar, na kwa maana hiyo ukija ukihesabu siku ya kuitishwa Baraza la Mipango kuna wajumbe karibu 200, ndio hao wanaokuja kupitisha mipango yenu ya kitaifa. Kwa hivyo, ilikuwa ni Tume ya Ushirikishwaji lakini ukaja wakati tukawa na Wajumbe wa Tume ambao ni wa kudumu, nalo hilo likawa ni tatizo jengine.

Mhe. Naibu Spika, ulifika wakati tukawa na tume ambayo kwa kweli ni kama *stop over* ya bajeti tu, kwamba mipango imeshaandaliwa ipitishwe Tume ya Mipango kabla ya kuja Barazani. Lakini kufanya hasa ile kazi ya kitaalamu kama ambavyo ilikusudiwa kufanywa chini ya muundo huu mpya kwa kweli hilo lilikuwa limekosekana.

Kwa hivyo, tume hii imeundwa na ukitizama hata kazi zake mbali ya kutajwa za jumla, lakini pia zimefafanuliwa kifungu kwa kifungu, yaani kila kazi ya tume basi kuna vifungu ambavyo vimejaribu kuzifafanua kwa urefu kabisa. Kwa hivyo, kutokana na sababu hizo mimi naomba kwa dhati kabisa nimpongeze Mhe. Waziri kwa maandalizi yao haya ya kitaalamu kabisa ya mswada huu wa Tume ya Mipango.

Mhe. Naibu Spika, suala moja ambalo lilikuja ni suala la muundo wa Tume ya Mipango yenyewe. Mhe. Naibu Spika, Mimi naomba tuiangalie kwamba Tume yenyewe kwanza tukiusoma huu mswada kutoka mwanzo mpaka mwisho, tutaikuta kuwa ina sehemu mbili, pengine hiyo inaweza ikatufanya labda tushindwe kuona utaalamu uko wapi na kazi za maamuzi ziko pahala gani. Tume ina tume yenyewe kwa maana ile ya Rais na wajumbe wengine wa Tume, lakini kwa upande wa pili kitaalamu hasa, na ambao ndio wataendesha shughuli za kila siku za Tume hasa, ziko katika sekretarieti ya Tume.

Mhe. Naibu spika, nadhani huu ni utaratibu wa kawaida kabisa kwamba kunakuwa na chombo cha maamuzi lakini pia kunakuwa na chombo cha kitaalamu. Sasa ukichanganya hivyo viwili, na hasa hiki cha sekretarieti hasa, ndicho kinachokusudiwa kwamba Tume ipate nguvu zake za kitaalamu kutoka pale. Ndio maana kuna Idara lakini pia kutakuwa na "*technical committee"*, kwamba taarifa yoyote itakayokuja, utafiti wowote utakaokuja baadae unakwenda kwa hii Kamati ya Wataalamu, ambayo itahusisha watu mbali wa kwenye tume, lakini na nje ya tume,na baadae ripoti ya hii Kamati ya wataalamu ndio itakwenda katika tume yenyewe ambayo ni ya Mhe. Rais na viongozi au wajumbe wengine kwa ajili ya kufanya maamuzi ya yale mambo.

Kwa hivyo, tunapozungumza Tume ya Wakuu wa Kitaalamu tuitizame katika mtazamo huo, na ndio makusudi. Na tukitazama za wenzetu takriban wote kwa mujibu wa hii *study* iliyofanywa ndio utaratibu wake, kwamba wanaposema Tume ni *think tank* maana yake ni kuimarisha zaidi utaalamu katika *level* ile ya sekretarieti.

Lakini Mhe. Naibu Spika, limekuja swali kwa nini Rais ndio awe Mwenyekiti wa Tume ya Mipango? Kwanza naungana na Mhe. Ali Mzee Ali na pia Mhe. Ismail Jussa Ladhu waliosema

kwamba hili linafaa zaidi kutokana na kazi zenyewe za Tume. Lakini tukiangalia hata kwenye Katiba yetu ya Zanzibar, kile kifungu ambacho ameki-*quote* Mhe Ali Mzee pale kifungu cha 125, Tume yenyewe sio chombo labda kama zilivyo *agencies* nyengine, lakini hiki kimepewa jukumu la msingi la kuandaa mipango ya nchi. Kwa hivyo, unaposema mipango ya nchi ni jambo la kitaifa.

Nadhani Mhe. Naibu Spika, Waheshimiwa watakubaliana na mimi kwamba katika nchi za wenzetu, hata katika nchi yetu inapotokea kuna vita basi Rais anaunda kinachoitwa *kind of war cabinet*, yaani ni Baraza la Mawaziri lakini Kamati maalum ndio itayosimamia suala lile la kitaifa kwa karibu zaidi. Sasa na mipango ya nchi, kuidhinisha nani apate kitu gani, vipi twende, hilo ni suala la kitaifa ni vita vyengine katika Taifa. Kwa hivyo, ndio maana ule muundo wa Tume katika takriban nchi zote kama hukumkuta Rais, basi utamkuta ni kiongozi wa *cabinet*, Waziri Mkuu, na Waziri Mkuu wa hizo nchi ambazo yeye ni kiongozi wa Tume ya Mipango basi atakuwa yeye pia ndie kiongozi au ndie *head war* wa *cabinet.*

Uzoefu ambao umeelezwa hapa labda nchi moja tu, Namibia wao labda Director General ndie anayekuwa kiongozi wa Tume ya Mipango. Lakini hata huyu anaitwa tu, lakini anaingia kwenye *cabinet* vile vile. Kwa hivyo, ule umuhimu wa kuwa na Rais ni kwa sababu ya uzito wa chombo chenyewe kama kilivyoelezwa ndani ya katiba, majukumu yake, lakini na uzoefu wa takriban asilimia 80 ya nchi ambazo zimefanyiwa uchunguzi kuhusiana na miundo ya Tume hizi za Mipango. Wengine wanaita *Planning Authority*, wengine wanaita *Planning Commission,* kwa majina yoyote lakini ukitizama uzoefu ni kwamba kiongozi ndie anayekuwa Mwenyekiti wa Tume ya Mipango yenyewe.

Kwa hivyo, mimi niseme kwamba nadhani wenzetu waliofanya hivyo kama vile Uganda hata Tanzania Bara nao wamefanya kwa uzito ule ambao hata sisi wenyewe katiba yetu imelitambua suala hilo.

Lakini kuna suala lile la Wajumbe wasiokuwa *X office,* yaani imesema kwamba Rais anaweza akateua wajumbe wengine wasiozidi watano. Ukweli imewekwa kwamba ni *optional* ili kutoa fursa isimlazimishe Rais kwamba lazima atafute watu wengine, lakini atafute pale *absolute*, atakapoona kuna mahitaji ya kufanya hivyo. Kwa hivyo, hii inatoa upeo zaidi kwa Rais mwenyewe kuona kwamba anahitaji watu wa namna gani, anahitaji watu wangapi na je anawahitaji katika kumsaidia kwenye jukumu hili?

Lakini unapoamua tokea mwanzo, kwamba muundo wa Tume uweje, uzoefu uliopatikana katika nchi za wenzetu ni kwamba hilo si jambo zuri sana, jambo zuri ni kwamba, wawepo wale viongozi wa msingi ambao ni wajumbe wa *cabinet*, lakini hawa wengine izingatiwe na mahitaji na ndio maana ikawekwa kwamba Rais anaweza. Tungesema kwamba Rais atateua, ina maana angelazimika kisheria na hata pengine mwenyewe hajaona kama kuna umuhimu huo, lakini sheria inamlazimisha na hilo uzeofu ambao umepatikana kwa wenzetu si jambo muafaka zaidi, muafaka zaidi ni kuwa na "*a very strong secretariat"* ambayo itaweza kufanya kazi za kitaalamu na baadae kupeleka kwenye hiki chombo kwa ajili ya kufanyiwa maamuzi.

Jambo jengine la msingi, ni kwamba kuliulizwa uteuzi wa wale wajumbe wengine watano wa Kamati ya Wataalamu kwamba hili litakuwa ni suala la Rais mwenyewe kama mwenyekiti ama litakuwa ni suala la Tume kama tume?

Hapa limewekwa wazi kabisa, kwamba hawa watateuliwa na Tume yenyewe kwa mapendekezo ya Waziri. Kwa hivyo, hawa hawatateuliwa na Rais, na kwenye sheria inapokuwa kuna wengine wanateuliwa na Rais, wengine ukasema na chombo chengine, haidhuru Rais yumo, basi maana yake nyinyi mnaopitisha sheria hapa mmekusudia kwamba hawa wateuliwe na hicho chombo na sio Rais. Kwa sababu kama mngelitaka wateuliwe na Rais, basi sheria ingesema hawa wateuliwe na Rais. Lakini kwa namna kilivyowekwa, ni wazi kwamba watateuliwa na Tume yenyewe kutokana na mapendekezo ya Waziri.

La mwisho, labda niseme ni suala la kifungu cha 31(3) ambacho Mhe. Ismail Jussa Ladhu aliuliza kwamba, sasa mbona huku tunasema ni Tume ndio yenye uwezo wa kuidhinisha, lakini huku tunasema hizi Kamati ndizo zenye uwezo wa kuidhinisha.

Mhe. Naibu Spika, nadhani kwenye uzoefu wa Tume zilizopita, au mpaka sasa hivi, utaratibu tunaoendelea nao ni kwamba hii mipango, kwa mfano wa kisekta inaanza katika Wizara, Wilaya au Mikoa, lakini kule kwa utaratibu wa sasa hivi, ni kana kwamba hakuna utaratibu maalum maana hili ni jambo kubwa. Lakini sasa hakuna utaratibu ulioangaliwa kuwa mamlaka ipi ndio ambayo itaidhinisha huu mpango wenyewe, ambao umetoka kwenye Wizara au umetoka kwenye Mkoa au Wilaya, kabla haujenda juu, haujafika kwenye sekretarieti baadae ukaishia kwenye Tume ya Mipango.

Sasa hii sheria inajaribu kuweka mfumo wa *development planning* kuanzia katika ngazi za chini mpaka ufike katika kiwango cha Tume. Kwa hivyo, ndio maana kifungu kile kimeweka wazi ili kusiwe na utatanishi, sasa mtu mwenyewe ambaye ataamua, kwa sababu wakati mwengine hata waziri anaweza akaja akasikia tu, kwamba huo mpango umeshapelekwa Wizara ya Fedha. Lakini yeye mwenyewe Waziri wakati mwengine anakuwa hana habari, Mkuu wa Mkoa inawezekana hana habari, wataalamu wamechukua mamlaka hayo.

Kwa hivyo, hili sasa ni kuliweka wazi, kwamba ile Kamati ya Uongozi ya Wizara, basi iwe na jukumu la kuhakikisha kwamba mpango unaoanzia katika Wizara, wao ndio wanaidhinisha. Lakini kuidhinisha kwao haina maana kwamba basi ndio huo umepita, lakini ni katika ile ngazi ambayo imezungumzwa, katika ngazi ya Wilaya ni kamati hiyo iliyoelezwa, katika ngazi ya Mkoa na katika ngazi ya Wizara, basi iliyopewa mamlaka hayo ni Kamati ya Uongozi, na kweli kuna mapungufu katika zile sheria. Kwa mfano, hata hiyo ya Kamati ya Uongozi lakini ni moja katika eneo ambalo limezingatiwa kwa ajili ya kufanyiwa marekebisho.

Labda la mwisho kabisa Mhe. Naibu Spika, ni lile suala la tafsiri ya Mwenyekiti, kwamba kwa nini tunajua Tume ya Mipango mwenyekiti ni Rais, lakini na pia tukaja na tafsiri ya Mwenyekiti.

Mimi niseme kwa kiasi kikubwa hilo si suala la kuwepo ile tafsiri au lisipokuwepo, kwa kweli inakuwa haiongezi wala haipunguzi kitu chochote, lakini ukweli utabaki kwamba, kama tume kwa wakati ule inaongozwa na mtu ambaye sio Rais basi hatuwezi kusema kwamba maamuzi haya yamefanywa, na bila ya kupata idhini ya Mwenyekiti kwamba hiki kikao hakikuwa na

Mwenyekiti au Tume haikuwa na mwenyekiti, ndio maana ya kuweka ile tafsiri. Hii ni kwamba, itakapotokea basi Rais hayupo lakini yupo mtu mwengine anayeongoza ama Tume au kikao. Kwa sababu wakati ule anaongoza kikao, yale maamuzi yakipita maana yake ni Tume, hatuwezi kusema kwamba pale hapakuwa na mwenyekiti, na ndio maana hiki kifungu kikawekwa.

Kifungu hiki mimi naweza nikakisema, kwamba labda ni kile kifungo cha shingo, kwa sababu shati zetu nyingi zina kifungo hapa juu lakini huwa hatukitumii, kimewekwa kwa sababu ndio utaratibu wenyewe kwamba inapotokea kuna haja ya kukitumia basi utakitumia pengine unapotaka kufunga tai utakitumia, lakini kipo sio lazima ukitumie, lakini inapotokea haja ili kuondoa utatanishi. Kwa hivyo, si suala la msingi, kikiwepo kisipokuwepo ni sawa sawa, lakini kimewekwa ili kusije kukatokea utatanishi na watu hawa wawili ni tofauti, Mwenyekiti ni mwenyekiti, na Rais naye ni Rais, haiwezekani kwamba Mwenyekiti wa Tume ya Mipango kwa sababu ni Rais akafanya kazi za Urais akiwa Mwenyekiti wa Tume ya Mipango, pale anakuwa na kofia nyengine na anapokuwa Rais ni kofia nyengine.

Kwa hivyo, huo ni utaratibu wa kawaida katika uandishi wa sheria ni kwa ajili ya kuondoa utatanishi pale ambapo unaweza ukaja ukajitokeza na hayo ndio madhumuni yake.

Mhe. Naibu Spika, nilikwambia la mwisho lakini niliombwa kuzungumzia kidogo suala la kiapo. Suala la kiapo mimi nimekubaliana naye Mhe. Ismail Jussa kwamba vile kilivyo sasa hivi kwenye hili jadweli kina mapungufu, na hili limeshaamuliwa kwamba lifanyiwe marekebisho, lakini kwa bahati mbaya nadhani lili*skip* ile *attention* ya hawa waliokuwa wakifanya marekebisho, lakini nakubaliana naye kwamba kama kilivyo kinahitaji kufanyiwa marekebisho.

Baada ya kusema hayo Mhe. Naibu Spika, na mimi niseme kwamba naunga mkono hoja, ahsante sana.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo: Mhe. Naibu Spika, kwa heshima na taadhima kwanza na mimi nataka nianze kama wenzangu walivyoanzia kwa kutoa pole kwa ndugu zetu wa Jimbo la Bububu, kwa msiba walioupata wa kupoteza Mwakilishi wetu tuliyempenda sana, lakini Mwenyezi Mungu alimuhitaji zaidi. Mwenyezi Mungu amlaze mahala pema peponi AMIN.

Lakini la pili, nataka na mimi nimpongeze sana Mhe. Mohammedraza Hassanali Mohammedali. Mhe. Raza tumemuapisha leo na sote tunamfahamu uwezo wake katika kulitumikia taifa, kama Mhe. Ismail Jussa alivyosema, tutafanya naye kazi kama ni Mwakilishi na ni Mzanzibari, na ni Mtanzania kwa faida ya wananchi wetu wa Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, baada ya maelezo hayo ya utangulizi, sasa nataka nianze kwa kumshukuru sana Mhe. Abdalla Mohammed Ali (Makamo Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo) Mwakilishi wa Jimbo la Mkoani. Kupitia kamati yake kwa kweli wamenisaidia sana, kwa sababu taarifa waliyoiwasilisha kwa kiwango kikubwa imepunguza maswali na imeweza kuwapatia Waheshimiwa Wajumbe majibu yale ya msingi.

Mhe. Naibu Spika, nataka niwatambue basi kabla sijatoa ufafanuzi kifungu kwa kifungu wale wote waliochangia kwa kusema, na wale wote waliochangia kwa maandishi kama kawaida yetu.

1. Nataka nimpongeze na nimtambue Mhe. Abdalla Mohammed, Makamo Mwenyekiti wa Kamati.
2. Mhe. Mahmoud Mohammed Mussa
3. Mhe. Rashid Seif Suleiman
4. Mhe. Saleh Nassor Juma, Mwanamapinduzi
5. Mhe. Ali Abdalla Ali
6. Mhe. Asaa Othman Hamad
7. Mhe. Suleiman Hamad Khamis
8. Mhe. Abdalla Juma Abdalla
9. Mhe. Ismail Jussa Ladhu
10. Mhe. Ali Mzee Ali
11. Mhe. Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

Halikadhalika Mhe. Naibu Spika, nataka nimtambue yule aliechangia kwa maandishi naye ni Mhe. Fatma Said Mbarouk.

Mhe. Naibu Spika, baada ya kutambua wale wote waliochangia nataka nitoe maelezo ya msingi au ya ujumla, na baadae niende katika vifungu ambavyo vimetakiwa kutolewa ufafanuzi.

Mhe. Naibu Spika, kwanza nataka tujiulize kwa nini tumeleta Sheria hii ya kuwa na Tume ya Mipango? Jibu lake ni kwamba, Tume imetambuliwa ndani ya katiba na ni taasisi chache ambazo Baraza hili tumezitungia sheria zimetambuliwa ndani ya katiba, tume ni moja wapo. Katiba yetu ya mwaka 1984 kifungu nambari 125 imeitambua Tume ya Mipango. Kwa hivyo, ilikuwa ni wajibu wetu kama wawakilishi wa wananchi, watunga sheria, tutunge sheria ya Tume. Lakini wengine wanaweza kujiuliza kwani Sheria ya Tume si ilikuwepo? Prof. Ali Mzee Ali ametoa ufafanuzi kidogo na mimi nataka nijalizie, sheria iliyokuwepo imepitwa na wakati. Sheria ile tuliiunda wakati Serikali ndie muandaaji wa mipango, serikali ndie anayeuza kila kitu na ndie anayenunua kila kitu. Leo tumefungua milango, tumeshirikisha sekta binafsi, tumeshirikisha taasisi zisizo za kiserikali, tumeona ni vyema kuwa na utaratibu wa kuwa na sheria mpya, ambayo itatoa nguvu zaidi kwa ushirikishaji wa sekta mbali mbali katika kukuza uchumi, na katika mipango yetu ya kitaifa.

Mhe. Naibu Spika, wengi wamezungumzia kuhusiana na muundo wa Tume, sitaki niongezee zaidi Mhe. Mwanasheria Mkuu namshukuru sana ametoa ufafanuzi wa kina. Katiba yenyewe inasema Tume ni chombo cha juu, unapomuondoa Rais, utakayemuweka yeyote yule kitakuwa sio chombo cha juu. Kwa sababu mamlaka atakuwa nayo Rais ambaye anakabidhiwa ushauri na Tume, kwa hiyo Rais naye atakuwa na haki ya kuelekeza na kutoa mapendekezo yake baada ya kukabidhiwa na Tume. Kwa hivyo, kitakuwa sio chombo cha juu tena, lakini utakapomuweka Rais kukiongoza chombo hicho kitakuwa na manufaa mawili makubwa. Kwanza Rais atafahamu moja kwa moja yale maelezo ambayo yanayotolewa na Wajumbe wa Tume, kutakuwa hakuna haja ya taarifa kuwa ni sekondari, atapata taarifa moja kwa moja.

Vile vile kutakuwa hakuna mtu mwengine wa juu ambaye atakuja kuya-*question* yale maamuzi ya Tume, ndio sababu za msingi pamoja na zile ambazo Mwanasheria Mkuu amezieleza. Huo ni uzoefu uko kila pahala katika dunia na ndio maana na sisi tumesema tusiende mbali na uzoefu

wa nchi za wenzetu. Tunaelewa Rais ana majukumu mengi, lakini hili ni jukumu moja kubwa zaidi kwa Rais kuangalia mipango ya nchi hii, hilo ni jukumu la kwanza la Mhe. Rais, ndio maana tukamuweka pale awe ni Mwenyekiti.

Mhe. Naibu Spika, kwa heshima yako sasa naomba kidogo nianze kutoa ufafanuzi kwa baadhi ya maeneo ambayo yaliyoulizwa na Waheshimiwa Wajumbe, nikianza na Makamo Mwenyekiti. Makamo Mwenyekiti ameeleza na mimi nakubaliana naye kwamba, tuwe na mipango mizuri yenye kutekelezeka, na ndio maana tumefanya maamuzi ya kuwa na Tume kama alivyosema Mwanasheria Mkuu, na kuwa na Sekretarieti ya Tume ndio itakayofanya kazi za kila siku za Tume, na ile tume itakuwa inakutana kwa vikao. Kwa hivyo, kuwa na tume lazima kuwe na mipango ambayo inayotekelezeka, nakubaliana na hili kabisa na ni wajibu wa sekretarieti ya tume kuipa mipango tume inayoweza kutekelezeka.

Mhe. Naibu Spika, vile vile Makamo Mwenyekiti amesema tume hii isiwe ya kisiasa, nadhani tunatazama watu zaidi kuliko kutizama chombo zaidi. Katiba inazungumzia chombo, na hata hao unaowaona wewe kama leo ni wana siasa ni wataalamu kwa upande wao. Lakini unapojadili mipango ya kitaifa wanatakiwa waijadili kitaalamu zaidi ndio maana ya Tume.Tume ni chombo cha kitaalamu hivyo wanatakiwa waijadili kitaalamu zaidi sio kisiasa. Na hili nakubaliana nae kabisa Mhe. Makamo Mwenyekiti.

Mhe. Naibu Spika, shemegi yangu Mhe. Mahmoud Mohammed Mussa ameeleza tatizo la ukusanyaji wa mapato, hili ni jukumu moja la Tume. Tume wana kitengo cha Sera na Kodi, katika ile sekretarieti ya tume kuna Kitengo cha Sera na Kodi, kazi yao moja ni hii, kuhakikisha kwamba mapato ya nchi yetu yanakusanywa kwa mujibu wa sheria, kwa mujibu wa taratibu na kwa mujibu wa kanuni za nchi yetu. Pia wanahakikisha kwamba vyombo vilivyopewa kazi ya kukusanya mapato vinaelekezwa mianya yote ili kuiziba mianya hii, sisi viumbe ni wazito sana, ukiziba hapa basi anazibua huku. Lakini ni dhahiri kwamba kazi moja ambayo tutatakiwa wajumbe wa Tume kupitia Sekretarieti yetu tuhakikishe kwamba mianya hii inazibwa.

Mhe. Naibu Spika, nataka nimshukuru sana shemegi yangu kwa hili na wapo waheshimiwa wengine wamelizungumzia suala la kuvuja kwa mapato, Mhe. Jussa naye amelizungumzia tutalifanyia kazi kadri ya uwezo wetu. Mhe. Naibu Spika, pia tutashirikiana kwa ukaribu zaidi na wananchi wetu pamoja na viongozi wetu na wataalamu wengine kutoa miongozo juu ya kuziba mianya ya mapato.

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Mahmoud amesema vile vile kwamba tufanye marejeo basi sheria zinazohusiana na mapato, nataka nikubaliane nae tunazifanyia marejeo sheria mbali mbali ili tuje tuzibe huu uvujaji wa mapato, na hivi karibuni tu tutaanza kuziwasilisha moja baada ya moja na ikiwemo ule utaratibu mzima wa mapato yanayovuja kutokana na mafuta, nalo tunalifanyia kazi.

Mhe. Rashid Seif Suleiman kwanza nampa pole siku mbili tatu alikuwa amelazwa nampa pole kwa hilo ndio mitihani ya Mwenyezi Mungu. Yeye amezungumzia muundo zaidi Mhe. Mwanasheria Mkuu ameuelezea kwa ufasaha zaidi na nina imani kubwa kwamba ameufahamu. Vile vile amezungumzia tofauti baina ya mswada huu wa kiswahili na ule wa Kiingereza. Nataka nimuhakikishie kwamba kwenye kamati tulikubaliana kwamba tuumalize na ule wa Kiswahili tuuweke sawa, halafu wanasheria tukakubaliana nao kwamba wautazame na ule wa Kiingereza

ili nao waweze kuuweka sawa. Kama kuna maeneo ambayo kidogo yana tofauti kilugha basi na hayo vile vile nataka nimuhakikishie yatawekwa sawa kabla ya Mhe. Rais hajatia saini.

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Saleh Nassor Juma naye vile vile amezungumzia kuhusiana na muundo wa Tume. Mhe. Mwanasheria Mkuu ameuelezea kwa ufasaha zaidi na mimi nataka nimwambie tu kwamba hakuna hata mmoja katika wajumbe hawa waliopendekezwa kuanzia Mhe. Rais, Makamo wa Kwanza, Makamo wa Pili ambaye *by profession* hatoitumia ile *profession* yake. Wazungu wanasema kwamba ameingia kwenye siasa *by default* lakini hawa ni ma-*profession,* Dk. Ali Mohammed Shein ana *profession* yake, Maalim Seif Sharif Hamad ana *profession* yake na Balozi Seif Ali Iddi ana *profession* yake. *Leave alone* mimi waziri niliyetajwa wa Fedha nina *profession* yangu. Kwa hivyo, tunaingia humu tuna *profession* zetu, tutaheshimu katiba inavyotutaka tufanye kwa kutumia utaalam, hatutotumia utashi wa kisiasa. Mipango ya nchi, uchumi wa nchi unahitajia zaidi utaalam kuliko siasa.

Mhe. Ali Abdalla Ali (Naibu Spika) ametaka ufafanuzi baadhi ya vifungu. Nataka niwambie kwamba kuna baadhi ya vifungu ambavyo ametaka ufafanuzi Mwanasheria Mkuu amevitolea maelezo hasa kile cha maadili tumekubaliana kwamba wote watafuata maadili, ile sentensi ambayo inayowaengua baadhi tutaiondoa ili wote waweze kufuata maadili.

Nataka vile vile nataka nimwambie Mhe. Ali Abdalla Ali aligusia kifungu cha 16 kuhusiana na takwimu zinazozalishwa na taasisi zisizo za kiserikali. Taasisi nyingi zinazalisha takwimu lakini mratibu wa takwimu hizi vipi zitumike kitaifa ni Tume ya Mipango. Huwezi kila mmoja akaleta takwimu yake halafu hizi kazi zinatumika tu kwa mipango ya taifa bila ya kuratibiwa. Lakini Tume ya Mipango nayo atalazimika kutoa miongozo kwa taasisi hizi ili wazalishe takwimu sahihi ambazo zitaweza kutumika kwa manufaa ya nchi yetu. Vyenginevyo tutakuwa tuna takwimu *cabbage in cabbage out.* Kwa hivyo, Tume ya Mipango ndio itakayosimamia uratibu wa hizi takwimu ambazo tunazozitumia katika kupanga mipango yetu.
cabage
Lakini vile vile Mhe. Ali Abdalla Ali alitaka kuelewa motisha. Mhe. Naibu Spika, pahala popote pale ili watendaji waweze kufanya kazi vizuri kuna haja ya kuangalia motisha zao. Tume hii itaangalia motisha za watendaji wake. Kwa mfano, ile kunitambua tu inatosha Omar Yussuf Mzee umefanya kazi vizuri, kunipa ile *certificate* tu kwamba nimefanya kazi vizuri inatosha, ni motisha. Wengine watafarnya kazi zaidi ili na wao mwaka kesho wapate kutambuliwa.

Lakini vile vile ile kunitambua jitihada zangu lakini ukaniona kwamba kinachonikwaza sina elimu ya kutosha kunambia sasa mwaka kesho nakupeleka ukasome *Bachelor of Science* au ukafanye *Masters.* Ile kunipa mafunzo tu ni motisha, kwa hivyo kuna motisha za aina nyingi ambazo tume itaziangalia wa watendaji wao zaidi ya ile motisha ya mishahara na nyongeza zake. Kwa hivyo, hizi ndizo ambazo tulizozikusudia katika utaratibu wetu.
Mhe. Assaa Othman Hamad amesema tungepatiwa semina zaidi kwa ajili ya huu mswada. Nataka niseme tu kwamba wazo la Mhe. Assaa ni zuri, lakini nataka nimkumbushe kwamba sehemu ya semina kwa ajili ya mswada huu ni ile ambayo tuliyofanya wikiendi iliyopita Pwanimchangani. Nina imani kwamba Mhe. Assaa alikuwepo katika semina ile na akawa msikivu na amefahamu masuala ya MKUZA, masuala ya Mipango, masuala ya Uchumi na nina imani kwamba amebobea lakini labda alikuwa anahitajia zaidi. Basi niseme tu Mwenyezi Mungu

akitujaalia akituwezesha tutakuwa tunaelimishana zaidi, tutafanya semina zaidi ili kila mwakilishi aweze kufahamu na kuweza kuwasaidia wananchi wake anaowaongoza.

Mhe. Assaa Othman Hamad amezungumzia vile vile muundo kama nilivyosema Mhe. Mwanasheria Mkuu ameshautolea maelezo na amekuwa na wasi wasi kwamba tafiti zitakazopelekwa kwenye tume kwa kuwa wapo wanasiasa labda zinaweza kupelekwa kisiasa siasa. Nataka nimwambie tu asiwe na wasi wasi huo kwa sababu utafiti wote unafanywa kwa mujibu wa *professionalism* na agenda ya ule utafiti uliokusudiwa. Sidhani itaendeshwa kisiasa kwa sababu tafiti nyingi zinakuja na matokeo ya ule utafiti na huwezi ukabadilisha matokeo ya utafiti zaidi ya kutoa mapendekezo yako nini cha kufanya katika suala lile. Lakini vile vile nataka niseme tutayazingatia zaidi ili maamuzi ya utafiti basi yaendeshwe kitaalam zaidi.

Mhe. Suleiman Hemed Khamis nae vile vile amezungumzia kuhusu habari ya muundo. Nataka niseme kwamba Mhe. Mwanasheria Mkuu amelitolea ufafanuzi wa kina juu ya muundo na juu ya chombo cha kitaalam lakini mawazo yake nayo tumeyachukua.

Mhe. Abdulla Juma Abdulla nae vile vile alisema hawa watumishi ambao sio wa kisiasa ni wepi. Akisoma kile kifungu ataona kwamba kuna wateuliwa pale ambao Rais anaweza akawateua. Mwanasheria Mkuu amelitolea ufafanuzi hawa wanaweza wakawa si wanasiasa anaweza akatoa wataalam tu kwa hivyo alitaka kuelewa ni wepi.

Suala la kula kiapo Mhe. Mwanasheria Mkuu ameelezea kile kiapo tumekifanyia marekebisho lakini kimsingi hichi ni kiapo cha kuwa mjumbe wa tume na kutekeleza majukumu ya tume. Mimi nimeapishwa Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi, nikaapishwa na kiapo cha Waziri, sijaapishwa kiapo cha Tume. Kwa sababu Marais wetu kiapo wanachokiapa wao wanaapa kiapo kwa kutekeleza kila kitu ndio tukasema hawa wao wasiape. Ndio kwa maana unamuona Maalim Seif Sharif Hamad Makamo wa Kwanza wa Rais, Balozi Seif Ali Iddi Makamo wa Pili wa Rais wanaingia Kilimo, wanaingia Elimu, wanaingia Afya, wanaingia Mazingira kwa sababu kiapo chao cha kutekeleza kila kitu kutokana na majukumu yao. Sisi wengine sio kutekeleza kila kitu una eneo lako la utekelezaji.

Mhe. Naibu Spika, mimi nilipoapishwa dhamana zangu ni Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo, ukinitaka niende kwenye Kilimo Mhe. Rais lazima aniteue kukaimu Wizara ya Kilimo siwezi kwenda. Hapa ndio kwa maana tukasema wacha sote tule kiapo cha kuwa Wajumbe wa Tume tutekeleze majukumu ya Tume.

Mhe. Abdulla Juma Abdulla vile vile amezungumzia kuachana na mapato kuvuja nimetoa ufafanuzi na tutajitahidi ili hili liwe ni jukumu la kipaumbele la Tume katika kufanikisha lengo letu.

Mhe. Naibu Spika, kwanza nakubaliana na Mhe. Ismail Jussa Ladhu kwamba Tume ni chombo muhimu kimekusudia kuleta mageuzi na *inshaallah* tutaleta mageuzi. Tume imekusudia kufanya kazi zake kwa kuangalia *vision* 2020 dira yetu ambayo imetengenezwa na wananchi wenyewe. Kuangalia MKUZA ambao umetengenezwa na wananchi wenyewe na nina imani kwamba haya ndio yatakuwa misingi ya utekelezaji wa majukumu ya Tume. Mhe. Jussa tutatekeleza mipango kama vile ulivyotoa tafsiri tutaangalia nini tutekeleze kwanza kwa faida ya watu wetu, nini

tutekeleze baadae kwa maslahi yetu sote. Hilo nakuahidi ndugu yangu sheria hii ikipitishwa Mhe. Rais akiitia saini na mimi nimeula ni Mjumbe wa Tume kwa mujibu wa *portfolio* niliyopewa.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu vile vile ametaka ufafanuzi juu ya *definition* ya Mwenyekiti, Mwanasheria Mkuu ameitolea maelezo na sina haja kurudia. Lakini vile vile amesema kwa nini tunawa-*restrict* Wajumbe wa Tume miaka mitatu. Ukisoma kile kifungu kinasema wanaweza kuteuliwa tena kwa kipindi chengine. Hii ina maana kwamba kama mjumbe umemuona hakutumikii vizuri usikae nae mpe nafasi aondoke aingie mwengine ambaye anaweza kukutumikia vizuri. Kama yupo mjumbe ambaye anaitumikia tume vizuri mpe nafasi aendelee kwa kipindi chengine.

Nafikiri mawazo yake Mhe. Jussa ndio mawazo ambayo ya mswada huu.
Hata akimaliza kipindi hichi bado ana nafasi waziri kumpendekeza kuwa ni mjumbe wa timu ya wataalam atasaidia katika kamati ya wataalam. Kwa hivyo, bado nafasi hii ipo na mimi nitakuwa karibu zaidi na wewe ili tuweze kusaidiana katika masuala haya.

Nadhani Mhe. Ismail Jussa Ladhu ameuliza kwamba tunamshauri Rais wakati yeye ni Mwenyekiti na ni sehemu ya Tume. Anapokaa pale ni kwa sababu tu amevaa koti, pale anapokaa kwenye Tume ni Mwenyekiti na unapomu-*address* pale ni Mwenyekiti. Nitatoa mfano mzuri.
Mhe. Naibu Spika, umekaa juu hapo naku-*address* Naibu Spika, ukikaa kule nitaku-*address* Mwakilishi. Kuna uzito tofauti, atakapokaa hapa ni Mwenyekiti lakini baadae tume hii inatakiwa sasa imuandikie Rais ili Rais apeleke maelezo ya Tume kwenye Baraza la Mawaziri. Hapo ni vitu viwili tofauti.

Kwa hivyo, mimi nataka kusema kwamba kama alivyosema Mwanasheria Mkuu na alivyosema Mhe. Ali Mzee Ali bado nafasi ya Rais kuwa ni Mwenyekiti ni nzuri zaidi kwa sababu hata kule anakoipeleka utenguaji utakuwa ni mdogo zaidi kuliko hata ukisema kwamba awe ni Mwenyekiti mtu mwengine.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu ametaka kufahamu kwamba kufuatilia na kuratibu miradi ya maendeleo hakutaleta mgongano baina ya Tume na Taasisi nyengine kama *ZIPA*. Nasema hakuleti mgongano, Tume itafuatilia miradi ya maendeleo wale *ZIPA* wanafuatilia miradi ya wawekezaji. Ile zaidi ni *private*, hawa zaidi ni *public*, hawa ndio ambao wanaotumia fedha za umma. Tumeona hapa Baraza linaidhinisha miradi, linaidhinisha fedha, Tume kabla Baraza hamjarudi wao wanatakiwa waanze kufuatilia ile miradi. Mmeidhinishiwa fedha, mmeidhinishiwa kutengeneza kilomita 13, leo mpaka wakati huu mmetengeneza kilomita 5 sababu zipi za msingi.

Lakini kule *ZIPA* nako kama kuna *interest* ya taifa *distortion* ya mazingira kwa miradi ya binafsi Tume hii hii tutaiagiza ifuatilie. Kwa hivyo, hakutakuwa na maingiliano katika sehemu hii, wao watafuatilia *implementation* za miradi ya sekta binafsi ambayo serikali haina fedha zake zinazoweza kupotea. Lakini tukitaka kuituma Tume hii nayo tutaipa maelekezo kufanya jukumu hilo kwa interest za taifa.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu pia alitaka kujua ushirikiano wa kiuchumi wa kikanda tutafanyaje wakati hatuna mamlaka. Nataka niseme tu Mhe. Naibu Spika, katika masuala ambayo sio ya

kimuungano tuna mamlaka kamili. Serikali ya Muungano wakipata taarifa ya mashirikiano ya kikanda wakiliona hilo suala Zanzibar sio la kimuungano wanaishirikisha Zanzibar. Hapa Zanzibar wataalam wetu wanakaa ndani kwanza wanalichakacha lile suala baadae wanakwenda wataalam wetu kukaa na wataalam wa Tanzania Bara baadae kutoa msimamo wa pamoja katika kushirikiana kikanda. Tatizo inawezekana limo ndani ni *communication,* inawezekana sekta moja ikapata suala wakadhani kwamba hilo suala ni lao peke yao wakasahau kwamba hilo ni suala la kiserikali la kitaifa zaidi kwa hivyo wakasahu kushirikisha wengine. Lakini ushirikishwaji na kutoa maoni yetu na ushiriki wetu tunakwenda kwenye mikutano kwa sababu wenzetu wanajua kwamba hii mikutano inahusika na Zanzibar tunakwenda tunawakilisha na sisi tumo humu ndani.

Mfano mzuri Kamati yetu ya Mahesabu ya Umma *(PAC)* inakwenda kwenye mikutano inashiriki kwa sababu wanajua wenzetu kwamba hii ina majukumu katika fedha za Zanzibar. Kitu muhimu nasema ni mawasiliano, mawasiliano yanapokuwa mazuri tutakwenda vizuri, mawasiliano yakiwa mabaya tutakwenda vibaya. Naomba mawasiliano yawe mazuri na namuomba sana Mhe. Ismail Jussa Ladhu katika eneo hili yeye yupo karibu zaidi na mimi kunipa baadhi ya taarifa tuendelee kupeana taarifa hasa ulivyokuwa wewe ni mwakilishi wangu.

Suala la Kamati ya Kitaalam na suala la Sekretarieti Mhe. Mwanasheria Mkuu amelizungumza vizuri sana na suala la kiapo pia ameshasema kwamba tutakifanyia marekebisho ili kukidhi ile haja kwa sababu tulikuwa tumeshazungumza lakini kwa bahati tu ndio tulikuwa hatujawahi kukifanyia marekebisho.

Mhe. Naibu Spika, suala la dhamana ya mradi Mhe. Ismail Jussa Ladhu, Mhe. Mwanasheria Mkuu wamelizungumza na mimi nataka nilisisitize. Mikoa ndio itakayoidhinisha mipango yao ya Mikoa yao, Wizara itaidhinisha mipango yake ya Wizara ikisha yote inakwenda Tume. Mmeidhinisha kwamba hii ndio mipango ambayo tunayoihitaji sisi kutekeleza ikisha inakwenda Tume, Tume sasa wao ndio watakaoiangalia kwa umoja na kuidhinisha mpango wa taifa. Kwa hivyo, hapa *responsibility* kwa mujibu wa sheria hii. Vyenginevyo mtaipa jukumu Tume ikae peke yake na kujifungia peke yake hili ndio tunalolikataa, tunataka ushirikishwaji wa wenza taasisi nyengine zishirikishwe ili ziweze kuandaa mipango yao na kuipeleka Tume.

Mhe. Ali Mzee Ali kwanza nataka nikushukuru kwa pongezi, nataka nikushukuru kwa kutoa historia yangu, sikushangaa kumuona Mhe. Ali anatoa historia yangu kwa sababu huyo ni kaka yangu ananijua sana. Inawezekana Mhe. Ismail Jussa Ladhu kashangaa lakini mimi sikushangaa. Nakushukuru sana kwa pongezi, nakushukuru sana vile vile kwa kutoa ufafanuzi juu ya muundo na kuwaomba Wajumbe tumuache Rais aiongoze hii Tume kwa faida yetu.

Nakushukuru sana kwa kueleza utaalam walionao viongozi wetu wale na mimi nimesisitiza kwamba viongozi wetu wale watatu wana utaalam wa kutosha. Kwa hivyo, nakushukuru sana kwa hayo na nakuomba na wewe tuendelee kushirikiana umenisaidia sana kutoa ufafanuzi katika baadhi ya maeneo mengi.
Mhe. Naibu Spika, Mhe. Mwanasheria Mkuu kwa kifupi yeye hakuniuliza masuala mengi isipokuwa amesaidia kutoa ufafanuzi. Kwa hivyo, nakushukuru sana Mhe. Mwanasheria Mkuu kwa ufafanuzi ulioutoa.

Mhe. Naibu Spika, wa mwisho Mhe. Fatma Mbarouk Said ambaye amechangia kwa maandishi. Kwanza nataka nimpongeze sana Mhe. Fatma nimesikiliza kwa makini sana, Waheshimiwa Wawakilishi kila mmoja alikuwa na hoja zake nzito. Hoja kubwa ya Mhe. Fatma ameiomba Tume iwe ni chombo cha kutoa elimu kwa wananchi juu ya uchumi na maendeleo yake.

Nakupongeza sana kwa hili na mimi nitaiambia sekretarieti kwamba hili walichukue. Wananchi wanataka kujua uchumi wao unakuwaje, wananchi wanataka kujua ni maeneo yepi yanayochangia zaidi. Kwa hivyo, ni vyema tukalifanyia kazi pamoja.

Lakini amekuwa na wasi wasi na yeye amesema kujitegemea huko kwa Tume na wakati wapo wanasiasa mle ndani watajitegemea vipi. Wala usiwe na wasi wasi kila akiwepo kiongozi mkubwa zaidi katika kamati yenu au katika tume yenu ndio mnaweza mkajitegemea zaidi. Usiwe na wasi wasi tume hii itakuwa inajitegemea, tume hii itakuwa ina mfuko wake, tume hii itakuwa na bajeti yake, tume hii itakuwa na Katibu Mtendaji wake ambaye atafanya maamuzi ya siku kwa siku kwa kushirikiana na idara zake na sekretarieti kwa ujumla.

Mhe. Naibu Spika, kwa kumalizia nataka niwashukuru wajumbe wote michango yao ni dhahiri kwamba mimi pamoja na wenzangu tumefarajika sana. Naomba niseme nia yangu ilikuwa ni kujibu hoja moja baada ya moja kama kuna mwakilishi ambaye hoja yake sikuijibu sio kwa sababu nimedharau kwa sababu tu labda sikuipata vizuri na namuomba radhi. Lakini kwa sababu tuko pamoja tutaendelea kuwa pamoja wiki mbili hizi tuko hapa wakati wowote anaweza kuja tukasaidiana katika kutoa ufafanuzi. Lengo ni kumfanya yeye mwakilishi afahamu na hatimaye kuwasaidia wananchi wake katika jimbo lake.

Mhe. Naibu Spika, baada ya maelezo hayo sasa naomba kutoa hoja.

Mhe. Naibu Spika: Sasa niwahoji Waheshimiwa Wajumbe wanaoafiki hoja aliyotoa Mhe. Waziri wanyooshe mikono, wanaokataa, waliokubali wameshinda.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo: Mhe. Naibu Spika, sasa naomba kutoa taarifa kwamba Baraza lako tukufu likae kama Kamati ya Baraza Zima ili kuupitia mswada kifungu baada ya kifungu. Naomba kutoa hoja.

KAMATI YA BARAZA ZIMA

Mswada wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Tume ya Mipango Nam. 5 ya Mwaka 1989 na Kutunga Sheria Mpya kwa ajili ya uendeshaji wa Tume ya Mipango Zanzibar

SEHEMU YA KWANZA
UTANGULIZI

Kifungu cha 1 - Jina fupi na kuanza kutumika.
Kifungu cha 2 - Ufafanuzi.

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Baraza Zima bila ya mabadiliko yoyote)

SEHEMU YA PILI
KUANZISHWA, KAZI NA UWEZO WA TUME

Kifungu cha 3 - Tume ya Mipango.
Kifungu cha 4 - Muundo wa Tume.
Kifungu cha 5 - Maadili kwa Wajumbe.
Kifungu cha 6 - Katibu wa Tume.
Kifungu cha 7 - Kiapo cha Utiifu pamoja na marekebisho yake.
Kifungu cha 8 - Kazi za Tume.
Kifungu cha 9 - Uwezo wa Tume.
Kifungu cha 10 - Kukasimu Uwezo.
Kifungu cha 11 - Mipango ya Maendeleo ya Kitaifa.
Kifungu cha 12 - Kuratibu Mipango ya Maendeleo ya Kisekta.
Kifungu cha 13 - Tume kama chombo cha kitaalamu.
Kifungu cha 14 - Kufuatilia na kutathmini.
Kifungu cha 15 - Mipango ya rasilimali watu na demografia.
Kifungu cha 16 - Usimamizi wa Takwimu.
Kifungu cha 17 - Sekretarieti.
Kifungu cha 18 - Kazi za Sekretarieti.
Kifungu cha 19 - Uteuzi wa Wakuu wa Idara.
Kifungu cha 20 - Wafanyakazi wa Tume.
Kifungu cha 21 - Uhusiano na Ushirikiano.

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Baraza Zima bila ya mabadiliko yoyote)

SEHEMU YA TATU
UTENDAJI WA TUME

Kifungu cha 22 - Uwezo wa Tume kuhitaji taarifa.
Kifungu cha 23 - Mawasiliano kwa Tume.

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Baraza Zima bila ya mabadiliko yoyote)

SEHEMU YA NNE
MWENENDO WA VIKAO VYA TUME

Kifungu cha 24 - Vikao vya Tume.
Kifungu cha 25 - Uamuzi wa Tume.
Kifungu cha 26 - Kumbukumbu za Mkutano wa Tume.

Kifungu cha 27 - Mafao na Posho za Wajumbe wa Tume.

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Baraza Zima bila ya mabadiliko yoyote)

SEHEMU YA TANO
MASHARTI YA FEDHA

Kifungu cha 28 - Fedha za Tume.
Kifungu cha 29 - Makisio.
Kifungu cha 30 - Hesabu na Ukaguzi.

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Baraza Zima bila ya mabadiliko yoyote)

SEHEMU YA SITA
MASHARTI MBALI MBALI

Kifungu cha 31 - Kuanzishwa kwa Kamati za Idara.
Kifungu cha 32 - Kanuni.
Kifungu cha 33 - Kufutwa kwa Sheria Nam. 5 ya 1989 na kubakiza.

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Baraza Zima bila ya mabadiliko yoyote)

(Baraza lilirudia)

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo: Mhe. Naibu Spika, ilivyokuwa Kamati ya Baraza Zima imeupitia mswada wangu kifungu baada ya kifungu na kuukubali pamoja na masahihisho sasa naliomba Baraza lako tukufu liukubali. Naomba kutoa hoja.

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe niwahoji wale wanaokubali hoja ya Mhe. Waziri wanyooshe mikono, wanaokataa, waliokubali wameshinda.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mswada wa Sheria ya Tume ya Mipango ya Zanzibar ya Mwaka 2012

(Kusomwa mara ya pili)

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo: Mhe. Naibu Spika, naomba kutoa hoja kuwa Mswada wa Sheria ya Tume ya Mipango ya Zanzibar ya Mwaka 2012 usomwe kwa mara ya pili.

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe niwahoji wale wanaokubali hoja ya Mhe. Waziri wanyooshe mikono, wanaokataa, waliokubali wameshinda.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

(Mswada wa Sheria ya Serikali ulisomwa mara ya pili na kupitishwa)

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe nichukue nafasi hii kwanza kumshukuru Mhe. Waziri na wataalam wake kwa kuleta mswada mzuri na kwa wakati. Pia niwashukuru Waheshimiwa Wajumbe waliopata nafasi ya kuchangia na wasiopata nafasi ya kuchangia ambao wameweza kuunga mkono mswada huu. Kwa hiyo, nawashukuru sana nawatakia kila la kheri na nawashauri tukasome mswada mwengine utakaowasilishwa kesho. Baada ya hayo machache naahirisha Baraza mpaka kesho saa tatu za asubuhi.

(Saa 1:00 usiku Baraza lililakhirishwa mpaka
tarehe 29/3/2012 saa 3:00 asubuhi)